Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Tano - Tarehe 19 Aprili, 2004**

*(Mkutano Ulianza saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni taarifa kuhusu Miswada iliyopitishwa na Bunge hili katika Mkutano uliopita wa Kumi na Nne. Taarifa ni kwamba, tulipitisha Miswada mitano katika Mkutano huo na yote sasa imeshapata kibali cha Rais na ni sheria za nchi. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (k. n. y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Baraza la Taifa la Kuhifadhi Mazingira *(NEMC)* kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2002 *(The Annual Report and Accounts of The National Environment Management Council (NEMC) for the Year ended 30th June, 2002).*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**: -

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Maendeleo ya Taifa *(NDC)* kwa Miaka ya 2001 na 2002 *(The Annual Reports and Accounts of the National Development Corporation for the Years 2001 and 2002).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 59

### Usumbufu wa Walimu Kufuata Mishahara Wilayani

**MHE. LUCAS L. SELELII (k. n. y. MHE. MGANA I. MSINDAI)** aliuliza: -

Kwa kuwa upo usumbufu mkubwa kwa Walimu wanaofundisha mbali na Wilaya wa kwenda kufuatilia mishahara yao Wilayani kila mwezi na hivyo kupoteza muda wa kufundisha kwa wastani wa siku 6 kila mwezi; na kwa kuwa Walimu wa Iramba Mashariki walishaanza kupokea mishahara yao Nduguti, kitendo kinachowasaidia sana Walimu hao kufanya kazi za kufundisha kwa makini zaidi; na kwa kuwa mwanzoni mwa mwezi huu, gari lililokuwa limewachukua Walimu waliotoka kuchukua mishahara yao lilivamiwa na majambazi kwenye eneo la kati ya Msungu na Gemanga na mtu mmoja aliuawa : -

(a) Je, hivi ni jukumu la nani kuhakikisha kwamba Walimu na Watumishi wengine wanalipwa mishahara yao karibu na vituo vyao vya kazi, ili kuokoa zile siku sita zinazopotea kila mwezi bila kufundisha na kuepusha uvamizi kama huo uliotokea ama kusababisha vifo?

(b) Je, ni kitu gani kilichosababisha mishahara ya Watumishi hao wa Serikali wanaofanya kazi Iramba Mashariki isipelekwe Nduguti na kama tatizo ni usalama; je, anayetakiwa kuhakikisha kuwa usalama upo ni mfanyakazi au ni Serikali?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuanza kupeleka mishahara ya Walimu/Wafanyakazi hao Nduguti au ianze kuwalipia Watumishi wote wa Serikali wanaofanya kazi Iramba Mashariki kupitia Benki ya *NMB* Singida ambako ni karibu na kwao kuliko *NMB* Kiomboi ambako ni mbali sana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi ni jukumu la Serikali na hasa Halmashauri kuhakikisha kwamba, Walimu na Watumishi wengine wanalipwa mishahara yao karibu na vituo vyao vya kazi. Kwa kuzingatia hilo, Serikali ilitoa agizo kwa Halmashauri la ulipaji wa mishahara kwenye Kata au Tarafa ili kuokoa siku ambazo Walimu na Watumishi wengine walikuwa wanapoteza kufuata mishahara yao Makao Makuu ya Halmashauri. Halmashauri zilitekeleza agizo hilo, lakini baada ya muda baadhi ya Halmashauri zilisitisha zoezi hilo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za usalama

wa fedha na Watumishi wenyewe na vile vile muda unaotumika kutegemea na ukubwa wa Wilaya katika kuzunguka kulipa hiyo mishahara.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu kubwa za kutopeleka fedha Nduguti katika Jimbo la Iramba Mashariki, nimezieleza katika kipengele (a), lakini kubwa zaidi ni lile la usalama wa fedha zenyewe na maisha ya Watumishi. Aidha, katika maeneo ya Nduguti kumekuwa na tishio la ujambazi ambapo wakati fulani gari lilivamiwa na majambazi maeneo kati ya Msungi na Gemanga na kusababisha kifo cha mtumishi mmoja. Kulingana na taratibu zetu, jukumu la kulinda mali na nchi kwa kweli ni la kila raia. Hivyo basi, raia wote pamoja na Serikali, wanatakiwa kuhakikisha kuwa usalama upo. Hata hivyo, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikihakikisha wakati wote usalama wa fedha na Watumishi. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kwa kweli kuwapongeza wenzetu wa Polisi kwa kazi nzuri wanayoitoa.

(c) Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali namba 11 la Mheshimiwa Hashim A. Z. Saggaf, Mbunge wa Dodoma Mjini, tarehe 11 Juni, 2003 nilieleza kwamba, Serikali imetoa maelekezo kuwa Watumishi wote wa Serikali wafungue akaunti Benki au Posta karibu na maeneo yao ya kazi ili mishahara yao ipitishiwe huko. Nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, mishahara ya Watumishi wa Serikali sasa imeanza kulipwa kupitia kwenye Mabenki mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba mishahara ilipwe katika Tawi la Benki la *NMB* la Singida badala ya *NMB* Kiomboi, itategemea akaunti za Watumishi hao zimefunguliwa katika Tawi lipi la Benki. Serikali hupeleka mshahara wa mtumishi mahali akaunti yake ilipo. Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuwa, awasiliane na Watumishi wote ambao wanaathirika kutokana na sababu hii ili waweze kufungua akaunti zao katika maeneo ambapo fedha zinaweza kupelekwa bila usumbufu. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunitambua.

(i) Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza jukumu la kupeleka fedha hadi kwenye Kata na Tarafa ni la Halmashauri ambayo ni Serikali, lakini kwa kuwa Watumishi hawa bado wanalazimika kwenda kwenye Halmashauri za Wilaya yaani Makao Makuu ya Wilaya kuchukua mishahara yao ambapo kumbe ingekuwa ni jukumu la Halmashauri na ambapo wanatumia fedha kwa ajili ya nauli, malazi na chakula. Je, Wizara iko tayari kuziagiza Halmashauri kuwalipa Walimu na Watumishi wengine ambao wanatumia fedha hizo ambazo Halmashauri ndiyo ingeweza kuzitumia?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba jukumu hilo la ulinzi na usalama ni la wote yaani raia pamoja na Serikali, pale inapotokea mtumishi ameibiwa pesa yake na majambazi; je, Serikali ipo tayari kufidia mshahara ule ambao uliibiwa kwa mtumishi ambaye ameathirika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, baadhi ya maeneo yako

mbali na Makao Makuu ya Halmashauri ambako Walimu na Watumishi wengine wanalazimika kufuata mishahara yao. Kama nilivyosema, nia ya Serikali ni nzuri na ndiyo maana tulitoa maagizo yale ya awali, lakini jambo hili litaendelea kutofautiana kati ya sehemu na sehemu kulingana na hali ya usalama ilivyo katika eneo linalohusika. Hata kama Halmashauri itabeba huo mzigo kwenda kulipa mishahara huko, lakini kama hali ya usalama hairidhishi ni lazima na wao watasitisha kwa sababu ni jambo ambalo sasa litakuwa limeongeza tatizo kuliko ilivyokuwa mwanzoni. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa kweli itabidi tuendelee kushirikiana kwa sababu hatuna jibu wala ufumbuzi wa moja kwa moja katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba mtumishi anapoibiwa afidiwe kutokana na gharama aliyoipata. Ninaloweza kusema hapa ni kwamba, Serikali hatuna utaratibu huo. Kwa hiyo, unakwenda kuchukua mshahara *at your own risk* na likitokea jambo kama hilo basi ni bahati mbaya.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu yaliyotolewa na Waziri ambayo yanaridhisha, lakini hoja ya swali ni kwamba, pia mishahara ya Walimu inachelewa sana kuwafikia. Kwa mfano, Jijini Mwanza Walimu wanapata mishahara yao kwa kuchelewa kwa zaidi ya siku 6 au 7. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba mishahara ya Walimu inawafikia mwisho wa mwezi sawa na Watumishi wengine wa Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, suala la kuchelewa mishahara katika baadhi ya maeneo inawezekana likawepo, lakini wote hapa ni mashahidi kwamba, maagizo yaliyokwisha kutolewa na Serikali ni yale ya kulipa mishahara hii ifikapo tarehe 25. Maagizo yalitolewa na Rais na Viongozi wote kwenye Halmashauri wanajua hilo. Sasa, ninaloweza kusema ni kwamba, kwa Mheshimiwa Stephen Kazi, kama *trend* hiyo inaonekana ndiyo mtindo kwa Halmashauri au Jiji la Mwanza, basi naomba sana tusaidiane tu ili tuweze kumsaidia kuweza kulikomesha mara moja kwa sababu kama ni kusema limesemwa sana. *(Makofi)*

Na. 60

**Njia za Waenda kwa Miguu Kati ya Majengo Jijini Dar es Salaam**

**MHE. ROSEMARY H. K. NYERERE** aliuliza: -

Kwa kuwa majengo mengi Jijini Dar es Salaam yana sehemu iliyoachwa kwa ajili ya wapita kwa miguu *(Pedestrians)* ambazo zinatenganisha sehemu ya kutembelea na barabara ya kupita magari na kwa kuwa hivi sasa maeneo ya waendao kwa miguu *(Pavements)* mengi yamezuiwa kwa minyororo/uzio na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa waendao kwa miguu na kwa kuwa katika majengo ya baadhi ya Ofisi za Balozi mbalimbali kama vile *Umoja House,* Denmark na kadhalika, kuna sehemu ya barabara

kwa ajili ya kupita kwa miguu *(Public Ways)* lakini zimewekewa minyororo/uzio unaowakwaza watembea kwa miguu: -

(a) Je, *pavements* hizo ni mali ya nani?

(b) Je, kisheria ni umbali gani unaotakiwa kati ya mpaka wa kiwanja/majengo na barabara?

(c) Je, Serikali inasema nini kuhusiana na usumbufu huo wanaoupata waenda kwa miguu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kambarage Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Sura ya 378, maeneo ya waendao kwa miguu *(walkways/pavements)* ni mali ya Serikali yanapokuwa kwenye bakaa la barabara *(Road Reserve).*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria za Miji Sura ya 101, umbali unaotakiwa kati ya jengo na barabara ni mita tatu ikiwa na maana ya jengo kuwa umbali wa mita tatu kutoka kwenye mpaka unaotenganisha kiwanja na barabara.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inakemea kuzibwa kwa njia ya waendao kwa miguu na kwa kweli kila itakapobainika itawachukulia hatua za kisheria wale wote watakaokuwa wametenda makosa hayo. Mfano mzuri ambao na yeye ameutoa ni ule uzio wa minyororo na vyuma uliokuwa umewekwa mbele ya jengo la Umoja wa Balozi za Ulaya, kandokando ya Barabara ya Mirambo, ambao baada ya kubanana waliuondoa. Kwa hiyo, Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam, zinaongeza na zinaendelea kufuatilia kwa karibu sana vikwazo vya aina hiyo popote pale vilipo ili kuweza kurejesha tena hali ya kiusalama kwa wale wote wanaotembea kwa miguu.

**MHE. ROSEMARY H. K. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa katika kipindi baada ya kuandika swali hili na kabla ya swali hili kusomwa hapa Bungeni, Balozi hizi zimeweza kutoa nafasi ya *pavements* kwa ajili ya watembea kwa miguu. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, ni vema tuwape pongezi Balozi hizi kwa kufanya hivyo?

(ii) Je, vyombo husika vitachukua hatua kwa sehemu zingine ambazo zimeziba *pavements* za watembea kwa miguu na kuzifunga kabisa kwa kufanya sehemu za maduka kama vile Mtaa wa Makunganya na maeneo ya Stesheni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ombi la Mheshimiwa Rosemary Nyerere la kuwapongeza hawa wakubwa, mimi nasita kwa sababu tumevutana vutana nao sana mpaka tukafikia pale tulipofikia. Kwa hiyo, walichokifanya ni baada ya shinikizo la kulia na kushoto ndiyo wakafanya hivyo na hata baada ya kuwa tumekubaliana hivyo, bado walitaka kujenga matofali ya zege kurudia jambo ambalo tulikuwa tumekwishalikataa. Kwa hiyo, kwa kweli nadhani ni vizuri tukasimama kidete tu, mtu yeyote anayevunja taratibu basi afanye marekebisho yanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Rosemary Nyerere kwamba, kwa hili swali la pili kwa kweli Halmashauri zote zimekwishaagizwa hivyo na tunadhania tutafanikisha kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, naomba labda ni-*caution* kidogo kwamba, inawezekana vile vile mtakuwa mmeona katika baadhi ya *walkways* tumeweka vizingiti. Hili linatokana na raia wakati mwingine kutokutaka tu kuheshimu sheria. *Pavements* zile hazitakiwi kuwa na vizingiti tulivyoweka, lakini ninyi nyote ni mashahidi, magari yanaacha barabara na hasa daladala. Kwa hiyo, tukisema kwamba, pamoja na kuhimiza sheria, lakini ni lazima tuhakikishe usalama wa raia unalindwa na ndiyo maana tumechomeka vizingiti katika sehemu nyingine ili kuzuia magari ya wakorofi yasipite huko. *(Makofi)*

Na. 61

**Barabara ya Chikuti - Lukande**

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA** aliuliza: -

Kwa kuwa Hifadhi ya Mbuga za Wanyama ya *Selous* Wilayani Ulanga ni pamoja na Vijiji vya Chikuti, Tarafa ya Vigoi na Kijiji cha Lukande kilichopo katika Tarafa ya Mwaya na kwa kuwa urefu wa barabara ya Chikuti - Mahenge - Mzelezi - Chirombora - Mwaya - Gombe hadi Lukande ni kilomita 66 lakini urefu toka Chikuti - Lukande ni kilomita 36: -

(a) Je, serikali iko tayari kufanya upembezi yakinifu ili kujua gharama ya kutengeneza barabara hiyo ya Chikuti - Lukande?

(b) Je, Wizara ya Maliasili na Utalii itakuwa tayari kushirikiana na Wizara ya Ujenzi ili kuifufua barabara hiyo ambayo kwa sasa hutumiwa na Wananchi wanaokwenda kwa miguu toka Chikuti - Lukande?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kupitia Menejimenti ya Pori la *Selous,* hutoa huduma ya kupitisha greda katika barabara zenye matatizo ya kupitika pale Wananchi wanapoomba. Kwa kuwa Vijiji vya Chikuti - Lukande vinapakana na Pori la Akiba la *Selous* na kwa kuwa Wizara inashirikisha Wananchi katika kuhifadhi wanyamapori na maliasili nyingine, hivi sasa Wizara yangu inafungua barabara inayounganisha Vijiji vya Chikuti hadi Mavimba kwa kukata miti na kung'oa visiki na hatimaye kupitisha greda.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inashirikiana na itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Halmashauri za Wilaya katika jitihada za kuwaondolea Wananchi kero ya usafiri katika maeneo yanayopakana na Mapori ya Akiba na Hifadhi za Taifa.

Aidha, Wizara yangu itaendelea kupokea ushauri wa kitaalam kutoka Wizara ya Ujenzi katika kuandaa mpango utakaowezesha kufufuliwa kwa barabara ya Chikuti - Lukande kwa kuwashirikisha Wananchi wa Vijiji husika kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga. Hivi sasa Wizara inatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Mahenge - Mbuga yenye urefu wa kilometa 51 kwa gharama ya Shilingi milioni 900 kutokana na uhisani wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* ambayo ipo katika Jimbo la Ulanga Mashariki.

Vile vile, napenda kumshauri Mheshimiwa Kasapira, awahamasishe Wananchi wa Chikuti na Lukande, waandae mapendekezo juu ya ufufuaji wa barabara hiyo kwa kuzingatia Sera ya Uhifadhi Shirikishi wa Maliasili. Wizara yangu itazingatia mapendekezo hayo katika maandalizi ya programu za uhifadhi katika Pori la *Selous* baada ya mradi wa ujenzi wa barabara ya Mahenge - Mbuga kukamilika.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Sasa hivi Wananchi wa Chikuti wanapita kwa miguu kwenda Lukande, Mifuko ya *TASAF* na Mfuko wa barabara Vijijini asilimia tunaipata kwa ajili ya uwindaji wa wanyamapori na wako tayari kuanza barabara hiyo. Naomba Mheshimiwa Waziri atamke kwamba yeye kama Waziri mhusika anatakiwa aanze ili vyombo vingine vimsaidie.

(ii) Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Machi, 2003 Mheshimiwa Waziri alitoa barua kwa maandishi kwamba anakuja Wilaya ya Ulanga kutatua matatizo ya akinamama ambao mpaka sasa wanaidai pesa Wizara yake. Sisi Viongozi wa Serikali tumemsubiri

Mahenge Mheshimiwa Waziri hakuonekana mpaka hivi sasa Wizara yake inalaumiwa sana Jimbo la Ulanga Mashariki...

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Je, Mheshimiwa Waziri analiambia nini Bunge hili pamoja na wale akinamama ambao aliahidi yeye mwenyewe kwamba anakuja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasapira anasema Waziri alitoa barua kwa maandishi, kwani kuna barua isiyokuwa na maandishi? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kusema Mheshimiwa Kasapira, atakubaliana nami kwamba, Wizara yangu imejitahidi sana katika barabara hizi za *Selous*. Kwa kweli ni mpango shirikishi kwa sababu wakati *ADB* ilivyokuja, mimi binafsi nilizungumza nao na wao hasa hasa nia yao ilikuwa kujenga nyumba zaidi za Watumishi, lakini tuliona kwamba kuna umuhimu wa kutengeneza barabara mbalimbali. Kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, kwa sababu wao walisema hii kazi ni ya Wizara ya Ujenzi, tulisema hapana, sera yetu ni ya kushirikisha Wananchi kwa hivyo walikubali. Kwa hiyo, fedha hizi ambazo zinatumika za *ADB* siyo za kujenga barabara yote, nataka kuliweka hili sawa. Ni kwamba, ni kwa kutengeneza barabara sehemu zile korofi. Pamoja na hayo ni kutengeneza maeneo ya kumwaga maji *(Drainage Systems)*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sitaweza hapa kutamka na kusema kwamba, tutashughulikia eneo hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge analieleza kwa sababu tayari hilo linafanyika, tungoje mpaka pale kazi hii itakapomalizika halafu ndiyo tutaweza kufanya hivyo, *otherwise* itakuwa tunajidanganya tu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kutofika siku ya tarehe 26, napenda nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, kwanza kabisa nilitoa tamko hapa Bungeni wakati najibu swali na ninataka kuweka wazi, ninanukuu *Hansard,* ilikuwa ni swali namba 47 la tarehe 6 mwezi wa pili, kutokea ukurasa wa 7 - 9, naomba ninukuu: "Napenda kusema kwamba, tathmini haitachukua muda mrefu kwa sababu kazi imeshaanzwa na inabidi iendelee, lakini tunazingatia mawazo aliyotoa Mheshimiwa Mbunge, ambaye yuko katika eneo hilo na mimi binafsi nitawaagiza watu wangu wafike huko na kuona kazi inavyoendelea." Watu wangu walifika, hapa mimi kwa kweli nilikuwa sikuahidi kulipa, naomba niseme hivyo. Lakini hata hivyo, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge alisema kwamba kuna watu ambao hawakulipwa na ni makubaliano ambayo ni kati ya *Mberu Construction* na wale Wananchi siyo Serikali, Serikali haikuhusika lakini *still* tukasema tufuatilie na katika kufuatilia baada ya majibu yangu kumekuwa na mabadiliko na ninayo hapa.

Mheshimiwa Spika, samahani sana kwa kuchukua muda mrefu ...

**SPIKA:** Endelea.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Lakini ni kwamba, kwa mfano deni la *cement* lilikuwepo na mhusika alikuwa ni Bwana Kitunga. Alikuwa anadai Shilingi milioni 13, amelipwa angalau Shilingi milioni 2 na *Mberu Construction.* Vibarua walikuwa wanadai Shilingi milioni 26 wamelipwa Shilingi milioni 10. Kokoto, mchanga na mawe walikuwa wanadai Shilingi milioni 8 wakalipwa Shilingi milioni 2.5. Magari, mitambo ilikuwa Shilingi milioni 40 na kadhalika. Hivyo, kwa kweli Serikali baada ya kutoka pale ilijitahidi. Lakini nasema ni suala ambalo ni la *Mberu Construction* na wale ambao ni wahusika na sisi tunazidi kulifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokuja kwangu siyo kwa makusudi, niliahidi nitakwenda na nilitaka kwenda, siyo kulipa lakini kuona hali inavyokwenda pamoja na mazungumzo mengine. Siku ile nilikuwa nimerudi kutoka safari ndefu, safari ambayo ilinichukua saa kama 20 na mabadiliko ya hali ya muda kutoka nchi hiyo kuja hapa. Kwa hiyo, nikaamka nikasema tutakwenda kwa ndege, lakini nikapata taarifa kwanza kwa watu wangu, lakini pia kutoka kule kule Ulanga kwamba, hali ya hewa ni mbaya sana kuweza kuruka na kutua katika kiwanja hicho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ajiandae kusafiri kwa safari ndefu ya gari. Kwa kweli mimi ni binadamu pia, ilikuwa vigumu sana kuweza kwenda kwa gari kwa wakati ule hata kama ningetaka na ndiyo maana nikaahirisha ile safari, siyo kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema na nimesema na nimeomba radhi Waheshimiwa Wananchi wa sehemu ile na Mheshimiwa Mbunge. Lakini ninamalizia kwa kusema kama vile anavyosema Mheshimiwa Kasapira, 'haijapata kutokea.' *(Kicheko/Makofi)*

Na. 62

**Vivutio vya Utalii**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k. n. y. MHE. FRANK G. MAGHOBA)** aliuliza: -

Kwa kuwa Tanzania inavyo vivutio vingi vya utalii kama wanyama, ndege, milima mirefu kama Kilimanjaro, bahari, maziwa na mito mikubwa na kwa kuwa jamii ya Wamasai imekuwa kivutio cha watalii kwa jinsi wanavyoendeleza utamaduni wao kwa mavazi yao ya kiasili: -

(a) Je, jamii hiyo ya Kimasai inafaidika vipi na mapato yanayopatikana kutoka kwa watalii hao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda cha kudumu cha kutengeneza mavazi ya Kimasai yakiwemo mapambo ya shingoni, mikononi hasa shanga zinazopendeza ili vitumike ipasavyo kama kivutio cha utalii?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuimarisha utamaduni huo wa Wamasai ambao ni kivutio kikubwa cha watalii kwa kuwajengea kiwanda cha viatu vyao vya asili vinavyotengenezwa kwa mipira ya magari iliyokwishatumika na kutoa ajira kwa Wamasai wenyewe ili wasimamie vilivyo utamaduni wao usiharibiwe kwa kuwekewa madoido ambayo yataharibu asili ya vazi lao na utamaduni na hivyo kuathiri kivutio hicho cha asili?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Frank Maghoba, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Maghoba kuwa, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vivutio vya aina mbalimbali vikiwemo vya asili na vya kihistoria. Pamoja na vivutio hivyo, tunao utamaduni, mila na desturi za makabila zaidi ya 120 nchini mwetu, ambavyo ni hazina kubwa na ya pekee. Ninaomba niweke wazi kuwa, kinachouzwa kama kuvutio cha utalii siyo kabila wala mtu, bali mila, utamaduni na hulka.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Serikali kupitia Wizara yangu ni kuhamasisha ushiriki wa Wananchi katika shughuli za kuendeleza maliasili na utalii kwa lengo la kujipatia kipato na hivyo kupunguza umaskini. Kwa misingi hiyo, jamii ya Kimasai kama zilivyo jamii nyingine za Tanzania, wamehamasishwa na wanashiriki katika utalii wa utamaduni *(Cultural Tourism),* ambapo kuna Vituo vya Longido, Mkuru na Engaruka, vinavyoshiriki katika aina hii ya utalii. Shughuli za utalii wa utamaduni zinaendeshwa na kusimamiwa na wanajamii wenyewe. Aidha, Wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwa kushirikiana na Baraza la Wafugaji, imeanzisha maboma matano ya kitamaduni *(Cultural Bomas),* ndani ya Hifadhi. Maboma hayo yanawapa fursa wenyeji kuuza bidhaa wanazotengeneza kwa mfano, shanga, mikanda, mikuki na kadhalika, kwa watalii wa ndani na wa nje. Vile vile, maboma haya yanawapa fursa wenyeji kuonyesha utamaduni na mila zao kwa wageni wanaoyatembelea.

Mheshimiwa Spika, Wamasai kama Wananchi wengine wanaoishi katika maeneo yenye shughuli za utalii wa uwindaji, wanafaidika na asilimia 25 inayopelekwa katika Halmashauri za Wilaya zao kwa ajili ya huduma za kijamii. Kipekee pia, jamii ya Wamasai wanafaidika na huduma mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, ambapo kwa mwaka 2003/2004 imetoa kiasi cha Sh.550,000,000/= kwa ajili ya huduma za kijamii. Fedha hizi zimeingizwa katika akaunti ya Baraza la Wafugaji, ambacho ndicho chombo cha uwakilishi cha wenyeji wa eneo hilo. Zana za mikono kutoka tamaduni tofauti huvutia wenyeji na wageni kwa sababu hutumika kwa matumizi mbalimbali na kwa mapambo. Uzuri na ubora wa mapambo ya Kimasai, kama zilivyo sanaa nyingine, ni ule usanii. Usanii ukishafanywa kwa mashine unapoteza hadhi ya usanii na hivyo kupoteza hadhi ya kuwa kivutio. Ili mapambo ya Kimasai yaendelee kuvutia na ili usanii udumu kuendelezwa na kurithishwa, ni vema ukaendelea kufanywa kwa njia zile za kiutamaduni. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Moja kati ya kitu kinachovutia katika jamii ya Wamasai ni ile dawa ya kujipaka inayoitwa *olkaria;* je, Wizara yake itawasaidia vipi Wamasai waieneze dawa hii madukani ili iweze kuwafikia Watanzania wote? *(Kicheko/Makofi)*

(ii) Kwa kuwa moja ya utamaduni wa Wamasai ni kutembea na visu virefu ambavyo vinakuwa nje nje kabisa na siku hizi kuna upekuaji katika *check points* mbalimbali. Je, Serikali itawasaidia vipi kuwaelewesha ili wasigombane na wale wanaowapekua? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, dawa hiyo ya Wamasai ya kujipaka ni sehemu ya utamaduni na kama nilivyosema ni kwamba, kwa watalii wa ndani na wa nje, kuna maeneo yale ya maboma yaliyopo. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge, anahitaji au na wengine wanahitaji wanaweza kupata kutokana na hayo maboma. Suala la visu virefu, nafikiri hili ni suala la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kuwa suala la mali au utamaduni mbali na kuwa ni Wamasai pekee ndiyo wanaonekana wanajulikana katika nchi hii; kwa nini Wizara isifanye utaratibu wa kuhamasisha makabila mbalimbali yaliyoko nchini, kuonyesha utamaduni wao, badala ya kung’ang’ania utamaduni wa Wamasai peke yao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, suala hili lilikuwa juu ya Wamasai na ndiyo maana nilijibu, lilikuwa siyo suala la makabila yote. Lakini lingekuja suala la makabila mbalimbali tungelijibu kwa upana zaidi. Lakini tosha kusema kwamba kwa kweli Wizara yangu sasa hivi inatilia mkazo suala zima la utamaduni kama nilivyoeleza maeneo ya Kondoa kwa mfano, maeneo ya Kusini, yanashughulikiwa na maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, ni jukumu pia la wananchi wenyewe kuhamasisha wananchi wenzao pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Na. 63

**Uwekezaji katika Usafiri wa Anga**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa makusudi imefungua milango wazi kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika sekta mbalimbali ukiwemo uwekezaji katika usafiri wa anga na kwa kuwa wasafirishaji wa kutumia ndege hasa zile ndogo hurusha ndege zao kwa safari za ndani kwa kuwa na rubani mmoja tu bila ya rubani msaidizi:-

(a) Je, Serikali kupitia chombo husika inalijua hilo?

(b) Je, kama inalijua inalichukua vipi hasa kwa kutambua rubani ni binadamu ambaye lolote linaweza kumtokea la maradhi ya ghafla na kusababisha rubani huyo kushindwa kuidhibiti ndege?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga hapa nchini, inafahamu kuwa zipo ndege ndogo za abiria ambazo huendeshwa na rubani mmoja bila ya kuwa na rubani msaidizi. Kisheria ndege zinazoendeshwa na rubani mmoja bila msaidizi ni zile zenye uzito usiozidi kilogramu 5,700. Ndege zenye uzito zaidi ya hapo hulazimika kuwa na marubani wawili au zaidi. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 30(5) cha Kanuni za Usalama wa Anga za mwaka 2003.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na hali ya maradhi inayoweza kumkumba rubani ghafla, zipo kanuni zinazombana rubani pamoja na mwenye ndege ili kuhakikisha kuwa tatizo kama hilo kwa kiasi kikubwa linaepukika. Kwa mfano, kwa mujibu wa Kanuni za Usalama wa Anga za mwaka 2003, kifungu cha 41 kinamtaka kila rubani awe anapimwa afya yake kila baada ya muda maalum kulingana na aina ya leseni aliyonayo kabla ya kupata mpya au kuongezewa muda. Kipindi kilichowekwa ni miezi sita au miezi kumi na miwili na kupimwa huko ni lazima kufanywe na daktari anayetambuliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usalama wa Anga hapa nchini. Aidha, kifungu cha 42 cha Kanuni za Usalama wa Anga za mwaka 2003, kinamtaka kila rubani aifahamishe Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga, pindi anapougua na leseni yake husitishwa kwa muda wote atakaokuwa mgonjwa. Kifungu cha 53(1) cha Kanuni hizo pia kinamzuia rubani asiye na afya njema kuendelea kurusha ndege na kifungu 53(2) kinamtaka mwajiri au mwenye ndege kutomruhusu rubani ambaye afya yake si nzuri kuendesha ndege.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa uwezekano wa rubani kudhurika ghafla kutokana na maradhi ni mdogo mno. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, tahadhari kubwa zinachukuliwa kuhusu afya ya rubani. Serikali inaamini kwamba, kwa kutumia kanuni hizi za Udhibiti wa Usalama wa Anga hapa nchini hali kama anayohofia Mheshimiwa Mbunge, itakuwa nadra sana kutokea.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Pamoja na kwamba amehakikisha marubani hao huwa wanapimwa afya zao, lakini kwa kweli kinachosikitisha ni kwamba kurusha ndege kutoka Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Tanga na kurudi ni masafa marefu sana. Kuna wakati nilisoma gazeti,

rubani mmoja wakati anatua na ndege alifariki wenzao wakafanikiwa kumwondoa na wakati ndege inashuka kule Ulaya. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kubadilisha sheria hiyo, kuweka marubani wawili kama *reserve* rubani yule mwingine kwa usalama wa wananchi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kwamba, uzito ndiyo unaofikiriwa zaidi na siyo masafa. Hizi ni sheria ambazo zinatumika hata katika *International Civil Aviation Organisation (ICAO)* siyo kwamba ni suala hili tunajitungia tu sisi Watanzania na kwa kweli hatuwezi tukasema ndege ya watatu iende na marubani wawili au ndege ambayo inachukua watu wanne iende na marubani wawili.

Mheshimiwa Spika, labda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa, ziko shughuli ambazo zinafanya ndege isiwe na marubani wawili kwa mfano, *specification* huko *manufacturers* wanapotengeneza wanasema ndege hii ni lazima irushwe na watu wawili hata kama ni ndege ya watu watatu, wana *specifications* zao. Au *operators* wenyewe wanapanga vile vile kwamba kutokana na ndege zangu nilizonazo, hali ilivyo nitahitaji kuwa na rubani mmoja. *Air Worthiness Certificate* inatoa kwamba kutokana na *Air Worthiness Certificate* iliyopo ndege fulani itachukua rubani mmoja au marubani wawili. Lakini kimsingi ni kwamba, uzito wa zaidi ya kilogramu 5,700 ndiyo tunachukua marubani wawili, lakini vile vile hata ukiona helkopta zote ni lazima ziendeshwe na marubani wawili. Hiyo, ndiyo sheria ya Kimataifa. *(Makofi)*

Na. 64

**Kurekodi Mazungumzo ya Mteja**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Kampuni za Simu za Mkononi yaani *Mobitel, Vodacom, Celtel* na *Zantel* zina mashine zenye uwezo wa kurekodi simu zote zinazotoka na kuingia kwa kila namba ya mteja saa zote 24 za siku:-

(a) Je, wanaweza kurekodi mazungumzo ya mteja iwapo itahitajika?

(b) Je, iwapo inawekezana kurekodi mazungumzo ya mteja na kwa nini kampuni hizo zisiweke mikataba ya kuhifadhi mazungumzo ya siri ya mteja ili yasitolewe kwa mtu au chombo kingine bila idhini ya maandishi ya mteja mwenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Makampuni ya simu za mikononi kama *Vodacom, Mobitel, Celtel* na *Zantel,* yana mitambo yenye uwezo wa kurekodi takwimu za simu zote zinazotoka na kuingia kwa kila namba kwa saa 24, lakini hawaruhusiwi kurekodi mazungumzo hayo.

Mheshimiwa Spika, kurekodi au kuingilia mazungumzo ya simu kwa nia yeyote ile ni kukiuka haki za Kikatiba za watumiaji. Hata hivyo, haki hiyo inaweza ikaondoshwa pindi watumiaji au mtumiaji atahatarisha usalama wa nchi au kujihusisha na vitendo vinavyokwenda kinyume na sheria za nchi kama vile kujihusisha na ugaidi, madawa ya kulevya na makosa ya jinai ya kupanga *(Organized Crime).*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa ningeomba kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wananchi wamejenga imani ya matumizi ya simu za mkononi kwa nini basi makampuni hayo sasa yasiongeze mtandao wake katika maeneo ya biashara kama vile biashara za utalii, biashara za madini, biashara za utafiti ambao unafanywa katika maeneo kama katika Kata, Tarafa ya Amani katika Wilaya ya Muheza na katika maeneo ambayo bado mtandao huo haujafika?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ingawa swali la nyongeza ni jipya na halihusiani kabisa na swali la msingi, lakini naomba nichukue nafasi hii nimjibu Mheshimiwa Herbert Mntangi, kama ifuatavyo: Makampuni ya simu za mikononi yanajitahidi sana kufikisha huduma zake vijijini hasa katika maeneo ya biashara, maeneo ya utalii, ndiyo maana ukienda kwenye mbuga za wanyama, unakuta kuna mawasiliano ya simu.

Nimwombe Mheshimiwa Herbert Mntangi kwamba, kama kuna matatizo katika maeneo yake niko tayari kushirikiana naye ili kuwaomba wenzetu wasukume zaidi maendeleo katika maeneo yake. *(Makofi)*

Na. 65

**Fungu Maalum la Kuinua Sekta ya Kilimo**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2002/2003, Wizara imetenga fungu maalum la kuinua Sekta ya Kilimo nchini:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kimetengwa kwa Wakulima wa Mkoa wa Ruvuma?

(b) Je, ni wakulima wangapi wanawake Mkoani Ruvuma watanufaika na mpango huo?

(c) Je, ni miundo mbinu gani itakayopewa kipaumbele katika mpango huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Viti maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 16.48 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5.42 zilikuwa ni nyongeza kwa Wizara kwa ajili ya shughuli za kilimo zinazotarajiwa kutoa matokeo ya haraka *(Quick Wins)* na zenye manufaa ya moja kwa moja kwa wakulima. Maeneo yaliyohusika ni yafuatayo: Uzalishaji wa mbegu, shilingi milioni 211.4, kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, shilingi milioni 500, Mfuko wa Taifa wa pembejeo, shilingi bilioni 2.5, kuendeleza kilimo cha wanyama kazi, shilingi milioni 300, Hifadhi ya Taifa ya Chakula, shilingi bilioni 1.9 na kuandaa mwongozo wa kuziwezesha Wilaya kuandaa mikakati na programu zao za kuendeleza kilimo, shilingi milioni 9.2

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kati ya shilingi bilioni 5.42, wakulima wa Mkoa wa Ruvuma walitengewa jumla ya shilingi milioni 698.97 kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya shilingi milioni 13.47 zilitumika kuendeleza kilimo cha wanyamakazi Wilayani Songea. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 2.47 zilitumika kutoa mafunzo kwa wakulima, shilingi milioni 10 zilitumika kukarabati Kituo cha Mafunzo ya Wanyamakazi cha Lilambo na shilingi milioni moja zilitumika kununua zana za kilimo cha wanyama kazi.

(ii) Jumla ya shilingi milioni 108.64 kutoka Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo zilikopeshwa kwa Mawakala wanne wa pembejeo katika Wilaya ya Songea Vijijini na kupitia Mfuko huo, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilikopeshwa shilingi milioni 244.16 kwa ajili ya Mfuko wa Pembejeo wa Tunduru. Aidha, shilingi milioni 113.7 zimetumika kununua matrekta sita mapya na zana zake kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Matrekta Wilayani Songea.

(iii) Kitengo cha Hifadhi ya Chakula, Kanda ya Songea, kilinunua jumla ya tani 2,215.1 za mahindi kutoka kwa wakulima wa Mkoa wa Ruvuma zenye thamani ya shilingi milioni 219.

(b) Tathmini ya matokeo ya mipango ya kilimo ya mwaka wa 2002/2003 haikuainisha idadi ya wakulima wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, walionufaika na mpango wa 2002/2003. Hata hivyo, kutokana na kwamba kilimo chetu huendeshwa na

wanawake kwa karibu asilimia 70 ni dhahiri kwamba, mpango huo umewanufaisha wanawake wengi.

(c) Kutokana na fedha zilizotolewa kwa Mkoa wa Ruvuma, miundo mbinu iliyopewa kipaumbele ni pamoja na ukarabati wa Kituo cha Mafunzo ya Wanyama Kazi cha Lilambo na uanzishaji wa Kituo cha Matrekta Wilayani Songea.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa bajeti hiyo, ilitoa hilo ongezeko kubwa la pesa kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula na kwa kuwa ongezeko hilo limeweza kuanza utekelezaji wa miundombinu michache ya kuendeleza kilimo, lakini bado nchi imeendelea kuwa na tatizo kubwa la njaa na pia kilimo kuendelea kutokuwa chenye tija. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba programu zote za kilimo zinafanya kazi kwa haraka na zinaenea katika maeneo mengi ya vijijini ili kukabiliana na tatizo la njaa na kuongeza tija katika kilimo chetu nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara inashughulikia miundombinu ya kilimo, lakini tatizo la njaa analolihusisha la kuendesha programu zote kwa haraka nchi nzima, nadhani hii haitahusu Ruvuma kama ilivyoulizwa na kama inaulizwa nchi nzima, tunasema ndiyo tunafanya kwa sababu kama unavyojua, Wizara imeanzisha mipango mingi pamoja na *(DADPs),* mipango ya *irrigation* na kadha wa kadha, yote hii ni kuhakikisha kilimo kinaelimika. Kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kuwa, hatufanyi hivyo, tunafanya hasa haya aliyosema. *(Kicheko)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa swali la msingi limezungumzia kutenga fungu maalum la kuinua sekta ya kilimo nchini na kwa kuwa kutokana na umuhimu wa pembejeo katika kilimo, Serikali iliamua kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo kwa ajili ya Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya na Iringa. Je, Serikali inajua kwamba katika Mikoa hiyo sasa bei za pembejeo zimepanda sana tofauti na ahadi ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, inawezekana anayosema ni ukweli. Lakini Wizara imehakikisha Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Iringa na Rukwa kuna Kamati zinazosimamia masuala haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Sasa kwa kuwa hatujapata taarifa rasmi kutoka Kamati hizo, naomba tushirikiane tutafute ukweli wa jambo hilo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa Mbinga ni sehemu ya Wilaya ya Mkoa wa Ruvuma. Je, katika hizo shilingi milioni 600 zilizopelekwa Mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Mbinga imepata kiasi gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tarakimu nilizozitaja kweli zilihusu Mkoa wa Ruvuma, kwa kuwa swali lilielekezwa Wilaya ya Songea, nilijibu Kisongea Songea. Sasa tukitaka takwimu za Mbinga, naomba suala hilo lilitwe kwa utaratibu maalum au tuonane baada ya kikao hiki nitamtafutia takwimu. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 66

**Kutajwa Mkoa wa Morogoro Kama Mkoa Muhimu kwa Kilimo**

**MHE. ABU T. KIWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Morogoro hususan Jimbo la Kilombero ni kati ya Majimbo yenye uwezo wa kulisha nchi hii ukizingatia kwamba ina ardhi ya kulimika *(Arable Land)* ipatayo hekta milioni 1.204 ambapo ni asilimia 6 tu sawa na hekta 70,000 inayolimwa; na kwa kuwa Mkamba, Kidatu na baadaye Lwipa, ambazo zinalima miwa na wakulima wengi wa Ifakara kuelekea Tanganyika Masagati kilimo chao ni cha chakula kama vile mpunga, mahindi na kadhalika; na kwa kuwa vyanzo vya maji sehemu hizo ni vingi na kwamba kilimo cha umwagiliaji kitawaongezea uwezo mkubwa wa kujikwamua na adui umaskini na kukiendeleza kilimo chao cha sasa na kuanza kulima miwa kama zao la biashara ili kukidhi mahitaji ya Kiwanda cha Kukamua Miwa kinachotarajiwa kujengwa huko Lwipa na Kampuni ya *ILOVO (Kilombero Sugar)*:-

(a) Je, kwa nini Serikali haikulitaja wala kuorodhesha Jimbo la Kilombero kuwa ni Jimbo moja muhimu kati ya majimbo yenye uwezo wa kulisha nchi hii?

(b) Kwa kuwa uzalishaji wa chakula Kilombero hauhitaji matumizi ya mbolea, je, Serikali haioni kuwa badala ya kugharamia mbolea ingegharamia uwezekano wa kuwapa wakulima wa Kilombero uwezo wa kununua matrekta na kuboresha kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haina mpango au utaratibu wa kutaja au kuorodhesha Majimbo ya Uchaguzi kuwa ni muhimu miongoni mwa Majimbo yenye uwezo wa kulisha nchi hii na hiyo ndiyo sababu ya Jimbo la Kilombero kutokutajwa au kuorodheshwa hivyo. Hata hivyo, Serikali inatambua kwamba, Mkoa wa Morogoro, hususan Wilaya ya Kilombero, una uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao ya chakula kwa kuwa una ardhi nzuri, inayofaa kwa kilimo na mito mingi isiyokauka inayoweza kutumiwa kwa umwagiliaji. Changamoto kwa uongozi na wananchi wa Morogoro ni kutumia uwezo huu wa kuzalisha mazao kuchangia upatikanaji wa chakula na mazao ya biashara kwa viwango vikubwa kuliko inavyofanyika sasa.

(b) Sina hakika kama uzalishaji wa chakula katika Jimbo la Kilombero hauhitaji mbolea. Uhakika huo utapatikana kwa kufanya uchunguzi wa kisayansi wa udongo huo kubaini madini yaliyopo na kwa viwango gani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatilia mkazo kilimo cha wanyamakazi na matrekta kwa nchi nzima na ili kuchangia juhudi za wananchi kupata zana hizo katika mwaka wa 2003/2004, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, umeanzisha utaratibu wa kutoa mikopo ya kununulia majembe ya kukokotwa na wanyamakazi, matrekta mapya na kukarabati matrekta mabovu.

Kwa upande wa Wilaya ya Kilombero, Mfuko wa Pembejeo ulipokea maombi 31 ya kukarabati matreka mabovu na kati ya hayo, 12 yamekwishapatiwa mikopo ya jumla ya shilingi 37,076,000/= na mengine mawili yanaendelea kushughulikiwa. Mfuko ulipokea ombi moja la mkopo wa kununua trekta jipya na ombi hilo linaendelea kushughulikiwa. Wakulima wanashauriwa kujiunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa ili waweze kupatiwa mikopo.

Kwa upande wa mipango ya umwagiliaji, mpango kamambe wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, umeainisha skimu 13 kwenye Mkoa wa Morogoro, ikiwamo Wilaya ya Kilombero, zenye ukubwa wa hekta 108,900 zinazofaa kuendelezwa. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Serikali kupitia mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs),* imetenga shilingi milioni arobaini kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya skimu ya umwagiliaji maji mashambani ya Njagi iliyoko Wilayani Kilombero. Skimu hiyo ina eneo lenye hekta 250 linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupewa nafasi hii. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa sababu Mheshimiwa Waziri amezungumzia juu ya kutaja umuhimu ni Mkoa tu na siyo Jimbo, naomba anieleze ana mpango gani kwa Mkoa wa Morogoro hususan kwa juhudi za Mbunge wa Kilombero kuanzisha Vituo vya Kilimo? *(Makofi)*

(b) Tunazungumzia tena Mkoa, wakati Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya akiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, alianzisha taratibu za kupata matrekta kutoka *FAO* na kuwakopesha wananchi ili wainue kilimo. Je, Serikali ina tamko gani juu ya kutoendelea kwa mpango ule? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kituo cha kilimo, kwa sasa hatuna mpango huo. Lakini siyo vibaya suala hili likajadiliwa hapo walipo katika Wilaya ya Kilombero na Mkoani, likaletwa Wizarani kwa ajili ya kushughulikiwa. Mimi ninaunga mkono mpango huo naona unafaa.

La pili taratibu za mpango wa *FAO*, huu mradi naona ulikuwa wa muda, ulikuwa siyo wa kudumu na haukuendelea baada ya hapo. Lakini tunamshauri Mheshimiwa

Mbunge, kama tatizo ni trekta, matrekta yanapatikana kutoka Mfuko wa Pembejeo wa Taifa kama nilivyoeleza na kwa maelezo zaidi tuonane, nitafafanua. *(Makofi)*

Na. 67

**Madhara Yatokanayo na Vifo vya Ukimwi**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Ugonjwa wa Ukimwi unaacha madhara mengi baada ya vifo vinavyotokana na ugonjwa huo kama vile watoto yatima, nguvu kazi ya Taifa kupungua, ongezeko la watoto wasio na makazi na utapiamlo, umaskini kuongezeka, kupoteza wataalam na kadhalika, ambayo kwa pamoja yanaathiri Taifa kwa ujumla. Je, Serikali imeandaa mikakati gani ya makusudi ya kukabiliana na madhara yatokanayo na ugonjwa huo hatari?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, katika Mkutano wa Saba, nilieleza kuwa, Wizara yangu kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii, inatekeleza mikakati mbalimbali ya makusudi ya kuwasaidia wajane na watoto walioathirika na Ukimwi. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

Moja, kuwapatia wajane misaada mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha kwa madhumuni ya kuanzisha shughuli endelevu za uzalishaji mali ili kuwaongezea uwezo wao wa kuwahudumia wale wanaowategemea ikiwa ni pamoja na watoto wao.

Mbili, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Madawa ijulikanayo kwa jina la *Abbott Laboratories and Pharmaceuticals Company,* imekuwa na utaratibu wa kugharamia matibabu kwa watoto yatima katika Hospitali ya Igongwe Wilayani Rungwe na pia imeandaa utaratibu wa kutoa mikopo kwa wajane kwa ajili ya kuanzisha shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ili kuwaongezea uwezo wa kujikimu kimaisha. Mpango huu unatekelezwa Wilayani Rungwe na utapanuliwa katika Wilaya zingine za Mbeya Mjini, Kilosa na Muheza.

Tatu, Wizara kwa kushirikiana na *UNICEF,* imeandaa kikundi cha wawezekaji haki jamii *(Para Legal)* ili kulinda haki za watoto yatima na wajane.

Nne, Wizara pia kwa kushirikiana na *UNICEF,* imeandaa kijitabu cha walezi wa watoto yatima wakiwemo wajane kwa madhumuni mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuainisha utaratibu wa kuwasaidia ndani ya jamii walizomo.

Mheshimiwa Spika, mikakati hii inayotekelezwa na Wizara yangu pamoja na ile inayosimamiwa na Taasisi zingine, yote inalenga kupambana na kupunguza madhara yanayotokana na ugonjwa huu hatari wa Ukimwi.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa suala la Ukimwi *trend* yake inakwenda katika *steep hill* na matokeo yake athari kwa mfano, watoto yatima ni wengi sana, kuna maeneo unakuta mtoto wa miaka 10 analea watoto wenzie, watoto wa barabarani wako wengi wametokana na wazazi wao kufa kwa ajili ya Ukimwi. Je, Mheshimiwa Waziri, sasa hivi *trend* inaonekana Rungwe, lakini Ukimwi unaonekana sehemu zote, naomba tu anisaidie hili la watoto yatima, watoto wa barabarani walioathirika kwa ajili ya wazazi wao kufa na Ukimwi, Serikali inachukua jukumu gani kwa kweli inasikitisha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda tu kumbukusha kwamba, nchini kote kuna vituo 52 vya kulelea yatima na Serikali inajitahidi kwa kadri ya uwezo wake, kuvisaidia kifedha vituo hivyo pamoja na kile ambacho kinaendeshwa na Serikali pale Kurasini. Lakini la pili, hakuna watoto wa barabarani, watoto wote wana wazazi wao. Tujenge utamaduni wa kuheshimu watoto wetu kwa sababu watoto waliopo Dar es Salaam kwa mfano kule mitaani wengi wao wana wazazi wao lakini kwa sababu tu ndoa zao zimevunjika, watoto wanaamua kurukia, siku hizi wamepata na jina wanaita chokoraa. Lakini kwa wale watoto yatima wengi wao tulitarajia watunzwe na ndugu wa marehemu na huu ndiyo utamaduni wa Waafrika siku zote, sasa hivi tunakoelekea hatujui ni wapi, kwa hiyo ni jukumu letu sisi kama viongozi, kwa kweli kuwahamasisha Watanzania wenzetu kutunza jamaa zetu na wale wanaoshindikana wapelekwe kwenye Vituo vya Watoto Yatima, ambako watapata malezi, badala ya kuwaachia tu waende barabarani ukififikiri wewe umepungukiwa na mzigo. Lakini la msingi zaidi tusizungumzie matokeo ya Ukimwi, tuzungumzie namna ya kupambana kuambukizwa na Ukimwi. Liwe ni jukumu la Viongozi wa Dini, Viongozi wa Serikali na sisi Wanasiasa, maana tukiona *soo* kuambiana juu ya kusubiri au kuwa mwaminifu, basi shetani wa ngono akipanda tutumie kinga hiyo ndiyo dawa nzuri zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 68

**Ubora wa Elimu Nchini**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATE** aliuliza:-

Kwa kuwa ubora wa elimu unategemea sana walimu walio bora kitaaluma na juhudi za kufanya kazi na kwa kuwa hivi sasa suala la kuboresha elimu nchini limepamba moto na ubora wake unaenda sambamba na walimu wa kutosha, masomo ya kisasa kama vile kompyuta na kadhalika:-

(a) Je, katika elimu ya msingi ni asilimia ngapi ya walimu wame-*up-grade* Kitaifa?

(b) Je, shule za msingi zilizo mbali na huduma ya umeme, Serikali inafanya juhudi gani kuwapatia elimu ya kompyuta?

(c) Je, hadi sasa ni shule ngapi za Sekondari zilizo na masomo ya kompyuta?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, imeshindikana kujibu swali hili kwa uhakika kwa sababu halina muda maalum lakini katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, jumla ya walimu 81,000 wamepandishwa vyeo. Mwaka 2001/2002 walipandishwa vyeo walimu 54,581 na mwaka 2002/2003 walipandishwa vyeo walimu 26,419.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya kutaka somo la kompyuta lifundishwe katika shule za msingi, ufundishaji wa somo hilo katika shule za msingi na Serikali bado haujaanza kwa sababu hatujawa na walimu walioandaliwa kufundisha somo hilo. Hivi sasa Wizara yangu iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mpango wa kompyuta katika Vyuo vya Ualimu vyote 34 vya Serikali kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano. Malengo ya mafunzo haya ni pamoja na kuwawezesha wakufunzi na wanachuo katika kutumia *ICT* kufundishia na kujifunzia kwa ufanisi katika vyuo vya ualimu, kujifunza namna ya kutumia *ICT* kufundisha masomo watakayokuwa wanafundisha na kutumia *ICT* kurahisisha mawasiliano ya kitaalam na kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuanza kwanza kufundisha somo la kompyuta katika Vyuo vya Elimu ya Ualimu. Utekelezaji wa mpango huu unatarajia kuanza katika *intake* ijayo ya Vyuo vya Ualimu, kwa lengo la kila anayefuzu katika vyuo hivyo awe na ujuzi wa kompyuta wa kawaida. Baada ya kuwa na walimu wa aina hiyo, ndipo tutaweza kuanza ufundishaji wa somo hilo katika shule zetu zote kwa kuanzia pale ambapo miundombinu kama ya umeme itakuwa imeimarika.

(c) Mheshimiwa Spika, katika shule za sekondari, somo la kompyuta linafundishwa na kutahiniwa katika shule 13 tu. Hata hivyo, zipo shule nyingi za sekondari zinazofundisha somo la kompyuta ingawa si kwa lengo la kutahiniwa kwa sababuya ukosefu wa walimu wa kufundisha somo hilo na kuwepo kompyuta chache au kutokuwepo kabisa kwa kompyuta katika baadhi ya shule.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Serikali, kutoa shukrani kwa Serikali ya Sweden na Shirika lake la *SIDA* kwa uhisani wao ambao umetuwezesha kuajiri Mtaalam Mshauri, ambaye mwezi huu wa Aprili, 2004, anakamilisha andiko la mradi wa kompyuta kwa Vyuo vya Elimu ya Ualimu vyote 34 vya Serikali na kuainisha mahitaji yote ya vifaa ambavyo vitanunuliwa kwa uhisani wao na kutuwezesha kuanza mafunzo hayo muhula ujao.

Na. 69

**Barabara ya Mnyerere - Lusala Kusimamiwa na Mkoa**

**MHE. LEPHY B. GEMBE (k.n.y. MHE. STANLEY H. KOLIMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Ludewa mwaka 1996 wakati anafungua Daraja la Mto Mnyerere - Lyamanzi - Lusala kwenye barabara inayounganisha Wilaya za Ludewa na Makete, aliagiza barabara hiyo isimamiwe; na Mkoa na kwa kuwa barabara ya Lusala - Makete ni muhimu kwa kuunganisha barabara za Mikoa ya Ruvuma,Iringa hadi Mbeya:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza agizo hilo la muda mrefu la Mheshimiwa Rais?

(b) Je, lini Serikali itachukua hatua ya kuendeleza barabara hiyo ili kuweza kuunganisha Mikoa hiyo mitatu niliyoitaja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Stenley Haule Kolimba, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b), ninapenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mnyerere - Lusala ni barabara iliyoko chini ya Halmashauri za Wilaya ya Ludewa na Makete. Barabara hii inaunganisha eneo la Ikonda Wilayani Makete na eneo la Mlangali Wilaya ya Ludewa. Barabara hii ina urefu wa kilometa 80 na ni fupi sana ikilinganishwa na ile inayozunguka kupitia Mjini Njombe. Barabara hii inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Makete kwa upande wa Makete na Halmshauri ya Wilaya ya Ludewa kwa upande wa Ludewa. Sehemu inayohudumiwa na Wilaya ya Makete ilifanyiwa matengenezo makubwa kupitia msaada wa *USAID* na inapitika vizuri. Aidha, sehemu ya upande wa Ludewa bado haijafanyiwa matengenezo yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba kujibu swali hilo kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilikuwa haina kumbukumbu za maagizo ya Mheshimiwa Rais aliyoyafanya wakati wa ziara yake Mkoani Iringa kati ya tarehe 1 - 6 Desemba, 1996. Hivi karibuni Wizara yangu kupitia Ofisi ya Meneja wa Barabara Mkoa wa Iringa, imefuatilia na kuipata taarifa hiyo toka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa. Hivyo, agizo hili linafanyiwa kazi hivi sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati wote Serikali ina nia ya kuiendeleza miundombinu yake husussan ya barabara ikiwemo barabara hii ya Mnyerere - Lyamanzi - Lusala hadi Makete. Tatizo kubwa ni upatikanaji wa fedha. Kama nilivyosema katika

maelezo yangu ya awali, *USAID* walitusaidia kutengeneza sehemu ya barabara hii upande wa Makete. Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha barabara hii.

Aidha, kwa kuwa bado barabara hii ipo chini ya Halmashauri za Wilaya, namshauri Mheshimiwa Mbunge, aiwasilishe kwa Halmashauri ya Wilaya hoja ya kipaumbele cha barabara hii ili iweze kutengewa fedha na hasa ukizingatia kuwa, TAMISEMI hupata mgao wa Mfuko wa Barabara, wakati huo huo Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kutimiza ahadi ya Rais iliyotajwa hapo juu.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara hii inayounganisha mikoa mitatu, Mbeya, Ruvuma na Iringa, ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi wa Mikoa hiyo ni lini barabara hiyo itatengenezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa barabara hii inaunganisha Mikoa mitatu muhimu, lakini bado barabara hii kwa kila mkoa upande wake ni barabara ya Wilaya siyo barabara moja kama inavyoonekana. Kwa hiyo, ningewaomba Waheshimiwa Madiwani na hasa Wakurugenzi Watendaji, wapeleke hoja hii kwa utaratibu unaotakiwa kabisa, kupeleka TAMISEMI maombi maalum juu ya ahadi ya Rais na Rais hakuahidi kutengeneza barabara hii. Ahadi ya Rais ilikuwa ni vitu viwili, ameahidi kutoa makalvati 9 katika barabara hii na ameiomba Ofisi ya Mkoa ifuatilie suala hili ili Wizara iweke kwenye Bajeti mwaka 1996. Ndiyo sasa tumepata hii ahadi kwa sisi kuifuatilia baada ya kupata swali hili. Kwa hiyo, ni maombi ya kujenga makalvati 9, ndiyo maana nimesema Serikali sasa inaifanyia kazi.

Na. 70

**Mafanikio Yaliyopatikana kwa *Net Group Solution***

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Kampuni ya *Net Group Solution* inayoendesha Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania *(TANESCO)* imekuwepo tangu Mei, 2002 na inategemea kumaliza kipindi chake ifikapo Mei, 2004 kipindi ambacho matatizo ndani ya Shirika hilo yameongezeka badala ya kupungua kama ambavyo wananchi wengi walitarajia; na kwa kuwa utendaji wake umeshindwa kutatua tatizo la umeme hapa nchini na badala yake kumekuwepo na jitahada kubwa za kukusanya madeni na kupandisha gharama za utumaiaji wa umeme, kitu ambacho kimesababisha nishati hiyo kuwa kitu cha anasa badala ya kuwa huduma muhimu kwa maisha ya kila siku ya Mtanzania:-

(a) Je, Serikai imepata mafanikio gani kutokana na kuwepo kwa Mkataba huo na *Net Group Solution* na je, inafikiria vipi suala la kuwaongezea muda wa kuendelea kuendesha *TANESCO?*

(b) Kwa kuwa sehemu nyingi za Mijini/Vijijini zinahitaji umeme na kwamba huduma hiyo imekuwa ni adimu kulipia gharama kubwa, je, Serikali inayo mipango gani ya kuwapatia umeme wananchi wa Nyamikona, Kalemera, Mkula, Malili, Ngasamo, Shighala, Badugu na Nyaluhande?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Raphael Masunga, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba uliowapa kazi *Net Group Solutions,* Kampuni hiyo ilipewa kazi zifuatazo: Kuboresha hali ya kifedha na kiutendaji ya *TANESCO,* kuongeza mapato, kupunguza gharama za uendeshaji, kubadilisha menejimenti, mtazamo wa menejimenti uwe wa kibiashara zaidi na kuimarisha njia za usafirishaji na usambazaji wa umeme na kupunguza upotevu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo yaliyotajwa, *Net Group* ilipanga programu ya kazi ya kununua vifaa vya kutosha, kuboresha upatikanaji wa umeme kwa kuimarisha njia kuu za usafirishaji na usambazaji, kupunguza upotevu wa umeme kwa asilimia 22 ifikapo Mei, 2004, kuongeza mapato ya *TANESCO* kufanya *auditing* za mita, kuandaa kumbukumbu sahihi za wateja ili wahudumiwe vizuri na kutayarisha programu ya mafunzo ya Mameneja na mfumo mpya wa kuendesha *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo ambayo *Net Group* ilipata wakati inaingia kazini ikiwa ni pamoja na kukataliwa na wafanyakazi, mgogoro wa Mkataba wa Hiari na ukame ambao umeikumba nchi yetu, Serikali imepata mafanikio yafuatayo: Mapato ya Shirika yameongezeka kwa asilimia 60 kutoka shilingi 10 bilioni kwa mwezi mwaka 2002 hadi shilingi 16 bilioni, upotevu wa umeme katika njia kuu za kusafirishia umeme umepungua kwa 4% kutoka 27% mwaka 2002 hadi kufikia 23% mwaka 2004, makusanyo ya ankara kutoka kwa wateja yameboreshwa kwa 24% kutoka 75% mwaka 2002 hadi 93%, wateja wameongezeka kutoka 471,000 hadi 527,000, gharama za uendeshaji zimepungua kwa 27%, vifaa vyenye thamani ya Sh.40 bilioni vimeshanunuliwa na vituo vya kuzalisha umeme vinavyojitegemea katika maeneo mbalimbali kukarabatiwa au vinaendelea kukarabatiwa ikiwa ni pamoja na kununuliwa *generators* mpya Vituo vya Mtwara

Vile vile *TANESCO* imefanya ukaguzi wa mita *(Metre Auditing)* na hivyo kuokoa shilingi bilioni 3 ambazo zingepotea kwa ajili ya wizi wa umeme. *TANESCO* pia imeweza kulipa karibu Sh. 10 bilioni kushusha *capacity charge* katika Mradi wa Umeme wa Songo Songo toka milioni 5.8 hadi dola 3.8. *TANESCO* imelipia umeme wa *IPTL* Sh.44 bilioni ili kuepuka mgao wa umeme, *TANESCO* imelipa Sh.22 bilioni kama mafao ya 21% ya wafanyakazi 1,294 waliopunguzwa kazi, ambayo ni asilimia 21 ya wafanyakazi, *TANESCO* imefundisha upya Mameneja 220 na *Net Group* hivi sasa inakubalika na wafanyakazi.

(a) Mkataba wa *Net Group* unaweza kuongezwa baada ya kupokea Taarifa ya *Monitoring Consultant* aliyeajiriwa na Bodi ya *TANESCO,* kupima ufanisi wa *Net Group*. Pia unaweza kuongeza baada hapo kutokana na mashauriano na uamuzi ambao utafanywa na Serikali. Hivi sasa, hatua zinakamilishwa kuongeza Mkataba wa muda mfupi wa miezi mitatu, kuanzia Mei, 2004 ili kutoa nafasi ya tathmini na majadiliano juu ya Mkataba wa *Net Group.*

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ya kupatiwa umeme aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, kwa ujumla Serikali inakamilisha mipango ya kuanzisha Mfuko na taasisi ya umeme vijijini ili kufikisha umeme vijijini. Naomba Mhshimiwa Mbunge, afanye subira Mfuko huu uanze na uimarike.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kufuatia hali ya ukame uliokuwa umeikumba nchi yetu, Bunge lako Tukufu katika Mkutano wake wa 14, liliidhinisha jumla shilingi bilioni 34 kuisaidia *TANESCO* kuendelea kutoa umeme kutokana na mitambo yake. Sasa je, pesa ilikuwa ni ruzuku au ilikuwa ni mkopo kama ni mkopo *Net Group Solution* watalipa baada ya muda gani na kwa *interest* ya asilimia ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, fedha ambazo *TANESCO* wamekuwa wakipewa na Serikali katika kipindi hiki cha ukame ambao haukutarajiwa ni msaada wa Serikali kwa *TANESCO* kuhakikisha kwamba, nchi yetu haiingii katika mgao wa umeme ambao ungegharimu uchumi wetu kwa kipindi cha miezi sita tu zaidi ya shilingi bilioni 800. Ni muhimu kwamba tumehakikisha kwamba tuna nishati ya kutosha.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kutokana na kukatika katika kwa umeme mara kwa mara pamoja na kuharibu vyombo vya wateja, imeonesha kwamba *Net Group* imeshindwa katika utekelezaji hasa wa mgao wa umeme na kuhakikisha umeme unapatikana wakati wote. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kumaliza Mkataba wa *Net Group* pale itakapofika Mei bila ya kuongeza na kwamba hasara iliyokuwa imepatikana ilipwe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wakati naeleza kazi iliyofanywa na *TANESCO,* nilitoa vigezo kwa kueleza Mkataba wao, walikabidhiwa nini na nini basi kutokana na Mkataba ule na programu ya kazi iliyopangwa wamefikia ufanisi kwa asilimia ngapi, sehemu hadi sehemu. Ni vizuri twende kwa takwimu zile ambazo zinapatikana na ambazo zinatokana na utafiti au tathmini iliyofanywa na watalaam ambao wamewekwa kutathmini kazi ya *Net Group.* Katika kazi zile ambazo zimefanywa na ambazo nimezizungumza katika suala zima la umeme, uboreshaji wa upatikanaji wa umeme, kuna sehemu mbili kuu. Kuna sehemu ya usafirishaji umeme kupitia njia kuu ya misongo mikubwa hii ya 220, 132, 66 na

kadhalika na kuna sehemu ya usambazaji umeme kwa mteja wa mwisho. Takwimu nilizozitoa zinahusu upunguzaji wa upotevu wa umeme au uboreshaji wa miundombinu katika hizi njia kuu.

Nakubali kwamba, bado ipo kazi ya kuhakikisha kama katika usambazaji, ukatikaji wa umeme na huduma kwa ujumla katika suala la usambazaji linaboreshwa. Lakini kiujumla na kutokana na takwimu ambazo nimezitoa hapa ni dhahiri kwamba, kazi iliyofanywa na *Net Group* ni kubwa zaidi kuliko ile sehemu ambayo wanatakiwa bado waifanye na kwa ajili hiyo na kama ambavyo nimesema kuhusu suala la mkataba, ni kwamba, tathmini inafanywa na Serikali itafanya uamuzi wakati muafaka.

Na. 71

***Kiwira Coal Mine***

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali sasa imetambua kwamba kuzalisha umeme kwa njia ya maji ni ghali sana na pia maji ni chanzo ambacho hakina uhakika endelevu *(Risk and Unsustainable)* na kwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na mamilioni ya tani za mkaa wa mawezi huko Mchuchuma katika Wilaya ya Ludewa na katika makutano ya Wilaya tatu za Ileje, Kyela na Rungwe ambako tayari Serikali imewekeza mabilioni ya fedha katika Mgodi wa *Kiwira Coal Mine Ltd.* ambao unazalisha makaa ya mawe na umeme unaouzwa *TANESCO:-*

(a) Je, eneo la *Kiwira Coal Mine* lina wingi gani wa makaa ya mawe ardhini na ni nini hatma yake?

(b) Je, kuna migodi mingapi ya aina ya *Kiriwa Coal Mine Ltd.* hapa nchini na inazalisha kiasi gani cha umeme *(megawatts)* unaouzwa na *TANESCO?*

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa mafao ya wafanyakazi wa Kiwira waliopunguzwa kazi na kuwapa likizo bila malipo mwaka 1996?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Eneo la Kiwira lina wingi wa makaa ya mawe ardhini kama ifuatavyo: Mashapo ya kiuchumi *(Economic Reserves)*, tani 35.14 milioni, mashapo sanifu *(Proven Reserves)*, tani 22.14 milioni na mashapo yanayoweza kuchimbika *(Mineble Reserves)* tani 14.64 milioni. Ili kuyafikia makaa hayo, kampuni hufungua njia za mgodi ardhini. Kwa sasa zipo njia mbili zinazojulikana kama *District 1 - 1* na *District 1 - 2.* Njia hizo mbili zitamalizika makaa ifikapo mwaka 2008. Hivyo, kampuni hapana budi ifungue

eneo jipya la mgodi litakalojulikana kama *District I - 4,* inabidi kazi ianze sasa ili ifikapo mwaka 2007/2008 uzalishaji wa makaa ya mawe usikwame. Kampuni inatafuta mbia mwenye uwezo kwani kufungua eneo jipya na kukarabati na kubadilisha baadhi ya mitambo na mashine chakavu zilizoanza kutumika mwaka 1988, zinazahitajika takriban Sh.2.6 bilioni.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa ni Mgodi wa *Kiwira Coal Mines* tu unaozalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe na kuuza *TANESCO.* Mgodi una mtambo wenye uwezo wa kuzalisha umeme Megawati 6 ambapo kati ya hizo, Megawati 2 hadi 4 huuzwa *TANESCO*. Mapato ya mgodi kwa mauzo hayo kwa *TANESCO* ni wastani wa Sh.90 milioni hadi Sh.100 milioni kwa mwezi.

(c) Mheshimiwa Spika, Februari, 1997 wafanyakazi 1,050 wa Mgodi wa *Kiwira Coal Mines* walipewa likizo bila malipo, hawakupunguzwa. Serikali inayafahamu madai ya malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi walio kwenye likizo bila malipo na fedha zinazohitajika kuwaachisha kazi rasmi kwa mujibu wa sheria ambazo ni Sh.476,553,438.60. Mpango uliokuwepo ulikuwa Serikali kuchukua madeni yote ya ndani ya mgodi yakiwemo madai haya kama ubia na Kampuni ya *CHITEC* kutoka Jamhuri ya Watu wa China ungefanikiwa. Baada ya ziara ya Waziri wa Fedha nchini China mwaka 2003, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alikutana na Balozi wa China, Mheshimiwa Yu Qingta, tarehe 26 Machi, 2004 kumweleza kuwa Tanzania sasa iko tayari kukaribisha wawekezaji kutoka China ili kuendeleza Mgodi wa Kiwira uweze kuzalisha umeme kwa kiasi cha Megawati 30 na hivyo kuchangia katika azma ya Serikai ya kupunguza kutegemea maji katika kuzalisha umeme nchini.

Na. 72

**Sabuni inayotengenezwa kwa Mbono Kaburi**

**MHE. HAOUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa huko Monduli kuna vikundi vya akina mama vinavyojishughulisha na mradi wa kutengeneza sabuni za kuogea kwa kutumia mbegu za mbono kaburi na kwa kuwa imebainika kwamba sabuni hizo ni dawa ya upele, uwawati, maradhi ya ngozi na pia hulainisha mwili na kwa kuwa sabuni aina hiyo zinapendwa sana huko Arabuni:-

(a) Je, Serikali inawasaidia/itawasaidia vipi akina mama hao ili sabuni hizo ziweze kukaguliwa na Shirika la Viwango ili waweze kuwa na uhakika wa biashara yao?

(b) Ikiwa Shirika la Viwango litathibitisha kuwa sabuni hizo zimefikia viwango vya ubora wa bidhaa vinavyohitajiwa, je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuwatafutia soko kwa ajili ya bidhaa hiyo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kutumia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* imeweka utaratibu wa kuwasaidia wazalishaji wa viwanda vidogo vikiwemo vikundi vya wanawake kuzalisha bidhaa bora. Utaratibu huu huwasaidia wazalishaji husika kupewa ushauri wa kitaalam kuhusu uzalishaji husika, kupewa ushauri wa kitaalam kuhusu uzalishaji wa bidhaa bora mpaka kuwawezesha kuzalisha bidhaa kwa viwango vya ubora unaotakiwa na hatimaye kupewa leseni ya kutumia alama ya ubora ya *TBS* katika bidhaa zao. Kwa mfano, Shirika limewasaidia wanawake wa Kiwanda cha Ubiri kilichopo Wilayani Lushoto, kuzalisha jamu, *tomato sauce* na *chilli sauce.* Wanawake hao wamefanikiwa kuzalisha bidhaa bora na sasa wanaweka alama ya ubora ya *TBS* katika bidhaa zao. Kwa wale wateja ambao hawajaomba *TBS* kupatiwa huduma zake kama vikundi vya wanawake wa Monduli, *TBS* inatarajia kuwatafuta na kupima bidhaa zao ili kuona kama ubora wake unalingana na matakwa ya viwango vya Taifa. Iwapo sabuni zinazotengenezwa na wanawake hao zitafikia ubora unaostahili, *TBS* itawapa leseni ya kutumia alama yake ya ubora. Alama hiyo ya *TBS* ya ubora itawasaidia kuuza sabuni zao bila matatizo.

(b) Serikali inakubali kuwa ipo haja ya kuwatafutia soko vikundi vya wanawake wa Monduli kwa ajili ya bidhaa hiyo. Serikali kwa kupitia *SIDO,* huwa inatoa mafunzo na mbinu za masoko, utunzaji wa kumbukumbu na upangaji wa bei.

Aidha, *SIDO* na Halmashauri ya Biashara ya Nje *(BET),* huwa inaandaa maonyesho ya kibiashara ya Kitaifa na Kimaifa ili wazalishaji kama hao wa Monduli waweze kushiriki na kutangaza bidhaa yao ili wapate masoko. Wafanyabiashara wengi wamenufaika na huduma za *BET* hususan katika kutafuta masoko kwa bidhaa zao. Hivyo, vikundi vya manawake wa Monduli, vinashauriwa kushirikiana na *BET* ili wawatafutie masoko katika nchi za Arabuni ambako inasemekana sabuni za aina hiyo zinapendwa sana.

**MHE. HAOUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ambaye amekiri kwamba, kikundi hicho cha Monduli bado hakijakaguliwa na wataalam ambao wangeweza kutoa nafasi ya kuwapa hati maalum ya bidhaa zao. Lakini je, Serikali haioni kwamba hilo ni tatizo ambalo vikundi vingi vya nchi hii ambavyo vinajaribu kuondosha umaskini lakini bidhaa zao haziwezi kufika mahali popote kwa vile Serikali haina chombo maalum ambacho kinawasimamia akina mama hao na vijana?

Kama Mheshimiwa Waziri, atakubaliana na mimi, je, analiambia Bunge hili chombo hicho ni lini kitaundwa ili kuwafikia vikundi vya akina mama na vijana wote katika nchi hii?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nisemema hapa kwamba, vyombo viko viwili, chombo cha kwanza ni *TBS.* Kama vikundi vya akina mama wako tayari na utengenezaji wa bidhaa ambao inatakiwa watafutiwe masoko, basi lazima wawaone *TBS,* ili wapime ubora wa bidhaa, maana bila kupima ubora wa bidhaa, haziwezi kuwa na ubora wa masoko. Hizi ni zama za utandawazi, ubora wa bidhaa ni muhimu kabisa, lazima tupime, tujue ubora wake na masoko yanaweza kupatikana.

La pili, yako Mashirika mawili, *SIDO* na *BET*, yote yanashughulikia kutangaza bidhaa zinazotengenezwa na wananchi wa Tanzania ili waweze kupata masoko ndani ya nchi na nje ya nchi. Lakini taasisi hizi lazima ziarifiwe kwa sababu hawawezi kujua wenyewe tu. Kwa hiyo, ndiyo maana ushauri wetu ni kwamba vikundi vyote vinavyotengeneza bidhaa lazima viwasiliane na taasisi hizi ili waweze kutafutiwa masoko.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa ufahamu wangu, vikundi vingi vya akina mama na vijana vilipata mafunzo kutokana na Shirika letu ya viwanda vidogo vidogo. Je, hatuoni kwamba sasa hivi ni muda mrefu tangu wamepata mafunzo hayo na kufanya *TBS* kushirikiana na *SIDO* ambao tunawaamini kabisa kwamba, inawafundisha njia nzuri ya kutengeneza vifaa hivyo ikiwemo matunda na mboga mboga ili waweze kuwapa hiyo fursa ya kupima viwango kwa haraka ili na wao waweze kupata soko la ndani ambalo sasa ni gumu ukiacha la nje tuanze na soko la ndani angalau basi kwa kushirikiana na *TBS* na *SIDO* ambao ndiyo wakufunzi wakuu wa vikundi hivi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, lazima watengenezaji wa bidhaa zile washirikiane ama na *SIDO* , *BET* au *TBS.* Ni kweli mafunzo yamewahi kutolewa kwa vikundi vidogo vidogo vya Mafia lakini ni muhimu vile vile kwamba, mafunzo yanaweza yakatolewa lakini waliopata mafunzo yale, wasiweze kumudu kutengeneza vifaa vinavyofikia kiwango kinachotakiwa. Kwa hiyo, hoja hapa ni kuendelea kupata mafunzo yale na baadaye wahitimu kutengeneza bidhaa zinazopaswa kufikia kiwango kinachotakiwa.

Na. 73

**Gharama za Ukaguzi wa Magari**

**MHE. ISSA MOHAMED SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa kuagiza gari kutoka nje ya nchi kama vile Dubai unamtaka mnunuzi kupeleka gari lake kukaguliwa ubora wake; na kwa kuwa kazi hiyo hufanywa na kampuni binafsi ya Dubai kwa gharama ya *USD*150 kwa gari moja ambazo ni sawa na Sh.165,000/= za Kitanzania; na kwa kuwa yapo makampuni mengi ambayo yana sifa za kutosha kufanya ukaguzi kwa gharama ya *USD* 50; je, Serikali haioni iko

haja ya kuwapa kazi hiyo kampuni ambayo italipisha *USD* 50 ili kuwapunguzia mzigo wa *USD* 100 Watanzania wanaoagiza magari kutoka Dubai?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Mohamed Salim, Mbunge wa Koani, kama ifuatavyo:-

Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*, kwa kufahamu uzito wa kazi ya upimaji na uhakiki wa ubora wa magari yaliyotumika, kiwango cha dola 50 ni cha chini sana. Hii inaashiria kuwa, kampuni hizo zinazotoza kiwango cha dola 50, haizielewi uzito wa kazi yenyewe hivyo, upo uwezekano mkubwa wa kutokufanya kazi hii kwa ufanisi unaohitajika. Ni wazi kuwa athari za kuingiza nchini magari mabovu ni kubwa zaidi kuliko punguzo la dola 100. Ndiyo sababu Shirika la Viwango Tanzania lilikataa kutoa wakala kwa makampuni hayo kwa kuelewa kuwa kazi ambayo ingefanywa kwa gharama ya dola 50 isingefanyika kwa uadilifu na ufanisi unaohitajika. Kwa wakati huu, gharama zinazotozwa na kampuni za ukaguzi wa magari yaliyotumika ni dola za Marekani 250 kwa Japan na dola za Marekani 150 kwa Dubai *(UAE).*

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha kuwa, magari yaliyotumika yanayoingizwa nchini, yanakidhi matakwa ya viwango husika ili kulinda maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla, pamoja na kuzuia nchi kuwa dampo la magari mabovu ya nchi zilizoendelea kiviwanda.

**MHE. ISSA MOHAMED SALIM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa magari yanayoingia Tanzania kwa mwaka yanafikia 20,000 na kila gari likilipiwa dola 150 ni sawasawa na dola milioni tatu ambazo ni sawa na shilingi bilioni 3.3 za Kitanzania; na kwa kuwa teknolojia wanayotumia Makampuni yanayofanya ukaguzi Dubai na Japan, *VETA* inao uwezo wa teknolojia hiyo; je, Serikali haioni ni vema kuipa kazi hiyo*VETA* ili ipate nafasi ya kujiboresha zaidi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda niseme nini kinafanyika ili uweze kufikia kiwango kinachohitajika. Kwanza, lazima kuhakikisha *steering system* ya gari lenyewe.

Pili, *lighting system.* Tatu, *break system.* Nne, *drive safety system.* Tano, *gearbox and break system.* Mambo haya yakifanyika, ndio unaweza kujua kwamba hili gari linafaa kuletwa Tanzania au hapana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini huwezi kuliingiza gari lile kwanza Tanzania halafu ulihakiki hapa je, likiwa baya utafanya nalo nini? Kwa hiyo, lazima uhakikishe kule kule gari linapotoka kabla halijafika Tanzania. Kwa hiyo, huwezi kukabidhi kazi hii *VETA* ingawa Serikali ingependa kukabidhi kazi hii *VETA. (Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali pia yamekwisha, saa nne na nusu sasa. *(Kicheko)*

Sasa ni matangazo ya vikao vya leo vya Kamati. Kuna Kamati tano ambazo zimepangiwa kufanya vikao vyake leo. Kwanza, ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti, anaomba niwatangazie Wajumbe wake kwamba kikao kitafanyika leo tarehe 19 Aprili, 2004, saa tano, chumba Na.219.

Pili, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athumani Janguo, anaomba niwatangazie Wajumbe kwamba, leo tarehe 19 Aprili, 2004 kutakuwa na kikao ukumbi Na.133 mara baada ya kipindi cha maswali kumalizika.

Tatu, Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)*, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa tano asubuhi, chumba Na.231.

Nne, Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Mgombelo, anaomba Wajumbe wakutane saa saba mchana, ukumbi Na.227 kwa ajili ya kukutana na Uongozi wa Shirika la Reli, *PSRC,* pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Tano, Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake, anaomba niwatangazie Wabunge Wanawake wote kuwa leo tarehe 19 Aprili, 2004 kuanzia saa saba mchana kutakuwa na kikao chumba Na.428, ghorofa ya nne.

Mwisho wa Matangazo ya vikao, tunaendelea na *Order Paper.*

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Taarifa Kuhusu Moto Uliounguza Makazi ya Rais

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Aprili, 2004, majira ya saa 11:50 alfajiri, moto mkubwa ulizuka katika Jengo la mMkazi ya Mheshimiwa Rais, lililoko eneo la Ikulu, Mjini Dar es Salaam. Jengo hilo liko upande wa Kaskazini mwa Jengo Kuu la Ikulu na haliungani moja kwa moja na Jengo Kuu la Ikulu.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo, moto huo ulianzia katika vyumba vya kulala vilivyopo ghorofani katika jengo hilo. Kwa bahati nzuri, wakati moto huo unatokea, jengo hilo halikuwa na wakazi ndani. Mheshimiwa Rais na familia yake, walikuwa Masasi kwa likizo fupi ya Sikukuu ya Pasaka. Walinzi waliokuwa wanalinda jengo hilo, walipoona moshi na dalili za moto, walitoa taarifa sehemu zote zinazohusika huku na wao wakifanya juhudi za awali za kujaribu kuuzima moto huo. Baada ya taarifa kutolewa kwa vyombo husika, magari ya Zimamoto yalifika eneo la tukio kutoka vikosi mbalimbali bila kuchelewa. Magari ya Zimamoto ya Jiji, Mamlaka ya Bandari, Uwanja

wa Ndege na hata kampuni binafsi ya *Knight Security and Rescue Services,* yote yalishiriki kikamilifu. Moto huo ulizimwa majira ya saa tatu asubuhi.

Hata hivyo, wakati moto huo unazimwa, ulikwishaleta hasara kubwa kwa jengo hilo. Kwa bahati nzuri kama nilivyosema, hapakuwa na wakazi ndani ya jengo wakati wa ajali hiyo na hakuna mtu aliyeumia wakati wa harakati za kupambana na moto huo. Hata hivyo, jengo hilo limeharibika sana. Paa lote limeungua kabisa na kuanguka na kuta za ndani zimeathirika vibaya hadi kupinda na kwa tathmini ya haraka, jengo hilo bila shaka litahitaji kujengwa upya kabisa. Kwa upande wa mali binafsi za Rais na familia yake, hakuna kilichoweza kuokolewa. Ukiacha vitabu vichache vilivyookolewa vutu vingine vyote viliteketea kabisa.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya moto kuzimwa, Serikali iliunda Tume ya Wataalam kutoka Idara mbalimbali na Taasisi zinazohusika, kuchunguza ajali hii mbaya ya moto. Ni mapema mno kusema chanzo cha moto huo ni nini hadi hapo uchunguzi utakapokamilika. Ningependa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, tuvute subira hadi hapo wataalam watakapomaliza kazi yao na kutoa taarifa. Tunajua Watanzania wamesikitishwa na kusononeshwa sana na ajali hii. Napenda kuahidi kuwa, Serikali itafanya jitihada zote ili uchunguzi huo uwe wa kina sana lakini pia ukamilike kwa haraka sana na wananchi kujulishwa matokeo yake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, vyombo na vikosi mbalimbali, vilifanya kazi kwa bidii na ushirikiano mkubwa wakati wa kupambana na moto huo. Juhudi zao sio tu zimeuzima moto huo kwa muda mfupi, bali pia zimesaidia sana kuudhibiti moto huo usisambae kwenye majengo mengine yaliyo karibu na jengo linaloungua hasa Jengo Kuu la Ikulu. Kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Watanzania wote, ninapenda kuvishukuru vyombo na vikosi vyote vilivyoshiriki katika kazi hiyo ya kuzima moto. *(Makofi)*

Aidha, kwa niaba ya Watanzania, ninapenda kumpa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Mama Anna Mkapa na familia nzima, pole nyingi sana kwa mkasa huu wa ajali ya moto uliowapata. Tunasema poleni sana, sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuiwasilisha taarifa hii kama taarifa fupi ya awali kuhusu ajali hii ya moto, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tukipata habari hizi za moto wa Ikulu katika magazeti tu lakini sasa kwa kuwa Bunge limepewa taarifa rasmi na Mheshimiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, sio vizuri Bunge lisiseme chochote, tukae kimya tu. Nafikiri ni vema Bunge liseme kitu. Kwa ajili hiyo, namwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge, aseme atakayoyasema kwa niaba ya Bunge. *(Makofi)*

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nasema kwa mara ya kwanza katika Bunge hili kwa wakati huu, ningependa nami niungane na wenzangu ambao

wamempa pongezi sana Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Kuchaguliwa kwa Mheshimiwa Mongella, kumeleta sifa kubwa sana na ya kwanza na ya aina yake kwa Watanzania wote na kwa Bara la Afrika. Namwomba Mwenyezi Mungu, amuongezee afya njema, maisha marefu na hekima ili aendelee kulitumia Bara letu la Afrika. *(Makofi)*

Pili, ningependa pia nimpongeze Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshughulikia mazingira, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. *(Makofi)*

Ningependa pia nichukue nafasi hii nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dr. Pius Ngw'andu, Mbunge wa Maswa na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Mawaziri wa Elimu ya Juu katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa ningependa nitoe mawazo kidogo kuhusu taarifa ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, nataka nimshukuru Waziri Mkuu na Serikali kwamba, jambo hili lilipojitokeza ni kweli kabisa watu walikuwa wanangoja wasikie Serikali inasema nini. Kwa hiyo, kwa niaba ya Wabunge wenzangu, nataka kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunajua kwamba hayo uliyoyasema ni baada ya wewe mwenyewe haraka ulipopata ripoti hiyo, ukaenda moja kwa moja Dar es Salaam kujionea mwenyewe, tunakushukuru kwa ripoti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa hiyo ya kusikitisha, ambayo imetolewa na Waziri Mkuu kwenye Bunge hili, napenda sasa niseme kwamba, naomba nitoe hoja kwamba, Bunge hili liipokee taarifa hii kwa masikitiko kama ilivyojitokeza. Pili, Bunge hili liiombe Serikali kama ilivyoahidi kwamba itaendelea kufanya uchunguzi na Kamati imekwishateuliwa na hatuna shaka kwamba uchunguzi huo utakuwa wa kina na baadaye taarifa itatolewa ili Watanzania waweze kujua chanzo hicho na hata baadaye hatua zitakazochukuliwa kuzuia mambo ya namna hiyo yasitokee tena kama kutakuwa na watakaohusika na uzembe basi wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kupitia kwako, Bunge hili likuombe wewe Mheshimiwa Spika, upeleke kwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na familia yake, pole zetu kwa mkasa mkubwa huu uliowapata na kama tulivyosikia kwa kupoteza karibu vitu vyao vyote vilivyokuwemo kwenye jengo hilo.

Mimi naelewa kwamba, kupotea huko kunamaanisha kwa mfano, kwa Wasomi vitabu vyote ambavyo Rais alikuwa amejiwekea kwa miaka vimepotea na vitu vya namna hiyo mara nyingi sio rahisi kuweza kuvirudisha pia na mali binafsi ambayo imepotea na kwamba Bunge hili baada ya kumpa pole kwa mkasa huo ambao umetokea, upeleke kwa Rais salamu zetu kwamba sisi Wabunge wote tunaendelea kumwombea Rais wetu afya njema na maisha marefu, ili aendelee katika kazi ya ujenzi wa nchi yetu ambayo hadi sasa ameifanya kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kunisikiliza na kuwaomba kwa nia moja kwamba, hii hoja niliyoitoa iweze kuungwa mkono na Wabunge wote ili kukuwezesha Mheshimiwa Spika, kupeleka salamu hizo za pole kwa Rais mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Kwa utaratibu wa Bunge kwa wale wasioelewa vizuri, hoja ikitolewa huwa inaungwa mkono angalau na Mbunge mmoja lakini leo Bunge Zima, Wabunge wote, wamesimama kuunga mkono, hajaipata kutokea. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nitatoa nafasi kwa Waheshimiwa wawili mmoja kutoka Kambi ya Wanawake, mmoja kutoka Kambi ya Upinzani ili nao wachangie kidogo hoja hii kabla hatujaiamua. Namwita Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba nichukue fursa hii ya kuunga mkono hoja nzito, yenye busara na umakini, iliyotolewa na Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ama kwa hakika Wabunge pamoja na wananchi wote kwa ujumla, tumeshtushwa na kuhuzunika sana juu ya mkasa huo wenye athari kubwa. Hata hivyo, sote tulifarijika sana tulipopata maelezo ya ziada kuwa, Rais wetu pamoja na mkewe, Mama Anna Mkapa, hawakuwepo wakati wa tukio hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunawajibika kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa haya yaliyotokea na naomba kwa ridhaa yako wakati tunamshukuru, tuongozwe na vitabu vyetu viwili vya Dini.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Tano ya Waraka wa Kwanza wa Paulo Mtume kwa Wathesalonike, mstari wa 16 - 18 una maneno haya...

**MBUNGE FULANI:** Naam!

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Nanukuu: “Furahini siku zote, ombeni bila kukoma, shukuruni kwa kila jambo maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu”. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Amen*.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, Nguzo ya Sita ya Imani ya Uislam inasema hivi: "Nakuamini kwamba mema na mabaya yanayokukuta wewe binadamu ni matakwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwako, *kheri wa shari mina-l-allah taala. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru wewe binafsi kwa kutupa nafasi ya kuweza kuzungumza mawili, matatu, kuhusiana na hoja ya Serikali pamoja na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Dr. Malecela, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na kwamba, sisi kama Kambi ya Upinzani, kwa kweli kama ulivyoona na kubainisha hapa Bungeni, tunaiunga mkono kabisa hoja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema baada ya kimya kirefu, hatimaye Serikali imetoa kauli kuhusiana na moto ulioiunguza Ikulu badala ya kuendelea kupokea taarifa za Vyombo vya Habari tu. Kambi ya Upinzani tulikuwa tunaendelea kushangaa kwani tangu Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipoliaga Bunge tarehe 13 Aprili, 2004 kwenda kushuhudia tukio, amerejea na akawa kimya na tumeendelea kuwa naye tu kwenye maeneo mbalimbali ya tafrija hapa na pale kama vile tukio lililotokea lilikuwa dogo tu. Kwa hiyo, tunapongeza kwamba, leo tumepokea taarifa na tumehakikishiwa kwamba, suala hili linaendelea kufanyiwa uchunguzi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuungua kwa Ikulu na hasa nyumba anayoishi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwenye Serikali, ambayo ina pesa nyingi, shilingi bilioni 102 zinakusanya kwa mwezi na ambayo ilipewa na Bunge hili zaidi ya shilingi bilioni 12 kufanya ukarabati, sasa kwa kweli ni jambo la aibu kwa Taifa na jambo ambalo limewashtua, kuwafedhehesha na kuwasikitisha Watanzania wengi, nje na ndani ya nchi. Katika hali ya jumla na mtazamo wa wengi, sio jambo la kupuuza na kuachia lipite hivi hivi bila kuchukua hatua kali na kujiridhisha na lugha tuliyozoea eti 'ajali haina kinga'. Kwa hiyo, hatua alizozungumza Mheshimiwa Malecela, tunaziunga mkono kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi kunapoungua nyumbani kwa Rais wa nchi ni wapi kwingine kunaweza kusiungue? Leo hii muda wowote ule sio ajabu hata jumba hili, Bunge pamoja na yaliyomo, Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Maofisa wa Serikali na wengineo, huenda wakaungua na kuteketea na hivyo mfumo muhimu wa kiutawala ukarejea kwenye ziro. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Serikali *must be serious to this issue.* Rais ndio kioo na taswira ya nchi, hebu fikirieni kwa afya aliyonayo Mheshimiwa Rais hivi sasa, huo moto ungemkuta chumbani kwake hali ingekuwaje, ingekuwa kashehe kubwa. Mungu ni mkubwa na Mizimu ya Mababu zake, Mheshimiwa Rais ni bahati alikuwa nyumbani kwao Masasi.

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza wote walioshughulika kuuzima moto huo, lakini pia ni vizuri sasa viongozi wetu wakaanza kujenga utamaduni wa kuwajibika kama zilivyo siasa za sasa za kiulimwengu zenye kuashiria Utawala Bora, kuwajibika kwa viongozi na hata kujiuzulu nyadhifa wanazokuwa nazo pindi matukio makubwa na ya kushtua kama haya yanapotokea. Ni jambo linalodhihirisha ustaarabu na ukomavu kwa utawala unaokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo si kwamba inaashiria kuwa mwajibikaji anakuwa ametenda jambo hilo moja kwa moja, bali ni kuonyesha kuguswa na jambo hilo na kuonyesha kwamba kwa mamlaka mhusika aliyokabidhiwa, alistahili kuweka mfumo au taratibu za kuzuia jambo hilo kabla halijatokea. Hivyo, kujiuzulu kwake au kuchukua hatua inayofanana na hiyo ni kutoa nafasi uchunguzi makini na sahihi kufanyika ipasavyo ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu na kuchukua hatua zinazostahili na pia ni kutoa nafasi na kuachia wenye uwezo na upeo ulio mkubwa wakaziba nafasi. Ndani ya jambo hilo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mfumo mzima wa Usalama wa Taifa, ni vizuri ukawajibika katika jambo hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu kwa bahati mbaya au nzuri, huwa anaona aibu kuwawajibisha watu ambao amezoea sana kuwa nao karibu. Tunamshauri Rais, endapo watu hawa wanaona aibu kuwajibika wenyewe, ni vizuri akakubali kumuua nyani bila kumwangalia usoni. Tume za kujiundaunda hazitatupa ukweli na badala yake zitatumika kuweka sawa mambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, matukio ya moto yamekuwa ni ya kufululiza mno kama ambavyo tumekuwa tunaona. Kuna usemi wa Kiitaliano usemao: *"Embwa teluga ommaiga keba etakaile mkila",* kwa maana ya kwamba, mbwa hatoki jikoni kama hajaungua mkia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini baada ya kuwa Ikulu anamoishi Mheshimiwa Mkapa na familia yake kuungua, ule mtazamo uliokuwa unaonekana kuendekezwa na Serikali wa kuwaacha wafu wazike wafu wao na hata tukirejea matukio ya Kilimanjaro, matukio ya *TANESCO* Ubungo, Benki Kuu, Wizara ya Mambo ya Ndani, *NASACO* na kadhalika, pamoja na matukio yenye utata ya kulipuliwa mabomu Zanzibar, sasa Serikali itakuwa *serious* na kutafuta ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mambo ya Serikali kuwa inakurupuka tu na kutoa maelezo yenye utata au wakati mwingine kuwarukia na kuwatuhumu hata wale wasiohusika, yaachwe mara moja na sisi wote kama Watanzania wenye kuipenda nchi yetu, tushirikiane na kusaidiana kutafuta mustakabali mzuri wa nchi yetu na hasa masuala ya usalama, utulivu na amani. Tukumbuke usemi usemao: "Ni heri kukinga kuliko kutibu". Tunashauri sasa vikosi vya kuzima moto viimarishwe na kupewa nyenzo za kisasa. Vikosi vya Zimamoto kwenye Halmashauri za Miji, Manispaa na Jiji viimarishwe tena kwani maeneo mengine vilifutwa na watumishi kupunguzwa eti ni kada zisizo muhimu. Mara nyingi imejitokeza kwamba, vikosi binafsi vya kuzima moto kila mara vikiitwa kushughulikia matukio ya moto huwa vinasuasua kuifanya kazi hiyo kwa kutaka kusainiwa mikataba ya malipo kwanza. *(Makofi)*

Mara nyingi hutokea ucheleweshaji mkubwa na pindi wanapokwenda kwenye tukio huwa wamechelewa na mali nyingi kuteteketea. Ni vizuri Serikali sasa kama inatambua kazi nzuri ambayo inafanywa na makampuni haya binafsi kama walivyoonyesha hivi sasa, ni bora iwekeane mikataba ya kudumu na Makampuni hayo ili yawe yakifanya kazi kwa haraka na bila kinyongo. Kwa uchumi wa sasa hivi, mkono mtupu haulambwi, kampuni hizi zina gharama zake. *(Makofi)*

Mwisho, tunaomba kujua, tumesikia kwamba Mheshimiwa Rais bado yumo ndani ya Ikulu hiyo hiyo iliyoungua, sasa isije ikawa suala hili likahamishwa toka mahali fulani kwenda kwingine. Tunaomba kujua usalama wa Rais pale alipohamishiwa. Pia maadam imetolewa kauli kabisa kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, mali zote binafsi za Mheshimiwa Rais zikiwemo nguo mbalimbali na kila kitu tunachokifahamu, kwa mtu ambaye anaunguliwa na nyumba, sisi tunaomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Taifa liguswe na jambo hili na kama inawezekana, Taifa limchangie chochote ili Rais asitembee uchi, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, vile vile nimepata michango ya maandishi kutoka kwa baadhi yetu lakini mmoja ningependa niusome, unatoka kwa Mheshimiwa Msindai, anasema: "Mheshimiwa Spika, Watanzania tunao utamaduni wetu wa kutoa pole kwa vitendo mahsusi. Hivi kuna ubaya gani Bunge tukikubaliana kutoa mchango mdogo wa kumsaidia Rais na familia yake? Najua Serikali itasaidia lakini sisi kama Wabunge, si vizuri tukatoa mchango wetu?". Sasa hilo halitazungumzwa hapa, tuna mkutano wetu wa Wabunge wote, ambao huwa tunazungumza mambo ya aina hiyo. Kwa sasa hivi napenda niwahoji ili tuamue ile hoja aliyoitoa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutoa Salaamu za Pole kwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, ilipitishwa na Bunge)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa Wanafunzi wa Vyuo na Elimu ya Juu wa mwaka 2004
### *(The Government Student's Loans Board Bill, 2004)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, walibaki Waheshimiwa Wabunge watatu, ambao hawajapata nafasi ya kuchangia nao ni Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, nawaita kwa mpangilio huo.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niwe....

**SPIKA:** Ngoja kidogo, Wabunge wanaokwenda kunywa chai waondoke. Unaweza kuanza sasa Mheshimiwa Isaac Cheyo na dakika zako zinaanza sasa.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi niwe mmoja kati ya watu ambao wanawapongeza wale wote ambao wamepata vyeo vikubwa vya Urais bila kimulimuli ikiwa ni pamoja na kaka yangu Dr. P. Ngw'andu, kuwa Rais wa Mawaziri kama ilivyosemwa na Dr. Malecela.

Mheshimiwa Spika, mimi sitakuwa na maneno mengi sana ya kuzungumza isipokuwa tu nasema hoja ambayo imewasilishwa ndani ya Bunge hili ni hoja ambayo tulikuwa tunaisubiri kwa muda mrefu tukizingatia kwamba *intake* ya wanafunzi wetu katika vyuo vingi hapa nchini ni ndogo sana. Kwanza haifikii hata elfu kumi kwa mwaka katika kipindi hiki ukilinganisha na nchi kama Kenya ambayo *enrolment* yao ni *about* 60,000 *students per annum* na wote wale wanaingia katika Vyuo mbalimbali. Kwa nini wanafunzi wetu ni wachache kiasi hicho? Ni kwa sababu vyuo vyenyewe ni vichache na *intake* yake ni ndogo, lakini pia ni kwa sababu wengi wanashindwa kwenda kwenye vyuo kwa sababu Serikali ilikuwa haina uwezo wa kuweza kuwasomesha wote.

Sasa Mheshimiwa Spika, umefika wakati ambao kweli watoto wote wa Kitanzania ambao wana sifa za kuingia Chuo Kikuu kwa kupitia Bodi hii ya Mikopo kwa wanafunzi, wengi waweze kupata nafasi ya kwenda kusoma. Hii pia tuione kwamba inakwenda sambamba na mfumo mzima wa elimu ambao sasa unatekelezwa hapa nchini kwamba tunakuwa na wanafunzi wengi wa shule za msingi ambao tunategemea mwakani au miaka inayofuata na wenyewe waingie katika mfumo kama ule wa MMEM ambao watakuwa wanafunzi wengi zaidi ambao wanasoma shule za msingi na baadaye watakuwa wanafunzi wengi zaidi wanaingia katika vyuo vya elimu ya juu na kwa mpango huu hata wale watoto wa maskini wa kawaida wanaweza kupata nafasi ya kuingia

Mheshimiwa Spika, tatizo langu ni namna gani *formula* hii itafanyika. Kwa sababu mara nyingi sana tumezoea watu wa aina fulani tu, watu wakubwa, watu wenye uwezo ndiyo wanaweza kupata mikopo. Mimi nataka kusema kwamba mikopo hii itakayotolewa kwa wanafunzi i-*take cross section,* hata mtoto wa maskini akiwa na *qualifications* tu, aki-*make application* yake iwe *considered* na aweze kuingia kupata mkopo ule na aingie Chuo Kikuu bila matatizo yoyote yale.

Mheshimiwa Spika, wengi wetu hapa pamoja na Mawaziri na watu wengine wote hapa tumepata elimu ya juu bure pamoja na ndugu yangu pale Dr. Sakila, tumekwenda *University,* tumesoma bure, tukapata kila kitu bure, pamoja na kwamba tulikuwa tunaongezewa na pesa ya kukaa Chuo Kikuu japokuwa ni ndogo, shilingi mia tano, lakini wakati ule ilikuwa ni hela nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, sasa tuangalie katika ule utaratibu ambao Mheshimiwa Waziri ameuzungumzia namna gani hawa watapata pesa. Ili Bodi iweze kuwa na hela za kutosha, mimi nilikuwa na-*suggest* kwamba moja ya njia kubwa kabisa ya kuweza kuongezea pesa kwa Bodi hii ili kutoa mchango wetu kwa Watanzania wengi ambao wanahitaji elimu ni pamoja na wale wote ambao walisoma kwa kodi ya wananchi wafanye kazi ya kuchangia. Mimi nilifikiria kwamba ingefaa zaidi leo hii wale wote ambao walisoma bure na wenyewe wakaonyesha mchango wao wa hela kidogo kusaidia Mfuko huu ili watoto wengi waweze kusoma. Mawaziri ambao wamesoma bure Chuo Kikuu hata ndugu yangu hapa ambaye ni *Clerk* kwenye Meza yake Mheshimiwa Spika, hawa walisoma bure. Sasa tutoe mchango wetu *ten percent* ya mishahara yetu hata kama ni kwa miaka miwili kwa ajili ya kuchangia Mfuko huu wa elimu, iwe kwa wote Ma-*principal Secretaries* na kadhalika, wote wachangie ili hela nyingi ziweze kupatikana ili kuweza kusomesha watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hiyo tu, kuna mashirika makubwa makubwa hapa nchini yanachimba madini, yanabeba almasi yetu, yanabeba dhahabu na kila kitu lakini hayachangii chochote kwenye elimu ya nchi hii. Ingekuwa ni jukumu zuri zaidi kungekuwa na *formula* kwamba hawa wote ambao wanachimba dhahabu, almasi na kadhalika, walipe *education levy* ili iweze kwenda kwenye Mfuko huu ili waweze kuchangia elimu kwa ajili ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hii nai-*support* moja kwa moja, nimesema sina kitu cha kuzungumza zaidi ya hayo, ninachosema tu *blessing,* Mungu hili na alitengeneze, watoto wetu wasome. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie katika Muswada uliopo mbele yetu, Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu wa Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukushukuru nichukue nafasi hii kwa sababu na mimi naongea kwa mara ya kwanza katika Mkutano huu, kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamechaguliwa kushika nafasi za Urais katika nafasi za Kimataifa. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Nafasi ambayo ni ya kwanza na nafasi hiyo ikatolewa kwake kwa mama wa kwanza katika Afrika. Mimi nampongeza sana, namwombea afya nzuri na Mwenyezi Mungu ampe busara ili aweze kutimiza majukumu yake ya Urais wa lile Bunge la Afrika kwa mafanikio ya kuweza kumpandisha zaidi labda baadaye katika ngazi za Kimataifa katika Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mazingira, kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Nafasi aliyopewa ni nafasi ambayo inaweka nchi yetu katika mazingira mazuri ya heshima na kazi yake ambayo amekuwa akiifanya katika nafasi hiyo. Nina imani kabisa mazingira yetu ya Tanzania kwa jinsi yalivyo yatampa

nafasi nzuri ya kuweza kuyaboresha ili kuweza kupunguza kiwango cha umaskini kinachotokana na mazingira mabovu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu vile vile kwa kuteuliwa kwake kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu katika Bara la Afrika. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili niendelee kuchangia Muswada uliopo mbele yetu, nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ngw'andu, pamoja na Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya katika hiyo Wizara. Napenda niwapongeze kwa dhati kwa mchango wao ambao wametoa kwa kuweza kuboresha elimu kwa Chuo Kikuu Huria *(Open University of Tanzania).* Hivi sasa wapo vijana wengi ambao wanapata elimu kwa bei nafuu ya karibu laki moja na hamsini kwa mwaka kitu ambacho ni gharama ndogo sana. Walimu na wataalam wa fani mbalimbali wanapata elimu kwa gharama nafuu sana na mtu anayepata elimu pamoja na kusoma elimu yake anayopata ni ya thamani kubwa kwa sababu si elimu ya nadharia peke yake lakini inakwenda sambamba na elimu ya vitendo. Sasa nafahamu katika ile Ofisi ya Rais katika Menejimenti ya Utumishi wote wanaosoma Chuo Kikuu Huria wanalipiwa na Wizara yao. Vyuo vya Elimu wanalipiwa na Wizara yao lakini walimu walioko mashuleni bahati yao mbaya hawalipiwi na Wizara yao. Nafikiri na wao wangefikiriwa kulipiwa na Wizara yao kwa sababu hata Serikali za Mitaa wanalipia watu wao wanaosoma *Open University of Tanzania.* Gharama yake ni ndogo na hakuna sababu kwa nini Serikali isichangie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo ungekuwa ni mkopo nafuu, nauita mkopo nafuu usio na masharti. Huu unaoletwa katika Muswada huu ni mkopo mgumu wenye masharti magumu na ambayo nitaelezea kidogo katika mchango wangu. Kwa hiyo, ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri kama angependa huu mkopo mgumu uweze kuwasaidia Watanzania, atoe nguvu zake zote katika kusaidia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mimi sina mgogoro na Muswada huu kwa sababu lengo lake ni kuwasaidia Watanzania wetu. Nikisema nina mgogoro nafikiri nitakuwa naifanyia Serikali yangu na wananchi wetu kitu ambacho si sahihi, kwa sababu kwanza Bodi yenyewe haijaanza kufanya kazi, kwa hiyo tukianza kuishutumu tunashutumu kitu ambacho hakipo. Tunachoweza kufanya ni kutoa ushauri. Kwa hiyo, ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri katika Muswada huu katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kuhusu masharti ya mikopo katika ibara ya 18 na 19 na pili, mazingira ya mikopo inayotolewa katika Ibara ya 21 na 22. Sasa nianze na masharti. Kwanza suala la ajira ya uhakika, wale ambao watakuwa wanakopeshwa kutokana na Bodi hii wakimaliza dhamana yao bila shaka itakuwa vyeti vyao. Lakini vile vile hawatakuwa na dhamana ya kutosha kulipa ule mkopo kama hawatapata ajira. Sasa hivi ajira katika nchi yetu bado inasua sua na ni ngumu. Sisi Watanzania tumeingia katika ushirikiano na wenzetu wa Afrika Mashariki Kenya na Uganda, mahali fulani nina imani tutakuwa na an open labour market na hii itatufikisha mahali ambapo competition itakuwa ngumu, wale tunaowakopesha je, tuna uhakika watapata ajira? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, hata wakipata ajira viwango vya mishahara ni vidogo. Mtu unayemkopesha unamlipa mshahara mdogo, sisi ambao tulisomeshwa bure ambao tumeita ni bure, mimi sipendi kuita bure, nasema tulisomeshwa kwa kodi za wananchi wa Tanzania. Hatuwezi kuita bure kwa sababu tulitumia fedha za nchi hii, ni gharama. Kwa hiyo siyo bure ilikuwa mikopo ambayo haina kulipa wala *interest,* ilikuwa mikopo tu ambayo mtu ulikuwa unachukua, unasoma halafu ukimaliza unakwenda kufanya kazi na ukifika katika kufanya kazi huna argument juu ya mshahara utakaolipwa. Unalipwa labda shilingi elfu nane au kumi wakati ule mishahara ilikuwa midogo, lakini tulikuwa tunaridhika. Uende National Service, ukafanye nini, unakubali, mishahara ilikuwa midogo, lakini tukishaanza kufikia hali ya mtu kukopa kwa ajili ya elimu yake kuanzia degree mwaka wa kwanza, wa pili na wa tatu halafu ukapewa mshahara mdogo ili ukalipe ule mkopo hapo ndiyo mgogoro utaanza.

Kwa hiyo Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Serikali ingejiandaa sasa kulipa mishahara ambayo inalingana na elimu ya hawa watu katika viwango ambavyo ni vya Kimataifa badala ya kuongelea suala la uwezo maana yake Serikali inasema mishahara midogo, uwezo mdogo, sasa mtu akishajisomesha kwa gharama zake, Serikali nayo ikubali kwamba suala la mshahara kulingana na uwezo halipo, litakuwa ni suala la mishahara kulingana na thamani ya elimu ya yule ambaye analipia mkopo ule. Lingine ambalo Serikali ingeangalia ni kuhusu masharti ya yule anayepewa mkopo. Anaweza kufukuzwa kazi kule alipoajiriwa, je, ataendelea kulipa ule mkopo vipi? Hilo nalo lingetafutiwa nafasi yake ndani ya Muswada huu ikiwa amefukuzwa itakuwaje. Labda amefukuzwa shule vile vile mwaka wa pili na kwa kushindwa masomo, kwa hiyo akaondoka shuleni, ile miaka miwili atailipia vipi? Hayo ni mambo ambayo bila shaka yataangaliwa katika utendaji ama ndani ya Muswada huu. Nafikiri hilo ni jukumu la Waziri kuliona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu mdhamini wa mkopo, guarantor. Ukiangalia katika ibara ya 22. Muswada unaeleza kwamba guarantor anaweza kuwa mzazi, mlezi au msamaria any person, nadhani ana maana msamaria mtu ambaye ana mapenzi mema tu na huyu anayeomba mkopo. Lakini mimi nafikiri tukiangalia hali halisi ya watu wetu na umaskini wao dhamana ya maskini ni maisha yake na uhai wake yeye mwenyewe, ndiyo maana wanasema hivi tajiri na mali yake na maskini na mtoto wake. Ukimwuliza maskini msingi wake mkubwa atakwambia ni mtoto, watoto wakue basi Mungu ataleta riziki ama neema ikitokea. Kwa sababu hata huo umaskini tunaoongelea hapa una ngazi zake tofauti au una viwango vyake. Kuna watu wanaishi in absolute poverty, hata pakuishi ni shida. Sasa huyu anakwenda kuomba dhamana atapewa dhamana na nani hata huyo ambaye ni msamaria anataka kutoa dhamana atatoa dhamana kwa mtu ambaye anafikiri kesho kama dhamana haikupokelewa anaweza akalipa. Ningeomba Mheshimiwa Waziri akaliangalie hili kwa sababu tuna vijana ambao wana uwezo mzuri sana wa elimu lakini wazazi wao wanaishi in absolute poverty. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu utatuweka mahali pa kuacha watu wa namna hii wenye haki za uraia wao bila kupata elimu ambayo wangetarajiwa kuipata. Kwa hiyo, Muswada huu usije ukawaweka watu hawa katika njia panda ya kuwaweka mbali na haki

zao za uraia. Kwamba hana mtu wa kumpa dhamana kwa sababu he is living in absolute poverty na nafasi hii ikawekwe waziwazi kabisa kwamba watu ambao wanaishi katika *absolute poverty* watawezaje kupata access na mikopo hii ambayo masharti yake mimi nasema ni magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu adhabu kwa ajili ya waajiri ambao watashindwa kurejesha ile mikopo ya watu waliowaajiri. Waajiri wengi wataanza kuajiri tu wale ambao wamejisomesha wenyewe, wakaona hawa wengine kama wana ukoma kwamba nikimwajiri huyu nikishindwa ku-remit michango yake ya kila mwezi maana yake ni kwamba nitashtakiwa ama nitapigwa faini ya shilingi milioni moja. Kwa hiyo, ili kuondokana na hiyo adha anamwuliza kwanza bwana wewe ni mtu wa masharti ya mkopo? Akisema ndiyo, atamwambia kazi hakuna. Kwa hiyo Muswada uangalie vile vile haya mazingira ya kumweka mwajiri katika eneo hilo itakuwaje. Kule kwetu tuna gypsum, tukapitisha sheria ndogo katika Halmashauri kwamba wale wanaonunua gypsum yetu watulipe kodi kidogo waikusanye kule, wai-*remit* kwetu, wale wakasema hatuna haja ya kuchukua gypsum ya masharti, kuna ambao wana gypsum haina masharti, tukabaki tupu. Kwa hiyo tukaangalie hili eneo vizuri. *(Makofi)*

Lingine ni kuhusu hawa wanafunzi wanaosoma, ningefikiri Mheshimiwa Waziri aweke mazingira kwamba vijana hawa wanapokuwa shuleni wapate nafasi ya kufanya kazi wakiwa shuleni ili kuwawezesha kupata kitu kidogo, hata Ulaya wanafunzi wanaosoma kule wanapewa nafasi ya kufanya kazi, kuuza madukani, kufanya kazi hotelini na kila mahali katika viwanja vya ndege. Siku hizi kuna watu wanaajiriwa kuuza maduka hawana *qualification.* Sasa kama tunaingia kwenye utandawazi iwekwe sheria kwamba wanafunzi wawe na haki wakati wa likizo kupata ajira ndogo ndogo za kuwawezesha kupata kipato ili kuweza kupata gharama za kuweza kulipia elimu yao na mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ningeomba Serikali kwa makusudi kabisa iweze kuchangia katika Mfuko huu wa mikopo ili wanafunzi hawa watakaokopeshwa wasilipe gharama zote za masomo yao kwa miaka mitatu kwani ni fedha nyingi. Serikali ifikirie itagharamia kiasi gani kwa sababu hawa watu bado wanakuja kulitumikia Taifa, kwa hiyo haijafika wakati wa kusomesha watu kama zamani, kama tunavyosema kwamba ilikuwa bure, lakini ilikuwa ni kwa kodi za wananchi, lakini kwa sasa hivi Serikali ikubali kutenga sehemu ya bajeti yake kila mwaka kwa ajili ya Mfuko huu wa mkopo ili wale wanaokopeshwa wasibebe mzigo wote hundred percent wabebe kwa percent fulani. Lakini tukisema vijana hawa wajisomeshe wenyewe a hundred percent gharama zake ni kubwa na hata wakianza kazi watakuwa wanaishi maisha magumu ya kuwafikisha katika mauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, wasomi ambao walisomeshwa na Serikali yetu na baadaye wakaenda kufuata *green pastures* walitumia kodi za wananchi wa nchi hii, sasa wao wanapata malipo ya fedha nyingi kule, wanakuja kuwekeza ndani ya nchi yetu. Naomba Serikali ifikirie fedha zinazotoka nje za watu wetu wanaotaka kuwekeza hapa lazima ichukue *tax* kidogo kwa sababu hapa wameondoka hawakutoa mchango wowote kufuatana na elimu waliyopewa. Tulifika pale Chuo Kikuu cha Sokoine,

madaktari karibu hamsini wapo nje ya nchi katika *green pastures.* Lakini tulipowahoji wanasema malipo hapa ni kidogo, wanaishi kwa fedha za *research.* Kama sasa Serikali haiwezi ikawalipa kulingana na elimu yao basi wale walioko kule ambao walisomeshwa kwa gharama za nchi hii wanapotaka kuja kuwekeza Serikali i-*tax* kidogo fedha yao wanayoingiza ndani ya hii nchi ili kuweza kuweka mstari, *demarcation* ya hawa vijana ambao sasa hivi wakisoma wasiwe na tamaa ya kwenda nje kupata *green pastures* wakati wamepata elimu yao kwa kusaidiwa na fedha za Serikali halafu baadaye wasichangie maendeleo ya nchi hii.

Baada ya kusema hayo nina imani muda ulionipatia umekwisha na hivyo napenda tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kutuletea Muswada huu ambao utasaidia maendeleo ya elimu ya juu katika nchi yetu. Nawapongeza sana na mimi nakubali Muswada huu na kuunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami naomba niungane na wenzangu kabla sijaanza kuchangia niwapongeze wenzetu waliochaguliwa kuwa Marais katika nyadhifa mbalimbali kutokana na Bunge hili. Kwanza kabisa ningependa nimpongeze Mheshimiwa Mama yetu Getrude Mongella ambaye amechaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Mimi ningependa kusema kwamba kuchaguliwa kwake kumeleta heshima kubwa kwa nchi hii pamoja na kuonyesha jinsi ambavyo wanawake wa Tanzania wanaheshimika katika nyanja za Kimataifa. Napenda kumpongeza sana. Pili, ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Mimi ningependa nimwambie kwamba wadhifa huu unaonyesha jinsi ambavyo wenzake wanathamini kazi yake, hivyo aendelee kufanya kazi yake vizuri katika mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Dr. Pius Ngw'andu jirani yangu kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu ya Juu kwa heshima kubwa. Naamini kwamba kuchaguliwa kwake kunaonyesha jinsi ambavyo yeye kama Waziri wa Elimu ya Juu na Teknolojia anavyofanya kazi yake vizuri na anavyoeleza mikakati yake vizuri ambayo ni mikakati ya Serikali ya Tanzania kwa wenzake. Ningependa niseme hivi ninawaombea Mwenyezi Mungu awape hekima na busara katika kutekeleza majukumu yao haya mazito waliyopewa kwa sababu wasipotekeleza vizuri heshima tuliyopewa basi itakuwa imeingia mashakani. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kwa niaba ya wanawake wa Morogoro kumpa pole nyingi sana Mheshimiwa Rais na familia yake kwa janga la moto lililotokea katika makazi yake. Sisi tutaendelea kumwombea Mwenyezi Mungu aendelee kumfariji yeye pamoja na familia yake na Mwenyezi Mungu amrudishie zile mali zake ambazo amezipoteza. Tunaamini kwamba kwa uadilifu wake bado Mungu ataendelea kumbariki na kumlinda yeye na familia yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu na Teknolojia pamoja na Naibu Waziri wake, wataalam wake na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kufanya kazi nzuri ya kutengeneza Muswada huu ambao umefika kwa wakati muafaka wakati ambapo Watanzania wengi wanahangaika kuwapatia watoto wao elimu. Nisiwasahau pia wenzetu wa Kamati husika, mara nyingi tunawasahau wanakamati wanaojadili Miswada. Nina imani kwamba bila wao Miswada mingi isingekuwa imeboreshwa vizuri, hawa wenzetu kwa kweli wamefanya kazi nzuri ya kuboresha Muswada huu. Napenda kuwapongeza. Baada ya pongezi pamoja na kuunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja ningependa kutoa mchango wangu na maoni machache kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kuangalia ibara ya 16. Ibara ya 16(2) ningeomba kama itawezekana kiongezwe kifungu kidogo cha (f) ambacho kitasomeka: *"Transport and travel expenses"*. Kwa nini nimefikiria hivyo? Nimefikiria hivyo kwa sababu watoto wetu wengi wanatoka mbali na vyuo vikuu. Vyuo vikuu vingi vipo kwenye kona moja ya nchi hii. Wanafunzi watasafiri kutoka kona zote za Tanzania kwenda kuhudhuria masomo yao, sasa tusipowapa usafiri watasafiri namna gani. Wengi wao wanatoka katika familia ambazo kwa kweli hali zao za kiuchumi siyo nzuri sana. Hivyo basi kama Taifa limeamua kuwawezesha basi tuwape na mikopo ya usafiri ili waweze kuwa wanahudhuria masomo yao kwa wakati muafaka isiwepo sababu ya kwamba nimekosa usafiri wa kuondoka kurudi shuleni au kurudi makwetu. Naomba hilo liangaliwe kama kuna uwezekano basi hiki kifungu kiongezwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni katika ibara ya 17(a) kwamba masharti ya kupewa mkopo, huyu mtu awe Mtanzania. Naanza kujiuliza huyu Mtanzania tunahakikishaje kwamba ni Mtanzania. Kwa masikitiko naomba kusema kwamba kuna wenzetu ambao tulisoma nao Chuo Kikuu, tukalipiwa kwa jasho la walipa kodi wa nchi hii. Baada ya kumaliza wakajiona kwamba kumbe wao wanatoka nchi zingine za jirani, wameondoka wamekwenda kutoa huduma katika nchi hizo ambazo walikuwa wanafikiri kwamba wao ni wazawa wa kule. Mimi naomba suala hili la uraia liangaliwe pia kwa mtazamo mwingine mpya hasa wakati huu ambao tuna Watanzania wengi ambao wanakwenda kujiandikisha kupata vyeti vya kuzaliwa kwa kutumia hati za viapo *affidavit.*

Mheshimiwa Spika, hizi *affidavit* ni kiasi tu cha mtu kumpa chochote mzee mmoja mahali, akaapa kwa miungu yake na mizimu yake kwamba alimfahamu baba yako na alimwona anazaliwa. Mimi naomba hilo liangaliwe upya namna ambavyo tunaweza kuboresha na kuthibitisha Utanzania wa watu wetu hasa kipindi hiki ambacho wengi wetu walizaliwa nyakati ambazo hatukuwa tunatilia umuhimu kuwa na vyeti vya kuzaliwa au kuandikisha watoto wetu. Hilo liangaliwe upya kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pia ningependa tuliangalie kwa makini ni kwa maeneo yetu ya mipakani. Tuna makabila ambayo yanaishi Tanzania na yanaishi upande mwingine wa mpaka. Ukoo huo unakuwepo upande huu na upande ule mwingine wa nchi yetu. Sasa itakuwa ni vigumu sana kuweza kupambanua kwamba ni Mtanzania yupi ambaye ni raia wa kweli wakati tuna makabila ambayo yana *move around* kutoka Tanzania kwenda Kenya au kwenda Uganda au kwenda Msumbiji na kurudi nchini.

Naomba hilo liangaliwe kwa makini pia na tuangalie namna ambavyo tunaweza kudhibiti wale Watanzania ambao wataingia humu ndani kwa sababu wanazungumza lugha na wana mila na desturi kama makabila ambayo yapo huku Tanzania.

Lingine ni kifungu cha (b) katika ibara hiyo hiyo. Tunaangalia umri wa ambao watakuwa ni *illegible* katika kupata mkopo huu. Ni vizuri kwamba kuingia kwenye Vyuo Vikuu vile ambavyo vina muda maalum wa kusoma wameweka miaka arobaini na tano lakini pale ambapo inasema kwamba miaka isiyozidi sitini kwa wale wanaoingia kwenye Chuo Kikuu Huria. Inawezekana basi tukafika mahali sisi wengine tutakapofika kustaafu ama tunaona kwamba hatuwezi kufanya shughuli nyingine basi tukajiandikisha kusoma, Chuo Kikuu Huria sijui kinachukua muda gani, lakini najua kwamba kinaweza kuchukua *a minimum of six years.* Sasa baada ya kufikia umri wa miaka 70 mara nyingi hata ajira hatupati, hata kama tukisema tutajiajiri wenyewe hiyo kazi tutafanya kwa muda gani ili tuweze kulipa huo mkopo kwa muda wa miaka kumi na tano.

Naomba hiyo *age ceiling* ya Chuo Kikuu Huria iangaliwe tena upya kwa sababu nia ni kusomesha vijana wetu. Yule ambaye anaona kwamba ana umri mkubwa na anataka kuendelea kusoma nafikiri atakuwa na uwezo wa kujilipia zaidi. Kwa hiyo, kipaumbele tuwape vijana wenye umri usiozidi miaka arobaini na tano kama kweli tunakuwa *serious* kwamba tunataka kuwa na Taifa lenye watu ambao wamesoma ambao watakuwa wanafanya kazi yenye tija katika Taifa hili. Pamoja na kuangalia pia kwamba *the life span* ya Watanzania haizidi miaka 57, sasa hivi imeteremka mpaka 47. Sasa kweli tukianza sasa kuwapa wale wachache ambao Mungu ameamua kuwakopesha umri tukaanza kuwapa pesa za kusoma, vipi Mungu akiamua kwamba ule mkopo wa umri anauondoa? Tutakuwa tunapoteza kile kidogo tulichonacho. Naomba huu umri uangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lingine linakuja pale kwenye masharti ya udhamini na dhamana. Tunapofika kwenye udhamini na dhamana ninaanza kuangalia mila na desturi zetu za Waafrika kwamba mwanaume anathaminiwa kuliko mwanamke.

Tukienda vijijini ni mzee gani katika kijiji atasema kwamba anaweka dhamana nyumba yake au shamba lake kwa ajili ya kumsomesha mtoto wa kike, ni wachache sana. Naomba hilo liangaliwe upya kwamba basi ikiwezekana hasa wanawake wajidhamini wenyewe. Linakuja suala la mwanamke ambaye ameolewa akaanza kupata matatizo katika ndoa na ana moyo wa kutaka kusoma.

Mheshimiwa Spika, itafika mahali hata yule mume wake ataanza kumfanyia fujo aweze kuweka dhamana kile ambacho wametafuta pamoja na yeye. Naomba kuwepo na *exception of rule* kwamba wanawake wapewe kipaumbele katika kuwa *considered* na tusiangalie sana mambo ya udhamini na dhamana, wajidhamini wenyewe na waji-*guarantee* wenyewe, na dhamana iwe ni cheti chake ambacho anakipata kutoka shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inakuja lile suala la kwamba mkopaji atalipa mkopo wake pale anapomaliza masomo yake au anapokuwa *discontinued.* Nashukuru kwamba

Mheshimiwa John Singo amezungumza hilo. Lakini inafika mahali anapokuwa *discontinued* mwanamke hata akirudi kule kwa baba yake hana hata shamba ambalo yeye anaweza akalifanyia kazi ili aweze kulipa mkopo. Sasa sijui suala hilo linakuwaje?

Suala lingine ni lile la kulipa mkopo unapoajiriwa au unapojiajiri wenyewe biashara ambayo ni l*icensed.* Sijui kwa nini hiyo *condition* ya *license* imekuja kwa sababu, mimi naweza nikawa mkulima, wanaomaliza kusoma hasa wale wenzetu wa Chuo Kikuu Cha Sokoine, wakaenda wakaanza shughuli zao za kutibu ng'ombe, kimya kimya vijijini, hawana leseni. Wengine tuseme wakaamua kulima mashamba yao kule vijijini hawana leseni, sijui hao tunawatafuta namna gani? Kuna wengine wamemaliza hata mpaka *Masters Degree* ukienda sokoni wanakuwa na viringe vya kuuza, vile viringe havina leseni vinalipiwa tu kodi katika Serikali za Manispaa au za Miji. Naomba pia kwenye hilo suala uangaliwe mtindo wa kuweza kumfuatilia mtu yeyote ambaye amemaliza ana mkopo na ana njia mbalimbali ya kujipatia kipato siyo kile kipato ambacho ni *license* ama *formal Employment*.

Mheshimiwa Spika, lingine ningependa kuzungumzia mazingira wanayosoma hawa vijana. Pamoja na kuwapa mikopo tunataka wasipate *Supplementary* tena wala wasikariri miaka. Sasa hayo mazingira wanayosomea sijui kama Mheshimiwa Waziri ameamua kuyatembelea wakati fulani. Unakwenda kwenye sehemu nyingine unakuta wanafunzi wamesimama madirishani wanamsikiliza l*ecturer* wanaandika *notes,* wengine hawana mahali pa kukaa huo ni ukweli mtupu. Unakwenda katika madarasa mengine kuna wanafunzi 600 wamekaa, kuna *lecturer* ambaye anaamua kuzungumza kwa Kiingereza kigumu sana akijua kwamba wanafunzi wetu hawaelewi kiingereza vizuri. Anazungumza kwa kutumia kipaza sauti ambacho kinatoa mwangwi, kina *echo.* Kwa hiyo, wanafunzi wanatoka kapa kabisa na kwa sababu hiyo ndiyo unakuta kwamba kila *semister* inayopita unakuta katika kozi fulani wanafunzi 30, 40 wanapata *discontinuation.*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pamoja na kuwapa sasa mikopo hawa wanafunzi wetu, basi Wizara husika iangalie kwamba mazingira wanamosomea hawa vijana wetu, na mazingira wamoishi hawa vijana wetu yanakuwa ni mazingira yanayowapa motisha kuweza kusoma na kuweza kupata mafanikio mazuri.

Mwisho kabisa Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia suala la udhamini kwa watoto yatima. Hawa watoto yatima unakuta kwamba wengi wao wanafundishwa na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. Naomba kusema kwamba mimi Shirika langu limedhamini wanafunzi kama 20. Lakini kwa mtindo huu wa sheria sasa hivi ninaomba kusema kwamba mimi nitaogopa hata wenzangu wa Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali wataogopa kuwadhamini hao watoto, kwa sababu itakapofika mahali wakashindwa kulipa mikopo, ile dhamana ambayo Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo ni omba omba tu, tunaomba fedha kutoka kwa wafadhili ili kuweza kuwasaidia watoto hawa, tutalipaje hizi fedha za Serikali? Naomba kwamba iangaliwe kama inawezekana watoto yatima wanaweza wakadhaminiwa na viongozi wa dini. Kwa sababu viongozi wa dini wako pale pale na wapo katika jamii ambayo wakiona mambo yanakuwa magumu wanaweza wakaomba waumini wao wakachangia au wakaanzisha mifuko maalum katika

makanisa na misikiti ya kuweza kuwaondolea hawa watoto yatima mzigo wa kulipa madeni.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuishauri Wizara husika katika kufuatilia hii mikopo tusitegemee ile Bodi ikiwa Makao Makuu yake Dar es Salaam wanaweza kweli wakafuatilia hii mikopo kwa njia ambayo italeta mafanikio. Ninaomba watumie mfumo wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwamba katika kila Mkoa kuna mwakilishi wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na wale ambao wanatarajia kumaliza kila mwaka katika Mkoa ule ama Wilaya ile hawa watu wapelekewe majina yao kusudi wakishirikiana na uongozi wa Serikali za vijiji na Wilaya waweze kuwafuatilia ili waweze kujua kwamba hawa vijana baada ya kumaliza masomo yao wamekwenda wapi, wameajiriwa, wamejiajiri na wanawezaje wakaanza kurudisha hiyo mikopo. Kwa mfumo huo wa ushirikiano Inter-ministerial collaboration tunaweza tukawa tumefuatilia vizuri sana hii mikopo ili Serikali isije ikaendelea kupoteza fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, mimi ningependa kuitakia hii bodi ambayo haijatengenezwa, itakapotengenezwa mafanikio. Namwombea pia afya njema Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na viongozi wake wengine ambao nina hakika kabisa kwa nia njema watahakikisha kwamba Watanzania walio wengi na vijana wetu watapata fursa ya kupata mikopo ili waweze kusoma. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kwa maandishi. Mpango mzima wa Serikali kufikia uamuzi wa kutoa mikopo kwa wanafunzi kwenye elimu ya juu nauunga mkono. Mikopo hii itolewe kwa wanafunzi wa vyuo vyote nchini yaani vyuo vya Serikali na watu binafsi. Maoni yangu kwenye Muswada ni kama yafuatayo:-

Kimapato sisi Watanzania tuko chini sana, kwa hiyo, Bodi yenyewe inapashwa ijiweke vizuri kubaini wale wanaostahili kupewa mkopo. Kukiongezea nguvu kifungu cha 6(b), Mjumbe *(Director of Technical Education),* chini ya kifungu 5(1)(c) aondolewe kwani anawakilishwa na *The Director of Higher Education* chini ya kifungu hicho hicho (b). Badala yake nafasi itolewe kwenye Idara ya *Rural Development* ya Benki Kuu au Ustawi wa Jamii. Idara hizi zinayo picha ya kila siku ya hali yetu na pia kipato chetu Watanzania. Kifungu cha 6(c) naomba kifungu hiki kiongezewe nguvu zaidi sehemu ya kurudisha mikopo *(repayment)*. Kama mikopo haitarudi, Mfuko utakwama *(Revolving Fund Characteristics).*

Kwenye sehemu ya III kifungu 7(I)(h) kwamba, mikopo kwa wanafunzi ubebe riba *(interest).* Hali hii inatuletea mazingira ya biashara, ningeshauri kama hatua ya kutunza thamani ya fedha, utumike mtindo wa *to pay the money to the U.S.A. Dollar or items of value,* ili thamani ya shilingi atakayokopa leo mwanafunzi ibakie na thamani hiyo hiyo miaka mitano ijayo au zaidi. Riba wakati wote inawakilisha ongezeko la fedha

na wala siyo kutunza thamani ya fedha tu. Kwa hiyo, nashauri kwamba, Serikali iachane na mtindo wa kutoza riba kwenye mkopo wa elimu kwa wanafunzi wanaotafuta elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sehemu ya IV ambayo inaainisha majukumu mbalimbali kwa wahusika mbalimbali, naomba pia nitoe maoni kwamba, kifungu cha 16(1) ambacho (2) kinasema: *"The financial assistance under section (1)"* tuongeze *sub-section (f) "Medical expenses"*. Nyongeza hii itamweka mwanafunzi kwenye hali nzuri ya kuwa na *package* kamili ya kumwezesha kuendesha masomo yake.

Mheshimiwa Spika, kawaida *life-expectance* ya Mtanzania ni miaka 55. Kwa hiyo, kifungu Na. 17(b) kinasema: *"Student admitted to the Open University of Tanzania and he is not more than sixty years of age."* Hali hii inaonekana ni hatari kubwa kwenye mkopo. Nashauri umri wa kukopesha usizidi miaka 50 kwenye *Open University of Tanzania* ili kuepuka mikopo mingi kupotea. Hali hii itaendana na hali halisi ya Benki zote kwamba hazikopeshi mzee.

Mheshimiwa Spika, kifungu Na. 18(2) kinamfunga mkopaji mwanafunzi kwenye ukiritimba mkali. Anapaswa awe na *collateral* yaani kitu cha kuweka dhamana. Zaidi ya hapo ni moja ya njia za dhamana kama mkopaji mwanafunzi atapata *guarantor*. Hali hii inamhusisha mwanafunzi na watu wengi mno wakati wa kuomba mkopo. Hawa wanafunzi tunaowazungumzia ni wale ambao kati yao wanafanya vizuri kwenye mitihani yao na wamepatiwa nafasi ya elimu ya juu kwenye vyuo lakini bahati mbaya hawana uwezo kifedha. Tunataka wafanye masomo yao kupitia Mfuko wa Mkopo huu.

Kwa hiyo, ningeomba kuwarahisishia njia ya kukamilisha maombi ya mkopo wao. Mimi naona tungefanikiwa kwa kumwacha mwanafunzi awe na mawasiliano na Bodi ya Mkopo tu. Baadaye afuatiliwe kwa kurejesha mkopo kwa kufungia cheti chake mpaka hapo atakapomaliza kurudisha mkopo.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukupongeza wewe, Naibu wako na watumishi wako kwa kuleta Muswada huu. Utawasaidia vijana wengi wenye uwezo wa akili wasio na fedha. Naomba Mheshimiwa Waziri afanye mambo yafuatayo:-

Kwanza, ili kukurahisishia kazi ya kutoa mikopo ya Watanzania kwa wasio Watanzania shirikianeni na Wizara ya Elimu na Utamaduni kuwatambua watoto raia wakianza *Form One* kama ilivyokuwa zamani. Hao wataendelea hadi Chuo Kikuu wakiwa raia.

Pili, watoto wanaotoka Vijiji vilivyo nyuma kiuchumi watakosa wadhamini kwa sababu wengi hawana uwezo.

Tatu, makato yaweze kumsaidia kuelimika na kumsaidia asiumie kulipa muda uwe zaidi ya mwaka mmoja ili mkopaji apate nafuu ya maisha kwani wengi hawapati kazi mara moja wakimaliza kwa sababu huo uwezo wa kulipa mara moja ni mfinyu.

Nne, nashauri mdhamini wa kijana iwe Halmashauri ya Wilaya kwani watajua wazazi na watamfuatilia kijana kwa urahisi zaidi kwa kutumia familia yake. Halmashauri ya Wilaya ziwe na watu maalum watakaowasiliana na *Board* kwa malipo.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki katika maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu ya sasa na hata baadaye kwa msingi huu naunga mkono Muswada huu moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mambo yafuatayo yaangaliwe:-

Moja, mwanafunzi asinyimwe mkopo kwa sababu ya umri wake bali kama anaweza kujidhamini apewe. Hii ni muhimu hasa pale wazee wanapohitaji kusomea elimu ya kompyuta na *information technology.* Ieleweke kuwa kutokana na janga la UKIMWI vijana ambao walikuwa wanategemewa wanaangamia sana na gonjwa hili kwa hiyo ni budi wazee nao wapate nafasi ya kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili halina budi kuepuka kupitisha sheria *(retrospectively)* kama Muswada huu unavyopendekeza. Nashauri watu waliokopa tarehe za nyuma walipe madeni yao kwa kuzingatia Mikataba waliyoingia wakati wanachukua mikopo husika. Ni vema Wizara ikaangalia kuwa na utaratibu wa kufuatilia madeni ya nyuma kama vile inavyofanyika katika ukusanyaji wa madeni ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ni muhimu kwa shughuli za elimu ya juu. Lakini sharti tukubali haitalipika. Ni dhahiri kwamba ulipaji wa mikopo hiyo itabaki kuwa nadharia. Tukubali kuwa Watanzania wanao utamaduni mdogo wa kulipa mikopo, kwa hiyo patahitajika elimu ya kujenga utamaduni miongoni mwa Watanzania, vinginevyo mikopo hii itaendelea kuwa matanga badala ya harusi kwa wataalam wetu watarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kuwataka Waheshimiwa Wabunge wote kuunga mkono hoja.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukiri kuridhika kwangu na ujio wa Muswada huu, japo umechelewa kidogo na ninaunga mkono moja kwa moja. Pamoja na hayo napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Kwanza, Bodi hii ijitangaze kwa urefu na mapana ili watu wengi kama inavyowezekana (wanafunzi na wafanyakazi) wauelewe ili wanufaike nao.

Pili, jitihada za makusudi zifanywe ili sehemu zote za Tanzania (Mikoa, Wilaya na kadhalika) watu wake wanufaike ama sivyo Mfuko huu utawanufaisha watu/wanafunzi wa Mijini tu.

Tatu, mikopo iwe yenye kukidhi mahitaji ya kusoma kwa ufanisi *(realistic).*

Nne, itungwe sheria ambapo waajiri wote waweze kuchangia angalau asilimia moja ya fedha zao za maendeleo, miradi katika Mfuko huu ili uweze kutuna kwa haraka na kuwanufaisha Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema tena naiunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Pius Ngw'andu pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Zabein Mhita, pamoja na Watendaji wa Wizara wote kwa jitihada zao katika kuleta Muswada huu ambao naamini utasaidia sana katika kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu vikiwemo vile vya sekta binafsi.

Aidha, ninaamini kuwa kurejeshwa kwa mikopo inayotolewa kwa wanafunzi kutatumika kama *Revolving Fund* ambayo itatumika kuhudumia wanafunzi wengi zaidi.

Mwisho, nashauri kuwa mtu yeyote anayetaka kujiendeleza apewe fursa ya kufanya hivyo bila kujali umri wake au kutumika kama kigezo cha kumzuia mwanafunzi mhusika kuchukua mkopo.

Kwa mara nyingine, narudia kuipongeza Wizara, ahsante.

**MHE. FATMA S. ALI (MCHUMO):** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Natoa pongezi za dhati kwa Waziri Ngw'andu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita na Katibu Mkuu kwa kuleta Muswada huu wakati hasa unaotakiwa.

Natoa pongezi kwa Serikali kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi ili waweze kupata Elimu ya Juu/Vyuo Vikuu ili twende sambamba na wakati. Lazima Tanzania tusomeshe wanafunzi wengi ili tuweze kukabili mabadiliko ya Sera za Elimu ya Dunia. Ombi langu ni kwamba Bodi ya Mfuko huo iwe na wajumbe wake sawa kwa sawa kijinsia yaani wanaume na wanawake sawa. Hii itasaidia wajumbe wa Bodi kuwafikiria zaidi wanafunzi wa kike kupata mikopo kwa wingi. Wanawake wasomi wanahitajika katika nchi yetu ili waweze kuwepo kwenye vyombo vya maamuzi.

Swali langu ni moja tu kwenye Muswada huu ni kuhusu wanafunzi waliopo Elimu ya Juu huko Zanzibar, idadi ya wanaofaulu ni kidogo. Tanzania Bara kuna mpango wa MMEM ambapo mpango huo unawaandaa wanafunzi kufaulu vizuri hadi wanapofika Vyuo Vikuu. Zanzibar hatuna mpango wa maandalizi hayo. Je, tutafikaje kwenye Vyuo

Vikuu kwa wingi kama wenzetu wa Tanzania Bara? Je, Mheshimiwa haoni kwamba Zanzibar tutafaidika kidogo sana na mikopo hiyo?

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nachangia moja kwa moja katika Ibara ya 16, kutokana na hali ngumu ya maisha na pia hata wamalizapo masomo hayo ni vigumu sana hata kupata kazi na pia hata wapatapo kazi mishahara ni midogo kwa hiyo basi kipengele hiki lazima tukiangalie kwa undani zaidi kwani kinaashiria moja kwa moja Serikali kujitoa kabisa katika kusaidia wanafunzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kutoa maoni katika Ibara 24 kuhusu ulipaji mikopo hiyo ndani ya miezi 12. Kulingana na mishahara na upatikanaji wa ajira, naona kiwango cha miezi 12 ni midogo sana na hata mwanafunzi huyo anapopata kazi hatamudu kulipa kwa muda huo. Kwa hiyo basi, naomba muda huo uongezwe ili wapate kujikimu hata kujijenga kwa muda huo kimaisha iwe hata miezi 30. Naomba kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe mchango wangu wa maandishi katika hoja ya Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kubuni mbinu ya kusaidia wale wanaotaka kupata Elimu ya Juu lakini hawana uwezo wa kuigharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hivi karibuni, mzigo wa gharama za Elimu ya Juu umekuwa unabebwa na Serikali kwa kiwango kikubwa. Jambo hili kwa kiwango kikubwa ilisababisha kasi ndogo ya ukuaji wa Elimu ya Juu. Serikali iliweza kuwalipia wale wachache tu waliobahatika kupata udhamini wa Serikali. Watanzania wengi sana ambao wamekuwa na sifa ya kusoma masomo ya Elimu ya Juu, wamekuwa wanashindwa kuendelea kwa kukosa udhamini. Muswada huu unajaribu kutatua tatizo hili kwa kuweka uwezekano wa yule ambaye angelishindwa kusoma kwa kukosa udhamini sasa asome.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa kuweko kwa uwezekano wa mikopo ya Elimu ya Juu kusiwe na matokeo ya Serikali kujivua kabisa kazi ya kudhamini wanafunzi wa Elimu ya Juu pale ambapo itaonekana inafaa. Ni jambo ambalo halina ubishi kuwa wengi wa Watanzania wanaishi katika lindi la umaskini mkubwa. Familia zenye shida ya kupata mahitaji yao ya kila siku zitaona elimu ya juu kama ndoto. Ukimwi nao umesababisha kuweko kwa idadi kubwa ya mayatima. Hawa nao wanayo haki ya msingi ya kupata elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Marmo, Mbunge wa Mbulu katika kikao cha tatu cha Mkutano huu wa Bunge lako alilieleza Bunge jinsi ambavyo baada ya zaidi ya miaka 40 ya uhuru, jamii ya Wahadzabe haina mmoja wao aliye na Digriii ya Chuo Kikuu. Ziko jamii nyingine za namna hiyo. Serikali lazima iwe katika mstari wa mbele na ielewe ni wajibu wake kuhakikisha kuwa wale ambao wanao uwezo wa kusoma elimu ya juu, lakini kwa sababu ya hali zao hawawezi kujigharamia, wanagharamiwa na umma bila uwezekano wa kuingizwa kwenye madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba kifungu cha 29 (1) kinaipa Bodi uwezo wa kumsamehe yeyote deni la Elimu ya Juu katika mazingira yaliyoainishwa katika ibara hiyo, ibara hiyo haitatui tatizo hili la umaskini. Msamaha huu unatolewa baada ya mwanafunzi kuingia deni na kumaliza masomo yake. Hii ina maana kuwa kwa yule atakayeshindwa kupata mdhamini wa deni lake au yule ambaye kwa umaskini wa familia yake anaona deni hilo litakuwa mzigo mkubwa kwa familia yake, hataweza kupata elimu ya juu kwa sababu ataogopa kuingia deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama hawa maskini wataweza kuchukua mikopo hiyo bila haja ya kuwa na wadhamini kutakuwa na matatizo ya urejeshwaji wa mkopo. Hawa wanakuwa na majukumu makubwa sana kifamilia baada ya kupata ajira. Hii inatokana na umaskini wa familia zao. Ikizingatiwa kuwa mishahara katika nchi yetu siyo mikubwa kuwabebesha watu hawa mzigo wa deni la Elimu ya Juu ni sawa na kuwahukumu katika maisha ya umaskini mkubwa. Kwa hiyo, ninaomba Serikali itoe tamko kwamba haijivui kabisa jukumu lake la kudhamini wale wanafunzi wanaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya kuchangia elimu ya juu ni sera iliyo sahihi kabisa. Wazazi wengi wamekuwa wanafanya hivyo, hasa katika nyanja za usafiri, malazi, chakula na matibabu. Kipato cha Mtanzania siyo kikubwa kwa walio wengi kiasi cha kuwawezesha kulipia gharama zote za Elimu ya Juu. Kifungu cha 16 (1) cha huu Muswada kinaongea juu ya mikopo kwa ajili ya w*elfare costs* za wanafunzi.

Kifungu cha 16 (2) (b), (c) na (d). Vifungu vyote hivyo vinahusu gharama vya elimu halisi kuhusu ufundishaji na hizi ndizo gharama kubwa katika Elimu ya Juu. Taifa linapata faida ya moja kwa moja kutokana na watalaam wanohitimu Elimu ya Juu. Kwa sasa waajiri wanalipa kodi ya elimu ya juu. Kifungu cha 25 cha Muswada huu hakisemi moja kwa moja kuwa hii *Higher Education Levy* itatumika moja kwa moja katika shughuli za *Board.* Ninashauri kuwa kwa kiasi kikubwa, Serikali ikubali kubeba mzigo wa *tuition fees,* vitabu na gharama za *field* na *practical training.* Itamkwe wazi kuwa vyuo vyote vya elimu ya juu, viwe vya umma au binafsi vipewe ruzuku ya Serikali kutoka kwenye makusanyo ya *Education Levy* kwa Uwiano wa wanafunzi wake. Hii ruzuku itumike kufidia gharama za *tuition* vitabu na *field* na *practical training.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika miaka ya 1967 mpaka miaka ya 1970 wanafunzi wa elimu ya juu hususan Vyuo Vikuu walikuwa wanapata mikopo ya kujikimu. Ni siri iliyo wazi kuwa mingi ya mikopo hii haijarejeshwa hadi sasa na kuna uwezekano hakuna kumbukumbu sahihi za wale ambao hawajarejesha mikopo hiyo. Ni

matumaini yangu kuwa mikopo itakayotolewa sasa itaendeshwa kwa njia ambayo itarejeshwa ili mpango huu uwe endelevu. La sivyo mpango mzima utakwama

Kwa hayo, niliyoandika, ninaomba nitamke kuwa ninaunga mkono hii hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. ISSA M. SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, natanguliza kutamka kwamba naunga mkono hoja ya Muswada huu wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ingawa unazungumzwa Bodi ya Mikopo ya Serikali. Niliona ingelikuwa vizuri zaidi ukachambua upya jinsi ya kupata mikopo hiyo na pia ikazingatiwa upya gharama za waombaji wa mikopo hiyo ambayo inaweza kutolewa kwa vijana ambao wazee wao ni maskini zaidi na wako mbali sana na Bodi hiyo.

Nakubaliana na muundo wa Bodi kama ulivyoeleza kisheria kwa maana kwamba Elimu hii ya Juu ni haki ya kila Mtanzania. Pamoja na kukubali huko kwa hatua ambayo Tanzania sasa imefikia. Sikubali kwamba sheria hii inatumika pia Zanzibar kwa sababu Elimu ya Juu ni suala la Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua tuliyofikia sasa kuna taasisi mbalimbali nchini ambazo zinamiliki vyuo vikuu. Tunakoendelea hata mtu binafsi kama atatimiza masharti yanayotakiwa anaweza kumiliki Chuo Kikuu. Kwa maana hiyo sioni mantiki ya Katiba yetu kuendelea kutamka kwamba Elimu ya Juu ni suala la muungano.

Ni vyombo kama vile tu ambavyo vinaratibu ubora wa elimu inayotolewa Tanzania vinaweza vikafikiriwa kuwa ni vya Muungano.

Kuna haja kwa Wizara hii husika, kuliona hilo na hasa ilivyokuwa ni Wizara ya kitaaluma mambo kama haya kubakia mikononi mwao tena kikatiba haliingii akilini. Suala la Muungano haliweza kumilikiwa na taasisi moja au mtu binafsi mfano Polisi, Jeshi, Mambo ya Nje na kadhalika.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaunga mkono hoja hii na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kuleta Muswada huu Bungeni, ili kuwasaidia vijana wanaosoma. Pamoja na hivyo ninaomba yafuatayo yaangaliwe:-

Kwanza, Sheria 10 inasema *Executive Director* wa *Board* atateuliwa na Waziri na hivyo maslahi yake yataainishwa ndani ya barua ya uteuzi toka kwa Waziri na siyo toka kwa *Board* kama Sheria 10 (2) inavyosema.

Pili, Sheria namba 11 (2) inasema huyu *Executive Officer* atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka minne (4). Ningependekeza kipindi kisiwe cha miaka fulani kwani anaweza kufanya kazi vizuri na hivyo akatumikia kwa miaka mingi zaidi ya hiyo minne

au minane au akafanya vibaya kiasi kwamba ikabidi waachishwe hata baada ya kufanya kazi mwaka mmoja au hata chini ya hapo.

Tatu, Sheria ya 11 (3) inasema *Board* inaweza kumwachisha kazi huyu *Executive Director* lakini siyo sawa kwani anayeweza kumwachisha ni yule aliyemwajiri yaani *appointing authority* ambaye ni Waziri na siyo *Board. Board* inaweza tu kupendekeza kwa Waziri kumfukuza kazi.

Nne, Sheria ya 11 (4) kwa kuzingatia hayo niliyosema hapo juu kifungu hiki nacho lazima kibadilishwe ili *Executive Director* akate rufaa kwenye chombo kingine zaidi ya Waziri endapo atakuwa hakuridhika kutokana na uamuzi wa Waziri.

Tano, Sheria ya 2 ni vyema kifungu hiki kisomeke kwamba *this Act shall apply to the United Republic of Tanzania.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Muswada ulio mbele yetu. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza katika Mkutano huu kupata fursa hii, ninapenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kumpongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na mwalimu wangu katika Taaluma ya Uongozi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mawaziri wote wa Elimu wa Nchi za Afrika na Mheshimiwa Arado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Wamepewa dhamana hizo kwa kutambua uwezo wao mkubwa sana katika masuala ya uongozi. Na hiyo ni heshima kubwa kwa Bunge hili na kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Dodoma hususan wanawake wa Wilaya ya Kondoa, Dodoma Mjini, Dodoma Vijijini, Kongwa na Mpwapwa ninayo heshima kuwasilisha kupitia Bunge lako Tukufu pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, ambaye kwa mara nyingine tena ameipandisha bendera ya Tanzania katika ramani ya ulimwengu kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Bunge la Kwanza la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba uniruhusu nipitie baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili Muswada huu. Kulikuwa na hoja kuwa Serikali kuwekeza kwenye elimu. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Remidius Kissassi na Mheshimiwa John Singo. Waheshimiwa Wabunge wameishauri Serikali kuwekeza kwenye elimu kwa kiwango kinachostahili. Baadhi ya njia zinazoweza kutumiwa kuwekeza ni pamoja na kutumia asilimia fulani ya mapato ya *TRA* na kuwekezwa kwenye elimu. Sheria ya Mfuko wa Elimu namba 8 ya mwaka 2001 inaelekeza Serikali itenga asilimia 2 ya mapato yake kwa ajili ya kuendeleza elimu. Hii ni takriban shilingi bilioni 37 ya bajeti

ya Taifa. Serikali mpaka hivi sasa inatenga kiasi pungufu ya hicho kiwango kutokana na ufinyu wa bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya *scholarship* kwa wanafunzi wanaofaulu vizuri. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa na maoni kwamba Serikali inawajibika kutoa *scholarship* kwa wanafunzi wanaofanya vizuri ambao watakuwa ni hazina ya wataalam kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Hoja hii iliungwa na Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa na Mheshimiwa Jackson Makwetta.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na hoja hii, lakini itashughulikiwa kwa utaratibu mwingine. Hii ni kwa sababu sera inaelekeza *scholarship* za Serikali zitolewe kwa wanafunzi wachache waliofaulu vizuri sana na ambao watasoma masomo yenye umuhimu maalumu kwa Taifa letu. Kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya gharama za kumuelimisha mwanafunzi wa Chuo Kikuu. Kulikuwa na hoja ya kutaka kupata gharama halisi za kumwelimisha mwanafunzi katika Chuo Kikuu. Mheshimiwa Leonard Derefa na Mheshimiwa Janet Kahama walitoa hoja hiyo. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba gharama za kumwelimisha mwanafunzi katika Chuo Kikuu zinaweza kufahamika kwa kutumia njia kadhaa za ukokotaji. Njia hizo ni *full costing, valuable costing, increment costing*. Kwa kutumia njia ya *full costing,* gharama hizo ni kama ifuatavyo:- *University of Dar es Salaam 2,900,181/= University College of Land and Archi-tectural Studies 1,580, 433/=. St. Augustine University of Tanzania 773,736/=, Tumaini University 1,117,458/=, Muhimbili University College of Health Sciences 3,384,495/=, Kilimanjaro Christian Medical College 1,349,053/=, Herbert Karuki Memorial University 1,485,548/=, International Medical and Technological University 787,114/=, Sokoine University of Agricultural 2,911,013/=, Open University of Tanzania 976,902/=, Dar es Saalam Institute of Technology 1,185,928/=.*

Mheshimiwa Spika, hoja ya ada zitakazotozwa na Bodi. Kulikuwa na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Ismail Iwvatta aliyetaka kujua ada zitakazotozwa na bodi. Kwa mujibu wa Ibara ya 7(1)(a) ya Muswada ada zitakazotozwa na bodi ni pamoja na ada ya maombi, ushauri wa kitaalam na adhabu kwa kutotimiza masharti ya mkopo. Ili bodi iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi, itawajibika kufanya kazi kwa karibu wanafunzi, waajiri na uongozi wa vyuo kwa njia ya ushauri ili kuhakikisha kwamba wote wanakuwa na ufanisi katika utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia kuna hoja ya kutumia cheti kama dhamana. Pendekezo hili lilitolewa na Mheshimiwa Ismail Iwvatta ni wazo nzuri, lakini lina utata kwa vile linabadilisha maana ya kawaida ya dhamana. Wakati wa kuwekeana mkataba cheti kitakuwa bado hakijapatikana. Je, endapo mdaiwa hatafaulu katika masomo yake na hivyo hatapata cheti itakuwaje? Tunapendekeza kuwahusisha waombaji wote na bima ya maisha kama aina moja tu ya dhamana.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na hoja kwamba idadi ya wajumbe wa bodi na jinsia. Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Janet Kahama na Mheshimiwa Fatuma Said Ali (Mchumo). Tunakubaliana na mapendekezo ya kutaka idadi ya wajumbe wa bodi iwe 14. Suala la jinsia limezingatiwa sana katika Ibara ya 5(2) ya Muswada ambapo Mheshimiwa Waziri anayehusika atahakikisha kwamba theluthi moja ya wajumbe wa bodi ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kufuatilia wakopaji. Waheshimiwa Wabunge walitaka kuwepo na utaratibu mzuri wa kufuatilia urejeshwaji wa mikopo ili wanafunzi wengi zaidi wanufaike. Ufuatiliaji wa wakopaji kunamaanisha pia kutambua uraia wao kabla hawajakopa. Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Rhoda Kahatano na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. Vyombo vya Taasisi mbalimbali kama vile Bodi za Leseni, Uhamiaji, Waajiri na Vyuo na kadhalika vitahusishwa. Aidha, kila mkopaji atakuwa na namba ya utambulisho.

Mheshimiwa Spika, rai hizo zitazingatiwa, wakati wa kutunga kanuni za utekelezaji wa sheria hii utaratibu wa kurejesha mikopo utawekwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia kuna hoja ya elimu kwa umma. Suala la kuelimisha wakopaji, waajiri, wadhamini na wananchi kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa za mabadiliko ya anwani za wakopaji kama sheria ilivyoelekeza na kurejeshwa kwa mikopo limepata msisitizo maalum. Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Profesa David Mwkyusa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali na Mheshimiwa Remidius Kissassi. Umuhimu wa elimu kwa umma ni suala lisilohitaji mjadala. *(Makofi)*

Vilevile kulikuwa na hoja ya kwamba sababu za kusamehewa mikopo. Kulikuwa na hoja ya kuongeza kipengele katika Ibara 29(1) ili kufanya kukosa ajira kuwa ni moja ya sababu ya kusamehewa mikopo. Ajira siyo kigezo pekee cha mtu kupata elimu, na hivyo kukosa ajira haiwezi kuwa sababu ya kusamehewa mkopo.

Vilevile kulikuwa na hoja ya kupanua Elimu ya Juu. Kulikuwa na hoja ya kupanua Elimu ya Juu kwa kupendekeza Vyuo vya Ualimu vya Dar es Saalam, Kleruu, Marangu, Butimba na Chuo cha *IFM* vigeuzwe kuwa Vyuo Vikuu. Hoja hii iliwasilishwa na Mheshimiwa Khalid Suru.

Mheshimiwa Spika, kupanua Elimu ya Juu ni jambo njema sana, namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Khalid Suru kwa kuliona hili. Hoja hii inashughulikiwa na Mradi wa Uhuishaji Taasisi za Elimu ya Juu ambao kwa hivi sasa umekamilika katika hatua ya awali kwa Vyuo vya Ufundi Stadi. Hatua inayoendelea sasa hivi ni Vyuo vya Elimu ya Juu. Serikali tayari imekwishaidhinisha maombi ya *IFM* na Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki pindi hali ya fedha itakaporuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vigezo vya kupata mkopo. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliona kwamba udahili katika Chuo Kikuu uchukuliwe kama sifa pekee ya

kumfanya aliyepata udahili huo apewe mkopo. Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman na Mheshimiwa Jackson Makwetta walikuwa na mtazamo huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kimsingi inakubaliana na wazo la kupanua wigo wa vigezo vya kumpa mkopo. Lakini vigezo hivyo ni lazima vizingatie uwezo wa kiuchumi wa mwombaji pamoja na masharti mengine kama yalivyoorodheshwa katika Ibara ya 17 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walitoa ushauri kwamba Mkurugenzi Mtendaji ambaye huteuliwa na Mheshimiwa Waziri kama Muswada unavyosema hastahili kuwajibishwa na Bodi kama Ibara 11(3) kinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na ushauri huo kama ulivyotolewa na Mheshimiwa Frank Mussati na Ibara hiyo imefanyiwa marekebisho na kufanya Bodi itoe mapendekezo kwa Mheshimiwa Waziri ili achukue hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, urejeshwaji wa mikopo uzingatie uwezo wa mkopaji. Hoja hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Rhoda Kahatano. Ibara ya 19(3) cha Muswada inampa fursa mkopaji kufanya makubaliano na mkopeshaji yaani Bodi juu ya taratibu za ulipaji wa deni kwa kuzingatia uwezo wa mkopaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu dhamana. Kulikuwa na hoja iliyotolewa na Rhoda Kahatano kwamba Halmashauri za Wilaya ziruhusiwe kudhamini wakopaji kwa vile Halmashauri hizo ziko karibu sana na waombaji. Hoja hii imekubalika kama ilivyoelezwa katika maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika hoja nitakazochangia ni muda wa kuanza kulipa mkopo. Imetolewa hoja na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, kwamba muda wa miezi 12 baada ya kuhitimu kabla ya kuanza kulipa mkopo ni mfupi mno. Mtoa hoja alipendekeza kwamba muda huo uwe miezi 30.

Mheshimiwa Serikali ninaamini kwamba muda wa miezi 12 ni kipindi muafaka kwa mkopaji kujiandaa kulipa deni lake. Hata hivyo, Muswada unampa fursa mkopaji wenye matatizo katika ulipaji kuwasiliana na Bodi kwa nia ya kupanga taratibu za ulipaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba kuunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu tena kusimama hapa kutetea hoja yetu ambayo tumeileta mbele ya Bunge. Natoa shukrani zingine kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika Muswada huu kwa kuzungumza na kwa maandishi.

Napenda pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao walipata fursa ya kunipongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mkutano wa Mawaziri wa Elimu Afrika siyo Elimu ya Juu, Elimu yote.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja ya Bunge kwa niaba ya Wizara yangu kumpa pole Mheshimiwa Rais wetu Benjamin William Mkapa, pamoja na familia yake kwa mkasa na ajali hii iliyotusibu.

Aidha, napenda kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango walioitoa sasa hivi katika mazungumza ya leo. Namshukuru pia kwa hali ya pekee Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Zabein Mhita kwa mchango wake katika kujibu hoja. Nachukua nafasi hii kumshukuru Katibu Mkuu wangu pamoja na Wakurugenzi wake na wataalam wote hasa kutoka kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuboresha Muswada wetu.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwa mchango wao ambao tumeuzingatia kama inavyoonyeshwa kwenye majedwali ya marekebisho ambayo tumeyatoa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wafuatao kwa mchango wao kwa mazungumzo. Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa John Singo, na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. *(Makofi)*

Aidha, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wafuatao kwa mchango wao kwa maandishi. Mheshimiwa Fatma Said Ali (Mchumo), Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Frank Michael Mussati, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi.

Mheshimiwa Spika, nitazingatia hasa maoni ya Kamati na maoni ya upande wa Upinzani katika majibu yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Huduma za Jamii kwa mchango wake wa tarehe 5 -6 Aprili, 2004. Wajumbe wa Kamati walitoa mchango mkubwa sana ambao umezingatiwa katika hati ya marekebisho ya Muswada huu. Aidha, tunaishukuru Kamati kwa mchango wake wakati wa kuuwasilisha Muswada huu ndani ya Bunge. Baadhi ya maeneo yaliyohitaji marekebisho kwa mujibu wa Kamati hii ni jina la sheria limerekebishwa, wajumbe wa Bodi tumerekebisha, kazi za Bodi nazo zimerekebishwa, masharti ya dhamana nayo yamefanyiwa marekebisho, kiwango cha juu

cha umri wa mkopaji ambacho nacho kimerekebishwa kwa kufutwa kabisa. Vipengele hivi vimezingatiwa katika hati ya marekebisho ya Muswada kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja zingine za Kamati zilihusu urejeshwaji wa mikopo ya awali kuanzia mwaka 1994. Serikali inakubaliana na hoja ya Kamati kwamba masharti ya ukopaji kwa mujibu wa sheria hii yahusuyo wahitimu waliokopa toka 1994 na badala yake mikopo ya wakati huo irejeshwe kwa mujibu wa masharti ya ukopaji ya wakati huo.

Sheria hii inatoa jukumu la mikopo hiyo kukusanywa kwa mujibu wa makubaliano ya wakati ule. Aidha, sheria ya *The Government Proceeding Act (GPA)* ya mwaka 1967 inaweza kutumika katika kukusanya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, masharti na dhamana ya mikopo. Serikali inakubaliana na hoja ya Kamati pamoja na hoja za Waheshimiwa Wabunge kupanua wigo wa dhamana ili wahitaji wengi zaidi waweze kunufaika na mikopo inayokusudiwa.

Lengo hasa ni kuwalenga wale maskini ambao hawana uwezo. Serikali itatazama uwezekano wa kuweka utaratibu ambao utazingatiwa katika ngazi ya Kata, Kijiji, Mashirika ya dini, Vyama vya Hiari na Halmashauri za Wilaya ili waombaji wa mikopo waweze kudhaminiwa na Vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Elimu kwa Umma. Katika majibu yake wakati Naibu Waziri akizungumza alieleza kwamba kwa vile huu ni utaratibu mpya wa kugharamia elimu, suala la Elimu kwa Umma ni suala la msingi na litazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, maoni kutoka kwenye Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Benedict Mutungirehi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, aliwasilisha hoja zifuatazo. Tafsiri ya neno *student* au mwanafunzi kwa kuwa tafsiri iliyotolewa kwenye Muswada inalenga kuongeza idadi ya wahitimu wa Shahada ya Kwanza au *Diploma* ya Juu.

Serikali na waajiri mbalimbali watakuwa na utaratibu mwingine wa kuendeleza taaluma za wafanyakazi wao yaani watakuwa na *Staff Development Programme* kutoka kwenye ofisi zao, Serikali kupitia Mpango kabambe wa Elimu ya Juu ambao unaanza mwaka 2003-2018 inaandaa utaratibu wa *Scholarships* au *fellowships* kwa ajili ya kuwafundisha Walimu wa Vyuo Vikuu, Utafiti, Sayansi na *Management.* Kwa hiyo, pengo hilo *MSc.* na *Ph.D, Post Graduate Courses* litakuwa limezibwa kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wajumbe wa bodi kwamba wasipungue 12 na wasizidi 14. Hoja hii kimsingi tunaikubali, wajumbe wa bodi watakuwa 14, na suala la jinsia litazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa malipo ya ziada kwa wanafunzi wanaosoma nje. Pamoja na kwamba hoja ya malipo ya ziada kwa wanafunzi wanaosoma nje kutoeleweka vyema.

Napenda kutoa ufafanuzi kuwa kuna makundi mawili ya wanafunzi wanaosoma nje hivi sasa. Kundi la kwanza wanafunzi wanaojilipa wenyewe hawa hawagharamiwi chochote na Serikali yetu. Kundi la pili, wanafunzi wanaokwenda kusoma nje kwa *scholarship* za nchi marafiki. Hawa kulingana na ugumu wa maisha katika nchi wanazokwenda Serikali huwasaidia malipo ya nyongeza kwa mkopo yaani *Topping Up Allowance* ili Kukabiliana na matatizo ya maisha huko waliko. Nchi zenye wanafunzi wanaopata *Topping Up Allowance* ni Urusi, Poland na Algeria. Mkopo kwa wanafunzi wanaorudia mtihani mwaka wa masomo Serikali inakubaliana na hoja hii na tayari imewekwa katika hati ya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nachukua baadhi ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwanza kwa kusema kwamba maoni yote tumeyachukua, tunayafanyia kazi na tutazidi kuyafanyia kazi. Mengine yatadhihirika katika mamlaka mliyonipatia ya kutunga kanuni. kwa hiyo, yatatekelezwa katika wakati muafaka utakapofika.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuzipitia hoja na maoni ya Waheshimiwa Wabunge kama yalivyowasilishwa kwa mdomo na kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge niliowataja hapo awali. Hoja hizo ziko kwenye maeneo makuu 21. Baadhi ya maoni mengi ameshayapitia Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo mimi nitachagua baadhi ya yale yaliyobakia. Kulikuwa na hoja ya kuondoa mianya ya rushwa na upendeleo katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walionyesha wasi wasi kwamba baadhi ya vipengele katika Muswada vinatoa mianya ya rushwa na upendeleo. Walionyesha wasi wasi huo ni pamoja na Mhe. Prof. Mwakyusa, Mheshimiwa Uledi, Mheshimiwa Dr. Kamala na Mheshimiwa Iwvatta. Mimi ninaafiki nadhani kwamba sheria nzuri ni ile iliyopunguza *discretional power* ya mtawala au mtoa maamuzi ili kuziba mianya ya rushwa na upendeleo. Kwa mantiki hiyo basi ibara ya 9(1) na 18 (2) zimerekebishwa. Wakati ibara ya 29(1)(b) imefutwa kwa mujibu wa jedwali la marekebisho.

Aidha, ibara ya 17(d) ambayo kwa maoni ya Mheshimiwa Dr. Kamala inatoa mwanya wa upendeleo wa rushwa. Inapendekezwa ibara kama ilivyo. Sababu za msingi za kutokubadilisha ibara hii ni umuhimu kuzingatia uwezo wa kiuchumi kwa wakopaji na pia kuyalenga makundi yenye mahitaji maalum na wale maskini ili wale ambao wanaweza kulipia waweze kulipia. Walengwe wale ambao hawana uwezo wa kulipia. Nimesema yalengwe makundi maalum katika jamii ambayo inaitwa *disadvantage groups.* Tathmini ya awamu ya kwanza na ya pili ya uchangiaji gharama na kuanza kwa awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala aliunga mkono hoja kwa masharti kwamba ajulishwe kama tathmini ya uchangiaji, gharama ya awamu ya kwanza na ya pili imefanyika. Aidha, alitaka kujua kama awamu ya tatu ya uchangiaji imeanza. Nafurahi kumwarifu Mheshimiwa Kamala na Waheshimiwa Wabunge kwamba tathmini ya uchangiaji gharama za elimu ya juu awamu ya kwanza na ya pili imekwishafanyika na

taarifa ninayo hapa Bungeni na wadau walishiriki kutoa maoni yao katika warsha iliyofanyika huko Morogoro mwezi Agosti mwaka 2002.

Mapendekezo ya wadau sio mapendekezo ya ripoti, maana ripoti ilipotoka wadau walikaa wakapendekeza yafuatayo. Yalikuwa ni kwamba kwa vile idadi ya taasisi binafsi za elimu ya juu imeongezeka na wanafunzi wenye sifa za kujiunga na taasisi za elimu ya juu nao wanaongezeka mwaka hadi mwaka. Awamu ya tatu ya uchangiaji elimu ya juu ilionekana imechelewa kutekelezwa. Wadau pia walitambua gharama kubwa zitakazojitokeza katika kugharamia awamu ya tatu na hivyo wakaishauri Serikali ianzishe chombo cha mikopo kitakachowasaidia wanafunzi kuzikabili gharama hizo.

Aidha, wadau waliishauri Serikali ianzishe taratibu zitazokiwezesha chombo cha mikopo ya elimu ya juu kiweze kumtambua muhitaji wa mikopo kutokana na uwezo wake mdogo kiuchumi. Wadau walioshiriki kwenye warsha hiyo waliona kwamba mikopo iliyotolewa tangu mwaka 1994 haijarejeshwa kwa sababu hakukuwa na chombo chenye uwezo wa kisheria kusimamia urejeshwaji wa mikopo hiyo ambayo marejesho yake yangeweza kusaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu kuufanya utaratibu huo uwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Bodi hii ya mikopo kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu ni kutekeleza maelekezo ya sera, matokeo ya tathmini ya awamu ya kwanza na ya pili ya uchangiaji wa elimu ya juu na kuongezeka kwa gharama za elimu ya juu ukilinganisha uwezo wa Serikali katika kugharamia elimu hiyo. Hoja ya msingi hapa ni kuwawezesha wanafunzi wengi zaidi kupata elimu ya juu kwa kuzingatia uhakika wa urejeshwaji wa mikopo. Kwa hiyo, tunaweza kusema awamu ya tatu ya uchangiaji imeanza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali kwa hali hii inajitoa katika kugharamia elimu ya juu. Majibu yake ni kwamba laa hasha! Huu wasi wasi kwamba Serikali inajitoa katika kugharamia elimu ya juu nawaomba kabisa Waheshimiwa Wabunge wauondoe kabisa. Hoja hii iliwasilishwa na Mheshimiwa Dr. Kamala, Dr. Lamwai na Mheshimiwa Derefa. Napenda kuwahakikishia Wabunge kwamba Serikali itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kugharamia elimu ya juu.

Serikali bado itaendelea kutenga fedha katika Bajeti kwa ajili ya kuendesha elimu ya juu, kumiliki taasisi zake za elimu ya juu, kugharimia mafunzo ya wafanyakazi katika taasisi zake, kutoa *seedmoney* kwa Bodi ya mikopo inayopendekezwa kuunda na mikopo hiyo itakuwa haina riba. Narudia mikopo hiyo haina riba, na kutoa fedha kwa ajili ya mfumo wa elimu ambao unasaidia maendeleo ya taasisi za elimu ya juu na za umma na za binafsi. Bado Serikali itaendelea kulipia wanafunzi ambao wana ushindi wa juu sana hawa Serikali itakuwa bado inawalipia. *(Makofi)*

Kutokuwepo kwa riba kwa mikopo hii kumetokana na Serikali kutambua kwamba ina mchango wake na wajibu wake katika kuendeleza elimu ya juu. Bila riba Bodi ya Mikopo ni wazi haitakuwa na uwezo wa kujiendeleza. Kwa hiyo, Serikali itatoa ruzuku

kwa Bodi ili iweze kuendesha shughuli zake bila kusambaza gharama hizo za utawala kwa mkopaji, huo ndio mchango wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mikopo toka mwaka 1994. Kama nilivyoeleza hapo awali tumepokea hoja ya Mheshimiwa Ireneus Ngwatura ambayo ameishauri Serikali kwamba mikopo ya wanafunzi kuanzia mwaka 1994 mpaka sheria mpya itakapoanza irejeshwe kwa utaratibu tofauti na ule unaopendekezwa katika Muswada huu. Suala hili tumeshalirekebisha. *(Makofi)*

Elimu ya Juu kuwa ni suala la Muungano. Tumepokea maoni ya Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman ambayo haoni mantiki ya elimu ya juu kuendelea kuwa ni suala la Muungano wakati ambapo mazingira ya sasa yamebadilika na namruhusu hata mtu binafsi mwenye uwezo kumiliki taasisi ya elimu ya juu. Suala la elimu ya juu ni suala la Katiba. Kama hoja aliyoitoa Mheshimiwa Suleiman ndiyo hiyo tu basi haibadilishi umuhimu wa elimu ya juu kuwa katika Muungano. Maslahi ya Muungano yanalindwa na Baraza la Ithibati ya Elimu ya Juu *(Higher Education Accreditation Council)* katika kulinda sera ya ubora wa elimu ya juu katika taasisi yoyote ya elimu ya juu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, sera ya elimu ya juu inatoa fursa kwa watu binafsi, jumuiya za kijamiij za kidini, vyama vya hiari na kadhalika kuanzisha taasisi ya elimu ya juu kulingana na maelekezo na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza kulikuwa na hoja za Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya ambazo alizungumzia tufikirie jinsi ya kuwasaidia wanafunzi usafiri kwenye mkopo. Kisera gharama za usafiri zimekuwa zikilipwa na wanafunzi tangu katika awamu ya kwanza ya uchangiaji na zitaendelea kuwa hivyo kwa sasa hivi. Kuhusu umri wa mkopaji tumesema kuwa hilo tumeshalibadilisha. Vile vile kulikuwa na hoja kwamba Serikali itenge fedha kwa ajili ya Bodi ya Mikopo. Serikali itaendelea kufanya *Capitalisation of Loan Board* mpaka pale ambapo Bodi yenyewe itafikia hatua ya endelevu.

Hoja za Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi alikuwa amezungumzia kifungu cha 6(b) kipewe nguvu zaidi. Tunamhakikishia Mheshimiwa Kazi kwamba kifungu hiki kinachohusu jinsi ya kuwatambua wenye kuhitaji mkopo kinajitosheleza na kwamba kina nguvu ya kutosha. Kifungu cha 5 (1)(c) kirekebishwe kwa kumwondolea Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi katika Bodi. Serikali inaona kuna umuhimu Mjumbe huyu akabaki kwenye Bodi kwa sababu anawakilisha vyuo vingine vya Ufundi ambavyo viko nje ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya haya ninayo heshima kutambua kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge imetusaidia sana na napenda kutoa shukrani kwako na Bunge lako Tukufu kwa kutuwezesha kuboresha hoja yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu wa Mwaka 2004 *(The Government Student's Loans Board Bill, 2004)***

**SPIKA:** Jina refu lina marekebisho.

*(Jina lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko yake)*

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko yake)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko yake)*

Ibara Mpya 19(a)

*(Ibara mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilitotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko Yake)*

Ibara ya 27
Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko Yake)*

Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake*

Jedwali la ukurasa 46

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa Wanafunzi na Vyuo Vya Elimu ya Juu wa Mwaka 2004 *(The Government Student's Loans Board Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima limepitia Muswada kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali. Naomba Bunge likubali kupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Hatua za kupitisha Muswada huo katika ngazi ya Bunge zimekamilika. Sasa utakwenda kwa Mheshimiwa Rais kupata kibali. Nilipanga kwamba tukishamaliza shughuli za Muswada huu tusitishe Shughuli za Bunge ili kusudi Waziri anayefuata atoe hoja yake saa 11.00 Jioni. Hakuna aliyepinga mawazo yangu haya kwa hiyo sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.16 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**Muswada wa Sheria ya Kurejesheana Wafungwa ya Mwaka 2004**
***(The Transfer of Prisoners Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kurejesheana Wafungwa ya 2004 *(Transfer of Prisoners Bill, 2004)* pamoja na marekebisho yake usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli yake ya leo asubuhi na Bunge kwa jumla, kwa Azimio lake la kumpa pole Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na familia yake, kwa taathira kubwa waliyopata kutokana na moto uliounguza makao yake rasmi hapo Ikulu.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu, uchunguzi unaendelea na tuwape nafasi wanaofanya waukamilishe ili tujue chanzo chake na hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe na Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika.

Pongezi zangu pia zimwendee Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshughulikia mazingira, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Uongozi la Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira *(UNEC)*.

Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mkutano wa Mawaziri wa Elimu wa Bara la Afrika. Kuchaguliwa kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu hao katika nyadhifa hizo za uongozi wa Kimataifa kumeinua heshima na hadhi ya Bunge letu na Taifa la Tanzania kwa jumla katika medani ya Kimataifa, hatuna budi kuwa na fahari nao. Nawaombea kila la kheri na mafanikio katika majukumu yanayoambatana na nyadhifa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulio mbele ya Bunge lako Tukufu hivi sasa ni wa sheria ambayo kama itatungwa itaiwezesha Tanzania kurejeshewa wafungwa na nchi za nje itakazoingia nazo mikataba kwa ajili hiyo. Sheria hiyo inakusudiwa kuwafaidisha raia wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakaopenda kufaidika nayo.

Hata hivyo, kwa kuzingatia kwamba suala la hifadhi ya wahalifu si la Muungano, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi atawajibika kuwasiliana kwanza na Waziri anayehusika na hifadhi ya wahalifu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kabla ya kufanya uamuzi wowote kuhusu ombi la Mtanzania Mzanzibari anayetumikia adhabu ya kifungo nje ya Tanzania ambaye anataka aje amalizie adhabu yake Tanzania. Waziri atafanya maamuzi kwa mujibu tu wa makubaliano na mwenzake wa Zanzibar. Utaratibu huo wa mawasiliano utahusu pia wahalifu raia wa nchi za nje wanaotumikia adhabu zao Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kurejesheana wafungwa waliokwisha kuhukumiwa kifungo baina ya nchi na nchi ni miongoni mwa fikra zilizoibuka katika miongo ya hivi karibuni. Nchi mbalimbali duniani zimejiwekea utaratibu wa kurejesheana wafungwa kwa kuwa na sheria pamoja na mikataba inayoeleza ni namna gani hukumu zilizotolewa katika nchi moja zinaweza kutekelezwa katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inaonyesha kwamba, utaratibu wa kuwa na mikataba ya kubadilishana wafungwa ulianza kutumika katika nchi za Ulaya Magharibi katika miaka ya 1960. Nchi za Scandinavia yaani Denmark, Finland, Iceland, Norway na Sweden mnamo mwaka 1963 ziliingia mkataba wa kubadilishana wafungwa ujulikanao kama *The Scandinavian Treaty of 1963.* Mikataba mingine iliyofuata ni ile iliyofanyika kati ya Denmark na Spain mwaka 1972, Ujerumani na Romania mwaka 1982 na kati ya Austria na Yugoslavia mwaka 1982. Mikataba hiyo iliendelezwa vile vile kati ya nchi za Ulaya Magharibi na nchi nyingine kwa mfano mkataba kati ya Uturuki na Marekani wa mwaka 1979, Ufaransa na Canada wa mwaka 1979 na ule wa Ufaransa na Morocco wa mwaka 1982. Jitihada hizo ziliendelezwa vile vile katika nchi za Jumuiya ya Madola ambazo ziliweka utaratibu wa kurejesheana wafungwa kwa kuzitaka nchi wanachama kuwa na sheria na mikataba ya kurejesheana wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Mataifa kwa kutambua juhudi hizo mnamo mwaka 1985 ulitoa tolea maalum linalohusu utaratibu wa kurejesheana wafungwa. Toleo hilo linajulikana kama *The Model Agreement of the Transfer of Foreign Prisoners of 1985.* Kuanzia hapo nchi mbalimbali duniani zilianza kutunga sheria na kuwekeana mikataba ya kurejesheana wafungwa. Barani Afrika jitihada hizo ziliendelezwa katika mikutano ya viongozi mbalimbali kwa kuzitaka nchi wanachama kuona uwezekano wa kutungwa kwa sheria za kurejesheana wafungwa katika nchi zao. Wakuu wa Magereza wa Nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika kupitia umoja wao ujulikanao kama *The Conference of the Eastern, Southern and Central African Headlock Collection of Services (CESCA)* ambao unazijumuisha nchi za Botswana, Burundi, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Zimbabwe, Rwanda, Seychelles, Afrika Kusini, Swaziland, Tanzania, Uganda, Zambia na Angola wamelitafakari suala hili.

Kwa wale wanachama wa *CESCA* ambao pia nchi zao ni wanachama wa *SADC* tayari wamekwishaandaa rasimu ya mfano wa utaratibu wa kubadilishana wafungwa ujulikanao kama *Bilateral Model Agreement between SADC Member States on the Transfer of Sentence Offenders.* Ili taratibu hizi za kubadilishana wafungwa ziweze kufanyika ni lazima kuwepo sheria za nchi na mikataba baina ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kurejesheana wafungwa kati ya nchi na nchi unatokana na hoja mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

(i) Nia hasa ya kumrekebisha mfungwa ni kumuandaa ili aweze kurudi katika jamii yake aliyoizoea na kwenda kuishi nayo. Mfungwa aliyehukumiwa kifungo ugenini na kuendelea kutumikia kifungu huko huko siyo rahisi kuweza kupewa programu ya urekebishaji ambayo itamfanya aweze kwenda kuitumia vyema katika nchi yake. Hivyo urekebishaji utafanikiwa zaidi iwapo utafanyika kwenye nchi yake kwani atakuwa karibu na ndugu zake ambapo mara amalizapo kifungo chake atakuwa amejiandaa vya kutosha zaidi kujiunga nao.

(ii) Maazimio mbalimbali ya Kimataifa yanazitaka Serikali ziheshimu utu wa wafungwa kwa kuwatendea haki bila ya kujali utaifa, rangi au dini zao. Wafungwa wanazo haki nyingi zikiwa ni pamoja na haki ya kutembelewa na ndugu, kupewa huduma, chakula, mavazi, kuishi katika mazingira mazuri na kadhalika. Katika baadhi ya Magereza wafungwa ambao si raia wa nchi waliyomo wanapatwa na matatizo kadhaa kwa mfano tatizo la lugha, aina ya chakula wapewacho wafungwa, kubaguliwa na wenzao, kutokuwa na mawasiliano na ndugu zao na kadhalika. Ili kujenga mazingira mazuri zaidi ya kuwapatia haki hizo za msingi ambazo zimekubalika Kimataifa jambo la kuwahamishia kwenye nchi zao linajitokeza na umuhimu mkubwa.

(iii) Iwapo wafungwa wengi wageni waliomo katika Magereza yetu watahamishwa na kurejeshwa makwao itasaidia kupunguza msongamano wa wafungwa na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama za kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha utaratibu wa kurejesheana wafungwa unatekelezeka ipasavyo, mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa.

(i) Ni lazima mfungwa ambaye anakusudiwa kurejeshwa kwenda kumalizia kifungo chake kwenye nchi nyingine awe amethibitishwa pasipo shaka kuwa ni raia halali wa nchi hiyo.

(ii) Mfungwa anayekusudiwa kurejeshwa ni lazima awe amemaliza mambo yote muhimu kuhusu shauri lake. Kwa mfano, ni lazima ithibitike kwamba kama aliomba rufaa au mapitio ya shauri lake tayari yamekwishafikiwa uamuzi wa mwisho na kwamba hana shauri jingine linaloendelea.

(iii) Ili mfungwa anayerejeshwa kwenye nchi yake aweze kufaidika na programu mbalimbali za urekebishaji zinazofanyika katika nchi hiyo ni lazima wakati wa kutuma maombi angalau awe amebakiwa na muda wa zaidi ya miezi sita kabla kifungo chake hakijaisha. Si busara kuwahamisha wafungwa waliobakiza muda mfupi kwani ni gharama na hakuna faid kubwa ambayo itapatikana siyo kwa mfungwa mwenyewe tu bali hata kwa Serikali.

(iv) Mfungwa anayerejeshwa ni lazima akubaliane na uhamisho huo, iwapo hatakubaliana na uhamisho huo mfungwa wa namna hii haitakuwa rahisi kufaidika na programu mbalimbali za urekebishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunayo maombi ya kubadilishana wafungwa, lakini tumeshindwa kuyatekeleza kwa sababu hakuna sheria inayoturuhusu tuwe na mikataba ya kurejesheana wafungwa na nchi za nje. Muswada huu unaowasilishwa leo mbele ya Bunge lako Tukufu unakusudiwa kuondoa kasoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unaelezea kuhusu umuhimu wa kuwepo sheria na mikataba, utaratibu wa kutuma na kupitisha maombi, uchangiaji wa gharama, uangalizi na ulinzi wa mfungwa akiwa njiani na utekelezaji wa hukumu zilizotolewa nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza, inahusu mambo ya utangulizi. Mambo hayo ni pamoja na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii na ufafanuzi wa maneno na misamiati iliyotumiwa katika Muswada.

Sehemu ya pili ya Muswada, inaelezea utaratibu wa kurejesheana wafungwa kati ya Tanzania na nchi nyingine. Ibara ya nne chini ya sehemu hii ya Muswada inaweka utaratibu wa kuzitambua nchi za kurejesheana nazo wafungwa. Nchi hizo ni zile ambazo Tanzania itakuwa imeingia nazo mikataba ya kurejesheana wafungwa.

Katika sehemu hii ya Muswada unawekwa utaratibu wa jinsi Watanzania wanaotumikia vifungo nje ya nchi wanavyoweza kuleta maombi ya kutaka kutumikia sehemu ya vifungo vyao nchini. Utaratibu huo unajumuisha yafuatayo miongoni mwa mengine: -

(a) Wajibu wa mfungwa kuwasilisha maombi yake kwa Waziri akiambatanisha taarifa zinazohitajika.

(b) Uwezekano wa kupokelewa kwa maombi ya wafungwa wasiojiweza kwa sababu ya umri mdogo au upungufu wa utimamu wa akili yatakayowasilishwa kupitia mawakala au wadhamini wao na

(c) Mazingatio ya misamaha ikiwemo ya Rais na kutumikia adhabu nje ya magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya Muswada, inaweka utaratibu wa kuwarejesha makwao wafungwa raia wa nje wanaotumikia vifungo vyao nchini Tanzania. Ibara ya 14 chini ya sehemu hii ya Muswada huu inaelezea kuwa mara tu baada ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuingia mkataba na nchi inayotambuliwa kurejesheana wafungwa, Kamishna Mkuu wa Magereza atawafahamisha wafungwa raia wa nchi hiyo madhumuni ya makubaliano hayo ili wafungwa watakaopenda miongoni

mwao waweze kupeleka maombi yao kimaandishi kwa Waziri kuomba kurejeshwa kwao kutumikia vifungo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya Muswada huu, inaelezea utaratibu wa hifadhi na hadhi ya wafungwa wakati wanahamishwa kuletwa au kutoka nchini ambapo watahesabiwa kuwa wako chini ya kifungo halali. Sehemu hii ya Muswada inaendelea kuelezea utaratibu wa kutumikia vifungo vyao vinavyoendelea, utaratibu wa misamaha na wa kutumikia adhabu ya kifungo nje ya Magereza au aina yoyote ya msamaha ambao utatambua uhalali wa adhabu itakayotolewa kuwa imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara za 18, 19, 20 na 21 zinaweka utaratibu wa namna ya kulipia gharama za kuwasafirisha wafungwa wanaorejeshwa nchini au wanaosafirishwa kutoka nchini, namna ya kuwahifadhi wafungwa wakati wa kurejeshwa au kusafirishwa, mamlaka ya Waziri ya kutunga kanuni na mwisho marekebisho ya sheria ya magereza kuwezesha mamlaka inayoshughulikia mambo ya wafungwa nchini kuwezeshwa kupokea wafungwa kutoka nje ya nchi kutumikia sehemu iliyobaki ya vifungo vyao katika magereza ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitoweza kumaliza hotuba yangu bila ya kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Shukrani zangu pia zinamwendea Mheshimiwa Dr. Lawrence Mtazama Gama, Mbunge wa Songea na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Wote wawili katika nyakati tofauti waliongoza majadiliano katika Kamati kwa ustadi mkubwa hadi mjadala ukamalizika kwa maelewano makubwa.

Nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa uelewa wao mkubwa na michango yao yenye upeo mkubwa na uchambuzi wa kina ambayo imewezesha kufanyika kwa marekebisho yaliyoimarisha hoja ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia wadau mbalimbali hususan Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na *Julius Chambers* kwa michango yao iliyotusaidia kujaliza upungufu mdogo mdogo uliokuwepo katika rasimu ya awali ya Muswada.

Katika mtiririko huu wa shukrani sitamsahau Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wasaidizi wake ambao walifanya kazi kwa karibu sana nasi kuhakikisha kwamba Muswada huu unakidhi haja iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kumshukuru Mheshimiwa Captain John Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Bakari Mahiza, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Nicas Banzi, Kamishna Mkuu wa Magereza pamoja na watendaji wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha Muswada huu hadi nikauwasilisha Bungeni leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe mwenyewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (k.n.y. MHE. DR. JOHN S. MALECELA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba sasa nitoe kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada ya Kurekebisha Wafungwa wa Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Kurejesheana Wafungwa wa Mwaka 2004 *(The Transfer of Prisoners Act, 2004).*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuwasilisha Muswada huu mbele ya Kamati kwa ufasaha. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza wadau mbalimbali walioshiriki katika kuboresha Muswada huu wakiwemo Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, wawakilishi wa *Julius Chambers* na wawakilishi wa *Legal and Human Rights Centre.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nawapongeza Wajumbe wa Kamati hii kwa kujadili kwa makini Muswada huu. Aidha, naipongeza Serikali kwa kuzingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Wajumbe pamoja na wadau kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kwamba lengo kuu la Muswada huu ni kuwa na sheria itakayowezesha kuwekeana mikataba na taratibu za kurejesheana wafungwa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyingine. Manufaa yake ni pamoja na kumuandaa mfungwa kurudi na kuishi katika mazingira aliyoyazoea, kumpa haki ya kutembelewa na ndugu zake na kuondokana na matatizo ya lugha na kubaguliwa. Vile vile, matarajio ya kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani na hivyo kuipunguzia Serikali gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu kuwa wafungwa wengi zaidi wataondoka kuliko watakaoingia nchini kwetu. Hivi sasa wapo wafungwa wengi ambao wameomba kurejeshwa makwao. Kwa kuzingatia manufaa na sababu za kutungwa sheria hii, Kamati inaunga mkono Muswada huu uwe sheria. Hata hivyo, inapendekeza kuwa

katika kuuboresha yafanywe marekebisho katika baadhi ya ibara na baadhi ya maneno yatolewe tafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inahusu wafungwa ambao ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakaopenda kurudi nchini na raia wa nchi nyingine watakaopenda kurudi makwao. Kwa kuwa nchini Tanzania ipo Sheria ya Magereza Tanzania Bara na ipo Sheria ya Vyuo vya Mafunzo Zanzibar inahitajika ibara katika sheria hii itakayowezesha kufanyika mashauriano kati ya Mawaziri wa pande zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar wenye dhamana na kusimamia sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mfungwa husika anaweza kuwa ama mwanamme au mwanamke, Muswada uzingatie suala la jinsia kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo mawasiliano kati ya nchi na nchi na kati ya nchi na mfungwa itafaa wawepo wadhamini ambao watasaidia Serikali kutoa maelezo kamili ya habari binafsi za mfungwa na endapo atatoroka na vile vile kumsaidia mfungwa kuona kuwa anapatiwa haki zake anazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kumpa haki mfungwa ya kuelewa maamuzi yanayomhusu, maandishi yawe katika lugha anayoelewa yeye mwenyewe na wawakilishi wake na ili kulinda ubinadamu na heshima ya mfungwa asafirishwe katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako Tukufu lijadili Muswada huu na hatimaye kuupitisha kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (k.n.y. MHE. FRANK G. MAGHOBA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Frank Maghoba, Mbunge wa Kigamboni, yafuatayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Kurejesheana Wafungwa wa Mwaka 2004 *(The Transfer of Prisoners Bill, 2004):-*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Kurejesheana Wafungwa wa Mwaka 2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 43 (5) (c) Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kudososa mapungufu yaliyomo ndani ya Muswada huu, naomba nikubaliane moja kwa moja na Bwana Julius Ndyanabo wa *Julius Chambers* anaposema kuwa: "Mfumo wa sheria katika nchi unaweza kuwa ni mhusika ndani ya Muswada huu wa sheria na unaweza kuwa ni tofauti." Kwa maana hiyo, kosa katika sheria za nchi yetu inawezekana lisiwe kosa kwa nchi nyingine. Mfano

Mjamaika akikutwa na bangi hapa Tanzania ni kosa, lakini kwa Jamaica ni kitu cha kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba wahusika walipe suala hili ufumbuzi wa kina ili kuondoa mtafaruku. Kama mfungwa anaomba arudishwe kwao wakati kwao hilo siyo kosa la kifungo, hiyo nadhani jamii lilipotendwa kosa itakuwa haikutendewa haki na ni bora kwanza amalize kutumikia kifungo ndipo aondoke kwenda kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 5 (1) (b) wakati nchi inaomba mfungwa arejeshwe na kutumikia kifungo nchini kwao. Katika Muswada huu sijaona sehemu ambayo inaeleza kwanza uchunguzi ufanywe kwenye nchi inayoomba mfungwa apelekwe kama sheria za magereza yao yanafuata misingi ya haki za binadamu au la. Hicho ni kitu muhimu kabla ya kukubali kubadilisha mfungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya Muswada huu wa sheria, inampa Mheshimiwa Waziri mamlaka au uwezo wa kukubali kumtoa mfungwa Gerezani na kumsafirisha akiwa chini ya ulinzi kwenda kwenye nchi husika ya mfungwa huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadri ninavyoelewa, Mahakama ikishatoa hukumu na mfungwa kwenda Gerezani, basi chombo au mtu yeyote mwenye uwezo huo wa kumtoa mfungwa ni Mheshimiwa Rais au Mahakama yenyewe baada ya kupitia upya kesi ya mfungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaomba kueleweshwa sasa kati ya Rais na Mahakama Mheshimiwa Waziri anasimama wapi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfumo wetu wa Muungano kuna mambo yaliyo ya Muungano na yasiyo ya Muungano, lakini yapo mambo ambayo robo yamo ndani ya Muungano na robo tatu hayamo katika sehemu ya Muungano.

Kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Ndani ni ya Muungano, lakini Chuo cha Mafunzo Zanzibar si cha Muungano. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie ni vipi mfungwa anayeombwa kurejeshwa kwao kwa sheria hii na mfungwa aliyefungwa kwa sheria ambayo si ya Muungano, Chuo cha mafunzo ambacho si cha Muungano, wakati mwenye mamlaka ya kumrejesha mfungwa kwa sheria hii ikipita ni Waziri wa Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaunga mkono upitishwaji wa Muswada huu wa sheria lakini inamwomba Mheshimiwa Waziri afanye majumuisho ya sheria inayotumika Tanzania Visiwani na hii inayopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wasemaji wote wakubwa kwa Muswada huo wamemalizika. Sasa hapa ninao wachangiaji watatu, bado nafasi iko wazi kama kuna watu wangependa kuchangia Muswada huu. Hapa ninao Mheshimiwa

Profesa Daimon Mwaga atakuwa wa kwanza, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali na Mheshimiwa Semindu Pawa. Sasa ninamwita Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kidogo huu Muswada wa Kurejesheana Wafungwa.

Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha Muswada huu vizuri na kwa kueleweka. Kwa kweli ni Muswada mfupi, vifungu vyake viko wazi kabisa sina sababu kwa nini nisiunge mkono mia kwa mia. Kwa hiyo, naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa niboreshe maeneo machache kwa lengo la kuimarisha Muswada huu. Katika ukurasa wa 5 au ninaweza kusema ibara ya 5(4) hapa imezungumzwa kwamba, mfungwa anaweza akahamishwa chini ya miezi sita kwa sababu maalum au kwa mazingira maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzifahamu hizo sababu maalum kwa Kiingereza wanasema *exceptional circumstances,* ni zipi? Ingekuwa bora Muswada huu ukaziorodhesha baadhi ili kuondoa kutofautiana katika kutafsiri. Hilo la kwanza.

La pili, ibara ya saba inazungumza juu ya mfungwa ambaye alikuwa kichaa alipofanya makosa na namna yake ya kumrejesha. Hapa sheria haitoi nafasi au Muswada huu hautoi nafasi kwa Serikali kuomba mfungwa wa namna hiyo arejeshwe Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ibara ya 5(b) iko wazi kabisa kwamba, nchi inaweza ikaomba mfungwa ahamishwe kutoka nchi moja kuja nchini Tanzania. Lakini inapofika kwa huyu mfungwa ambaye alifanya makosa akiwa hana akili timamu, sheria au Muswada huu hautoi nafasi hiyo.

Naomba irekebishwe hapo ili Serikali yetu iwe na nafasi ya kuomba wafungwa waliofungwa nje, kwa sababu ya hali ya kutokuwa na akili timamu. Kwa hiyo, hilo jambo la pili nilikuwa naomba liboreshwe katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, liko katika Ibara ya 18 (3) inazungumzia juu ya gharama za kumsafirisha mfungwa wa namna hii. Hii Ibara ya 18 (2) inasema: "Gharama hizi zitalipiwa na mfungwa mwenyewe." Lakini kifungu cha 3 kinasema: "Gharama za kumsafirishia mfungwa zitakuwa ni deni la Taifa kwa Serikali."

Sasa mimi nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri, aseme ni lipi hasa, mfungwa atajigharamia mwenyewe kujirejesha au Serikali itagharamia na kama litakuwa ni deni kwa Taifa, ulipaji wake utakuwaje? Je, utazingatia uwezo wa mfungwa huyu au vipi? Kwa kweli katika vifungu viwili hivi inahitajika kuviweka wazi zaidi ili ijulikane huyu mtu anayetaka kurejea anafanyafanyaje katika kujigharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne katika Ibara ya 19 na Ibara zingine zote zilizobaki, nilikuwa nashauri kwamba Serikali, yetu ione uwezekano wa kuwekeana mikataba na nchi zile zote ambazo Watanzania wengi wanaishi kule wanafanya kazi kule bila kusubiri kwanza wafungwe. Sisi tunajua uwezekano wa kufahamu hilo upo kabisa kwamba nchi gani Watanzania wako kule kwa wingi wanaishi, wanafanya kazi. Sasa iwe ni nchi za mwanzo kabisa kuwekeana mkataba nazo ili endapo wananchi wetu kule wakifanya makosa basi wajue wana haki ya kurejea kuja kumalizia vifungo vyao nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nilikuwa nashauri kama ikiwezekana kuanzishwe Masjala katika Idara ya Magereza Makao Makuu ya wafungwa wote walio nje ya nchi ili tuwatambue na tuwe na kumbukumbu kamili za Watanzania waliofungwa nje na tuwe na Masjala yake ili pamoja na mambo mengine kuangalia na kufuatilia ustawi wa vifungo vyao na pengine tunapoona kuna haja ya kuomba warejee Tanzania basi tuwe na mahali pa kuanzia, tuwe na kumbukumbu nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi baada ya kusema hayo, huu Muswada kama nilivyosema ni mfupi, uko wazi, lakini ningependa kuboresha katika maeneo hayo niliyoyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa taarifa aliyotoa leo asubuhi, kwa kweli hakuchelewa, siku sita hazikuwa ni kidogo kwa taarifa nzito kama ile ya Serikali, kama ilitokea labda kama alichelewa, kwa kweli ilitakiwa atoe taarifa sahihi ambayo haitagongana na taarifa ambayo tutaiona huko mbele ya safari. Kwa hiyo, nataka nimpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwamba yale yote ambayo tulielekezana kule kwenye Kamati ameyaweka kwa faida ya Taifa hili. Lakini vile vile niipongeze Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kweli watendaji wake wamefanya kazi kubwa sana hata Muswada huu Mheshimiwa Waziri akauwakilisha kirahisi kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Kurejesheana Wafungwa ni muhimu sana kwa Taifa letu na hauwezi kutuathiri kwa sababu tukiangalia kwa mujibu wa taarifa tunaambiwa kwamba historia inayoonyesha kwamba Marekani au nchi za Ulaya Magharibi wanaweza kuingia katika nchi hii na zile za *Scandinavian Countries* ambazo zimeanza kwenye miaka ya 1963 utakuta kuna miaka 44 mpaka leo kwa nchi za Ulaya Magharibi zina miaka kama 41 kwa *Scandinavian Countries.* Kwa hiyo, Muswada huu ni muhimu sana kwa Taifa. Kwa hiyo, mimi naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeunga mkono Muswada huu pamoja na marekebisho kwa sababu tunasema kwamba wafungwa wote walioko nje ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu wote Watanzania walioko nje wamesafiri aidha kwa *passport* ya Tanzania na kwa Uraia wa Tanzania.

Kwa hiyo, kile kipengele alichokiweka kuonyesha kwamba Waziri wa Muungano wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Waziri anayehusika na Magereza Zanzibar, wanaweza wakazungumza, imesababisha nisimame ili kuunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Vinginevyo kwa kweli usingelileta kuelewana kwa sababu lazima ingeleta mgongano mkubwa ambao sasa hivi hali ya nchi yetu umeiona wenzetu wanatafuta sababu ndogo ambayo inaonyesha labda kiubaguzi.

Kwa hiyo, natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa hii aliyoiweka wazi kabisa na akaweza kufanikisha kuleta Muswada huu na hautakuwa na malumbano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu katika sehemu ya 4 ya Muswada huu unaelezea utaratibu wa hifadhi na hadhi ya wafungwa kutoka au kuletwa nchini kuwa watahesabiwa wako chini ya kifungo halali. Kwa hiyo, nina imani kwamba Waziri ataangalia uzito wa yale makosa ambayo kwetu sisi ni makosa na kwa wenzetu si makosa.

Lakini vile vile ule uhalali na uangalie na ule usalama wao mle njiani. Kama ataleta mfungwa ndani ya nchi ya Tanzania na ni mfungwa halali vile vile tupate taarifa mle njiani kwamba asije akawa amesumbuliwa na yale mataifa ambayo tumebadilishana wafungwa.

Lakini kubwa zaidi kwenye Muswada huu ni kulinda haki za binadamu, pia vile vile kuondoa msongamano wa magereza, tuitumie nafasi hii kwa wafungwa wote wa nje walioko katika Taifa letu la Tanzania waweze kuondoka ama wapewe muda mfupi sana.

Kwa hiyo, nimesimama hapa kuongezea nguvu kwamba mara tu Waziri atakapopata ruhusa ya sheria hii kazi ya kwanza ni kuondoa wafungwa wote wa nje walioko katika nchi yetu kuziandikia zile nchi zao ili waondoke mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nichangia katika Muswada huu ni juu ya wafungwa watoto kuchanganywa katika Magereza na watu wazima. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kuzingatia kanuni na sheria ya kimataifa ambayo inaelezea kuhusu wafungwa watoto kuchanganywa na watu wazima.

Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri ningekuomba sambamba na Muswada huu ili kutimiza haki za binadamu tuweze kuwanusuru watoto wengi ambao wako katika magereza yetu ambao wamefungwa na watu wazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa ziarani Kagera, tumewakuta watoto wadogo wengi sana wamefungwa na watu wazima, wengine wako mahabusu. Kwa hiyo,

sambamba na hili ambalo tunasema kwamba ni haki za binadamu tuliangalie kwa uzito wote ili kuiomba Serikali ijenge Magereza maalum na ya muhimu sana ili kuwanusuru watoto hawa na magereza ya watu wazima ili tusiwaingize watoto katika migogoro ambayo haina maana. Ikiwezekana Serikali itenge fedha maalum kwa kutumia JKT ili ijenge Magereza haraka sana ili tuweze kuwaondoa watoto wadogo katika Magereza yale ya watu wazima ili waweze kutumikia yale magereza yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na namuunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuchangia machache kuhusu Muswada huu wa Sheria wa Kurejesheana Wafungwa, neno la msingi ni kurejesheana.

Sasa kuna mambo machache ya kubainishwa kwa sababu katika utaratibu wa nchi duniani zilizopata Uhuru na zile ambazo ziko katika maeneo mbalimbali tukaungana kwa maeneo kama vile Nchi za Jumuiya ya Madola, *SADC, East Africa, African Union* kwa ajili ya malengo maalum.

Lakini kwa haki za binadamu liko ndani ya mikono ya dunia, Serikali za nchi zilizoko madarakani ili kuangalia uwezekano kwamba yale ambayo yanakubaliana katika kuhakikisha kwamba wananchi wao wanapata haki, basi wakubaliane ili kuweza kuyafikisha mahali ambapomakubaliano hayo yatatekelezwa. Hivyo basi nchi ambazo zinakubaliana zinawekeana mikataba na baadaye zitunge sheria ili kuweza kuziwasilisha na kuweka ndani ya tovuti zikaonekana dunia nzima. Huu ni utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kuna mchangiaji mwingine kule. Ulikuwa unanichanganya kidogo Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa nazungumzia utawala bora, ahsante nashukuru sana. Ningeomba Waziri awe mwangalifu kwa suala kama hili nyeti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, endelea.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nilipokuwa narekebisha mambo haya nilikuwa naangalia mfumo wa dunia kwa ujumla ili mataifa yao yatunge sheria zilizo nzuri na zisimamiwe vizuri ili kusudi wananchi wao wafaidike na sheria hizo. Sheria iliyokuwa mbele yetu inakidhi hoja hiyo, ila nilikuwa nimechanganyikiwa neno kusema kubadilishana, unapobadilisha siyo kwa *value* ile ile kwamba una wafungwa 10 na nchi ile ambayo unawabadilisha walete wafungwa 10, hayo ni mateka siyo wafungwa.

Hii haizungumzii jinsi ya kurudishiana kwa *value, quantity and quality,* bali inazungumzia maeneo ambayo ni mahususi yaliyotajwa kwenye Ibara ya 3, 5 katika ukurasa 38 kama alivyobaini Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga. Sasa neno kubadilishana lilileta fikra tofauti kidogo kabla haujasomwa Muswada huu.

Lakini napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwamba katika kikao chenu Wizarani tarehe 24 Januari, 2004 chini ya Mwenyekiti, Bwana Bakari Mahiza na

aliyekuwa Katibu wa kikao hicho Bwana Mhogole, kulikuwa na wajumbe 8 wameorodheshwa, kwa kuzingatia muda siwezi kuwasoma wote kwamba mlibainisha taratibu za msongamano wa wafungwa katika nchi yetu ndani ya Magereza na hiyo ambayo imeonyesha kabisa kwamba Magereza yetu vile vile hayakidhi kupokea kwa sababu yana msongamano na kuna jedwali namba nne linaonyesha matatizo na ukubwa huo na akatoa mapendekezo jinsi ya kuchukuliwa hatua.

Kwa mfano, mpaka tarehe 1 Januari, 2004 katika kiambatanisho namba (k)(1) imeonyesha kabisa kwamba Magereza yetu yana idadi ya wafungwa wengi karibu asilimia 304 kuliko inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilibainisha maeneo machache tu kwa mfano Bukoba uwezo wa Gereza kisheria linachukua wafungwa 804, lakini walioko tarehe ile ambayo nilitaja juu ya karatasi yangu siyo juu ya Bunge ni wafungwa 1,181, Ukonga uwezo wake ni wafungwa 735, lakini walioko ni wafungwa 2,329, Arusha uwezo wake ni wafungwa 400 lakini walioko Gerezani ni wafungwa 1,838.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lindi uwezo wake ni wafungwa 44 lakini wako wafungwa 603, Morogoro uwezo wake ni wafungwa 90 lakini wako wafungwa 444. Hiyo naeleza kabisa hata kama kubadilishana huko maana yake ni kuwarudisha Watanzania kuja kwenye Magereza ya Tanzania watabanana katika Magereza hayo hayo niliyotaja katika *volume* na *quantity* ambayo nilikuwa nimenukuu hapo juu. Hali hii itaongeza gharama, vurugu za baridi, kashfa za kina, maisha ya kutengana ndani ya magereza hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza vile vile gharama kwamba kusafirisha mfungwa huwa ni nchi anakotoka kwenda kwenye nchi anakoelekea kwamba itakuwa gharama ya huyo mfungwa mwenyewe. Hii itarudisha wafungwa wenye uwezo kuwapeleka katika nchi zao.

Kwa hiyo, inakuwa ni *transferable* ya watu ambao wana uwezo na vile vile hapa nime-*question* kwa wafungwa ambao Watanzania wa aina mbili, tuna watu wenye uraia mara mbili, tuna Watanzania na kuna Watanzania kwa nasaba *(Tanzania by decently)* anafungwa leo, Muswada huu tunapitisha anakuambia yeye ni raia wa Uingereza anakuonyesha *passport* anapelekwa Uingereza kumbe alikuwa ni Mtanzania wa hapa hapa.

Kwa hiyo, Kamati itakayoundwa na Waziri kwenda kwa kina *deeper analytical charity, prevailing reality* ya wahalifu wa aina hiyo na imeonyesha jedwali pale kwamba jumla kuu ya wafungwa ni karibuni wafungwa 26,620 na ukichanganya na mahabusu pamoja, mahabusu 18,111 utapata jumla ya wafungwa 45,205.

Sasa mahakama ni mbalimbali lakini Gereza ni moja hakuna wafungwa ambao wanakwenda Gereza la Mahakama ya Mwanzo pamoja hata ukiwaambia kwamba wewe ni Mahakama ya Mwanzo unafungwa miezi mitatu, nakwenda kwenye Gereza moja, watu wanasema Mahakamani kuna sheria, wanasema hakuna haki, ziko haki kwa sababu *case Complainant (CA), Accused (A), Struggle by Explaining (SE),* atakaposhindwa tu pale basi unakuta anapelekwa magerezani.

Halafu muda ambao mfungwa anatakiwa arejeshwe au apelekwe wanasema usizidi miezi sita. Kuna wafungwa wa maisha, kuna wafungwa wa zaidi ya miaka 30, lakini anatakiwa afungwe halafu alipe faini na alipe fidia wanasema vyote viwili. Hapa *transfer* inakuwaje kwa mambo kama haya? Naomba tupate ufafanuzi wa vitu vidogo vidogo kama hivi. Hicho ndicho kipimo cha mchango wangu kwa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Muswada ulioko mbele yetu.

Kwa kweli napenda kumpongeza Waziri kwa kuandaa Muswada huu ambao unalenga katika kuzingatia haki za binadamu kwa kuwarejesha wafungwa katika nchi zao walipotokea ili waweze kupata huduma ya kuonana na ndugu zao na kutumikia kifungo katika nchi zao. Lakini nina maneno mawili/matatu ya kutafuta ufafanuzi.

La kwanza ni lile la mfungwa kutumikia hukumu aliyopewa, je, ni wafungwa wa kiasiasa ama labda wale wa vita? Wako wafungwa wa kisiasa na wako wafungwa wa kivita *(prisoners of war).* Kama ni hivyo, je, huyu mfungwa anaporejeshwa katika nchi yake ataendelea kutumikia kifungo kile cha nchi yake au kifungo cha pale ambapo amehukumiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu katika sehemu zingine utakuta kwamba mfungwa kama amepewa hukumu labda ni wa kisiasa na anarejeshwa katika nchi yake kwa ridhaa yake mwenyewe labda kwa sababu anapenda kwenda kutumikia *(sentence)* hukumu yake nchini kwake wakati mwingine inaweza ikatokea badala ya sisi kumsaidia kwa kuzingatia haki za binadamu, tukampeleka machinjioni. Je, katika mazingira ya namna hiyo, kuna *assurance* gani kwamba mfungwa huyu anaporejea katika nchi yake ataendelea ku-*serve sentence* ile aliyopewa katika nchi ile alipofanya uhalifu na kuhukumiwa?

Lingine ni lile la nchi inayompokea yule mfungwa, inatoa *assurance* gani kwamba mfungwa yule anaporejeshwa pale wataendelea kuzingatia hukumu iliyotolewa katika nchi ile aliyotoka? Ningependa Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia kutupatia ufumbuzi wa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu adhabu zinazohusu labda malipo na sehemu zingine wana adhabu za ku-*cane* (viboko) na nchi zingine hazichapi viboko. Je, kama nchi moja imetoa hukumu ya viboko mfungwa anapomaliza muda wake wa kifungo na nchi nyingine haina utaratibu wa viboko, naomba kufahamu iwapo upo utaratibu wa nchi hizi kukubaliana katika kubadilishana wafungwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mchango huo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Muswada ni mzuri kwa sababu unalinda haki za binadamu. Nampongeza Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, sina mwingine wa kuchangia sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aweze kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa tena fursa nyingine ya kuja kufanya majumuisho juu ya mjadala huu mfupi, kuhusiana na Muswada niliouwasilisha hivi punde unaohusu Kurejesheana Wafungwa na Nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuunga mkono Muswada huu na michango yao ya kuboresha hapa na pale. Shukrani zangu nazitoa tena kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama toka walivyotusaidia ndani kule kwenye Kamati na mpaka hapa katika uwasilishaji wao ambao kwa kweli kwa kiasi kikubwa wamenisaidia sana kutoa ufafanuzi wa namna tulivyobadilishana mawazo mpaka tukafikia hatua ya kufikia Muswada huu kuwasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada umebahatika kupata wachangiaji sita wa kuzungumza na mmoja kwa maandishi. Waliochangia kwa kuzungumza kwanza ni Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, ambaye amezungumza kwa niaba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa John Singo. Mchangiaji pekee wa kimaandishi ni Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa. Wote hawa nawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, alizungumzia mambo matatu ambayo pengine yanajitokeza kwa kutaka maelezo zaidi. Suala la mashauriano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kweli katika majadiliano kwenye Kamati ndipo lilipojitokeza lakini kama mtakavyoona wale Waheshimiwa Wajumbe, watakapokuwa wameshaona kwenye *schedule of amendment* hilo tumeshalifanyia kazi. Kwa hiyo, ule wasiwasi kwamba kutafanywa kazi upande mmoja tu na mwingine labda ushitukizwe haupo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naib Spika, zingatio la jinsia hali kadhalika tumelizingatia katika Muswada. Ombi la mawasiliano na mfungwa kuwa yawe kwa lugha anayoielewa hayo ni miongoni mwa mambo ambayo tutajazia kwenye kanuni zetu.

Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, naye alizungumzia mengi akazungumzia makosa ambayo kwa upande mmoja baina ya nchi zile zinazorejesheana wafungwa upande mmoja ni kosa na upande mwingine si kosa.

Muswada umejitahidi kulizingatia hilo, lakini hayo ni miongoni mwa mambo ambayo yatazingatiwa wakati Waziri anazingatia ombi la mwombaji. Kama patakuwa na hali ya mkanganyiko kwa kosa ambalo pande moja ni kosa lakini upande wa pili si kosa anaweza alikataa kabisa ombi lile. Kubwa ni kwamba hata taratibu zote zilizowekwa Kimataifa ni kuhakikisha uwiano mzuri ni kwamba mtu anamaliza adhabu yake kama

vile ambavyo ilitolewa kwenye Mahakama ya nchi ambayo iliyokuwa imemfunga aliyoanzia nayo adhabu yake aliyoitoa kwa kadri inavyowezekana hilo ndiyo hitaji la msingi. *(Makofi)*

Lakini ni suala la kupima kuna mambo mengine madogo madogo kama lile la viboko nalo ni miongoni mwa mazingatio bila shaka ni kama nchi ambayo pengine kwa mfano mfungwa amefungwa nchi ya nje na amepigwa viboko kwanza kabla hajaingia, halafu vimewekwa vingine vya kuja kumalizia akitoka, sasa kama kwetu hakuna adhabu ya viboko basi katika mawasiliano unaweza tu ukawaambia kwamba hivyo viboko vyenu mmalizieni kabisa huko maana huku hakuna adhabu ya viboko, akija huku akimaliza muda wake basi anakwenda zake tu. Kwa hiyo, ni miongoni mwa mambo ambayo yatakuwa yakizingatiwa kwenye majadiliano. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uchunguzi wa ndani ya nchi halimo, kabla hatujafikia uamuzi wa kumrejesha mtu na hili nadhani limezungumzwa pia mwishoni na Mheshimiwa John Singo kwa kiasi fulani.

Ni kweli inawepo hofu kwamba akiachiwa mfungwa ukimruhusu akienda katika nchi na mkawa mna wasiwasi kwamba hatatendewa haki kwa kiwango kile ambacho angetendewa katika nchi kwa mfano yetu nadhani hayo ni miongoni mwa mambo ambayo yanazingatiwa na ndiyo maana imewekwa humu kwenye kipengele cha sheria.

Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa ambaye amehoji nafasi ya *AG* kwa nini ameingizwa *AG* badala ya Mahakimu? Hii ndiyo nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mawasiliano ya Waziri kabla hajatoa maamuzi miongoni mwa mambo yatakayozingatiwa katika mawasiliano hayo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kupima kama ni kweli akiruhusiwa huyu mfungwa kwenda kule atatendewa hiyo haki hasa akiwa yumo mwetu na bila shaka itatokea nafasi katika mawasiliano hata kupewa fursa na mwenyewe mfungwa kupewa dhirio kwamba unaweza kwenda huko ukakosa haki.

Sasa yote hayo yatapimwa kama ata- *insist* na kama sisi tutaridhika kwamba haki itakuwepo na tumepata *insurance* kwa Serikali inayohusika tunaweza tukaruhusu. Lakini kama hatukuridhika na *insurance* au uhakika ambao tutakuwa tumepewa na upande wa pili ombi hilo linaweza likakataliwa. Kwa hiyo, huo utaratibu mzima uliowekwa katika sheria ambao si mwepesi wote lengo lake ni kutoa nafasi ya mawasiliano na mashauriano kama hayo.

Halafu alielezea Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, aliona kama Waziri anamtoa mfungwa. Nafasi ya Waziri kwenye sheria hii ni kuruhusu mfungwa kama ameomba arejeshwe katika nchi yao kama ni wa kwetu au kuruhusu kama ni Mtanzania aliyeko nje arejee au kuja kuendelea kumaliza kifungo chake nchini Tanzania. Sheria hii haimpi uwezo Waziri wa kutoa msamaha wa kifungo hata kidogo. Ni kuhakikisha kwamba ile *process* ya adhabu inaendelea kama ni ndani au nje ya nchi. Kwa hiyo, hakuna mgongano katika hilo mwenye uwezo wa kutoa misamaha kama hiyo kwa mujibu wa katiba yetu ni Mheshimiwa Rais peke yake.

Kuhusu wafungwa wa Zanzibar au kuhusiano suala la Zanzibar ni kama nilivyokwishaelezea tumefanya marekebisho hayo kuhakikisha yapo mawasiliano na mawasiliano kwa kweli hayatahusu kuhoji sheria, kama sheria ya Zanzibar au vipi status ile ya sheria ya Zanzibar hata kidogo ni kama je, huyu mfungwa aliyeko zanzibar ambaye ameomba arejeshwe nchi kwao Mheshimiwa Waziri, anayehusika na hifadhi ya wafungwa au wahalifu kule Zanzibar anakubali? Kama anakubali sawa, hakubali ombi linakataliwa au mfungwa aliyeko nje ambaye ni mkazi wa kudumu wa Zanzibar anataka arejeshwe nchini Tanzania mawasiliano na Waziri anayehusika na hifadhi ya wahalifu kule Zanzibar ni kama arejee au asirejee. Hatuzungumzii sheria ya wafungwa wa Zanzibar au sheria ya Vyuo vya Mafunzo ya Zanzibar hilo si suala la Muungano na bila shaka tutakuwa tunazungumza nao kabla ya kuanza utaratibu wa utekezaji tutakuwa na mazungumzo nao katika kuweka utaratibu hasa katika kutunga kanuni na maelewano kama hayo.

Sasa ni wao wenyewe tena kuamua kama watapenda kuzirekebisha sheria zao au zibaki kama zilivyo, hilo ni lao wenyewe na wala haliathiri utekelezaji wa sheria hii. Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, alizungumzia urejeshaji wafungwa waliobakisha chini ya miezi sita. Akataka kujua hizo sababu maalum ni zipi zitajwe. Hazikutajwa makusudi katika Sheria hii kwa sababu si rahisi kuzitabiri bila ya Muswada ni kwamba chini ya miezi sita pasiwepo na uhamisho. Lakini sasa linaweza jambo ambalo si la kawaida. Wakuu wa Nchi wanaweza wakaombana, Kiongozi wa nchi anaweza akamwomba Rais wetu au Rais wetu anaweza akamwomba kiongozi mwenzake wa nchi za nje. Sasa kama mmefunga kabisa mlango kama huo inakuwa tena haitaweza kulitekeleza jambo kama hilo na mengine ya aina hiyo yanayoweza kutokezea.

Halafu alizungumzia kwamba Muswada hautoi nafasi kwa wafungwa wasio na akili timamu. Muswada umetoa hiyo fursa kwa wale wote, tumeiweka kwa namna ambapo kama mfungwa ni mtoto mdogo au ana upungufu wa akili anaweza kuwakilishwa. Tumezungumzia uwakilishi pale, atawasilisha ombi kwa Waziri kwa niaba ya mfungwa mwenye sifa kama hizo kwamba ni mtoto mdogo au mwenye upungufu wa akili. Kwa hiyo tume-*assume* kwamba wapo na watapenda kuitumia haki hiyo na wakipenda kuitumia ipo nafasi.

Kuhusu suala la kurejesheana gharama za wafungwa, kwenye Ibara ya 18 pale nadhani imezungumzia suala hilo la gharama. Pale tumeeleza kwamba gharama zitabebwa na mfungwa mwenyewe. Lakini pia katika sehemu hiyo hiyo imewekwa fursa kama mfungwa hana uwezo, kama mfungwa ana ndugu zake hawana uwezo, Waziri anaweza akaruhusu Serikali zitumike gharama za Serikali za kumrejesha. Sasa pale palipozungumziwa deni, ni kwamba tunatarajia utaratibu wa kawaida. Wahusika wote, mfungwa pamoja na wadhamini wake katika utaratibu wa kawaida, inatarajiwa kwamba Serikali itagharamia ule usafirishaji lakini baadaye fedha zile zirejeshwe Serikalini. Ndiyo maana lilivyozungumziwa lile deni.

Kwa hiyo, likishakubalika baada ya mawasiliano, Serikali pamoja na mfungwa au wadhamini wake, kwamba gharama watazirejesha wakatiliane saini mikataba kwa mujibu

wa Kanuni zitakazokuwa zimetungwa. Serikali kwa urahisi kwa kurahisisha lile zoezi itagharimia halafu baadaye watatakiwa wahusika kuzirejesha.

Halafu kwamba Tanzania isisubiri watu wafungwe ndiyo wawekeane mkataba na nchi fulani, nadhani hii ndiyo *spirit* ya huu Muswada. Maadam tulikuwa hatuna mkataba na nchi yoyote na wafungwa tayari wapo, kwa hii ya mwanzo bila shaka itakuwa tutaanza baada ya wafungwa kuwa wapo. Lakini baada ya sheria kupita itaanza tu *series* za mazungumzo na nchi hasa kutokana na mikataba hii ya kimataifa ambayo inatuelekeza huko, kwa mfano nchi za *SADC* ambazo tayari zimeelekea huko. Bila shaka ile *protocol* ikishapita tu nchi zote *automatically whether* una wafungwa kule nchi nyingine au huna *automatically* zitaanza mazungumzo na kutiliana mikataba ya kurejesheana wafungwa.

Kwa hiyo, hatutasubiri kwamba mpaka watu wafungwe kwanza ndiyo tuingie mikataba na ninakubaliana na ushauri wa kuweka *inventory* ya Watanzania wote walioko katika Magereza ya nchi za nje. Nadhani sasa kwa utaratibu huu wa sheria ambayo tunajaribu kuiweka hapa sasa hivi, itawezekana kutokana na haya mawasiliano. Sasa hivi tutakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuwajua Watanzania walioko Magereza nchi za nje kuliko hivi sasa.

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, alizungumza mengi ambayo kimsingi tulikwishakubaliana kwenye Kamati na akaomba kwamba wasifungwe pamoja na watu wazima. Bila shaka hilo si sehemu ya Muswada lakini ni miongoni mwa mikakati ambayo tayari inafanyiwa kazi na Tume zetu za Kamati za Bunge, moja ya Ulinzi na Usalama na ile ya Katiba, Sheria na Utawala.

Hivi karibuni zilikuwa na kikao cha pamoja kutwa nzima tulijadili suala hili la matatizo yetu ya Magereza, msongamano pamoja na namna wanawake wanavyotunzwa katika Magereza na namna watoto wanavyotunzwa. Kwa hiyo, hayo ni miongoni mwa mambo ambayo tutayafanyia kazi tu, nje ya utaratibu wa Muswada huu.

Mheshimiwa Semindu Pawa, alitusaidia hapa kutoa ufafanuzi wa istilahi. Namshukuru, ndiyo maana hatukutumia hilo neno kubadilishana. Kubadilishana ni mateka wa kijeshi, lakini hapa tumesema ni kurejesheana ni nchi inarejesha wafungwa ili wakaendelee na shughuli zao. Halafu wakawa vile vile na wasiwasi kwamba watu wasiokuwa na uwezo Sheria hii itakuwa inawakandamiza. Nadhani nimeshatoa maelezo kwamba ipo *provision* ndani ya Sheria kwa wale ambao hawatakuwa na uwezo.

Lakini kwa maombi mengi ambayo tunayo hivi sasa ambayo hatujaweza kuyatekeleza kwa sababu hatuna sheria hii. Mengi kwa kweli ni ya watu wenye uwezo na ndiyo maana *thrust* tukaiweka kwenye watu kujigharamia au kugharimiwa na wadhamini wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoa wale wanaozamia meli, lakini wengi wanaokwenda kule kwa taratibu za kawaida kwa kweli ni watu wenye uwezo. Kwa hiyo, ni vizuri kwa wakati inapowezekana mzigo huu tukawagana Serikali na familia zao. Halafu akaulizia kuhusu *transfer* au urejesheanaji wafungwa kwa wale wenye *fine* au

adhabu nyingine, nalo nimeligusia awali kwamba hapa zaidi tunatazama wafungwa walioko magerezani, bila na vifungo vya nje ya magereza kama *Parole* nazo zimewekwa kwenye utaratibu. Lakini *fine* ya kurejesha haiishi, kwa sababu *fine* atalipa kabisa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama ile nchi ambayo inamwondoa yule mfungwa kumpeleka kwingine kama hawataitaka fine yao kabisa sidhani kuwa huku nchi nyingine itakuja kutaka kuidai na aghalabu ukilipa *fine* hufungwi. Kwa hiyo, maadam atakuwa amefungwa suala la *fine* litakuwa halipo. Sasa hizo adhabu nyingine kama za viboko ni kama nilivyokwishazungumzia mapema.

Mwisho ilikuwa Mheshimiwa John Singo, alizungumzia mambo mawili makuu ambayo nayo kwa kiasi wakati nilipokuwa nikiwajibu wengine itakuwa nimeyagusia. Baada ya ufafanuzi huo na majumuisho hayo sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria wa Kurejesheana Wafungwa usomwe mara ya pili. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kujeresheana Wafungwa wa Mwaka 2004**
***(The Transfer of Prisoners Bill, 2004)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu tu nataka ufafanuzi tu kwenye hiyo Ibara ya 14 (1) na ya (2) hapa nimeona kimetumiwa cheo cha *Commissioner of Prisons.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda nieleweshwe pengine kuna mabadiliko kwamba kiongozi wa chombo hicho sasa siyo *Principal Commissioner* ni Kamishna au pengine inatumika Sheria ya mwaka 1967 wakati wanageuza cheo kuwa *Principal Commissioner* kule haikubadilishwa. Kwa hiyo, ndiyo maana tunafuata hapa. Nilitaka tu ufafanuzi hapa. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa William Shellukindo kwa kuliona hilo. Kwa hiyo, nakubali sehemu hii tufanye marekebisho apitie huu wadhifa wa *Principal Commissioner of Prisons.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kujeresheana Wafungwa wa Mwaka 2004**
***(The Transfer of Prisoners Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba radhi nilitaka kufanya haraka sana, nadhani nina hamu sana. Naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima limeupitia Muswada wa Kurejesheana Wafungwa wa mwaka 2004 *(The Transfer of Prisoners Bill, 2004)* kifungu kwa kifungu na kuupitisha pamoja na marekebisho yaliyofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Muswada huu ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI, NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, kwa shughuli za leo hapa ndipo tumefikia mwisho. Kabla sijaahirisha Shughuli za Bunge, niseme tu nimepewa vi-*note* vingi kuhusu Muswada ule ambao unakuja baadaye wa Fedha.

Nimepata vi-*note* vikisema, huu Muswada ni *technical* sana kwa hiyo tungekuwa na nafasi ya Semina ili tuelimishwe.

Lakini nilishauriana na upande wa Serikali, wakasema kesho bado Kamati inaendelea na kazi, kwa hiyo, kwa wale ambao wangefikiri wanapenda kuchangia zaidi au kujielimisha zaidi kwenye Muswada, basi kesho wanaweza kuhudhuria kikao cha Kamati ambacho ni wazi tu kwa Mheshimiwa Mbunge yeyote kwenda kushiriki katika majadiliano ingawa kikanuni hutapiga kura kwa maana kama kutakuwa na migongano katika kufikia uamuzi.

Lakini tunayo ruhusa ya kushiriki kikamilifu. Kwa hiyo, kesho nimeambiwa Muswada huu bado utaendelea kwenye Kamati. Kwa hiyo, unaweza kupata nafasi ya kwenda kushiriki.

Baada ya maelezo haya sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.16 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne Tarehe 20 Aprili, 2004 Saa 3.00 Asubuhi)*